

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 26 Mei, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO  
WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 278

### **Tatizo la Maji Musoma Vijijini**

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI** aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo kubwa la maji katika Wilaya ya Musoma Vijijini hasa vijiji vya Kabulabula, Bugoji, Kangetutya na Saragana. Aidha, visima vilivyochimbwa na wanakijiji hao vinakauka wakati wa kiangazi.

Je, ni lini Serikali itahakikisha programu za maji zinapelekwa na zinatekelezwa kwa umakini katika Wilaya ya Musoma Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bita Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli visima vingi hasa vilivyochimbwa na kufungiwa pampu hukauka wakati wa kiangazi na hivyo kuathiri upatikanaji wa huduma katika maeneo husika. Sababu kubwa ni mabadiliko ya tabianchi hali inayosababisha maji kupatikana katika kina kirefu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua changamoto hiyo, Serikali kuititia Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Maji (*WSDP II*) imeanza kufanya usanifu wa mradi mpya utakaotumia Ziwa Victoria kama chanzo cha maji cha uhakika. Vijiji vitakavyoingizwa katika mpango huo ni Kabulabula, Bugoji na Saragana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sokombi swalii la nyongeza kama unalo.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwoneyekiti, ahsante. Nasikitika sana kwa majibu ya Waziri ambayo yamekuwa ni hayo hayo yakijirudia. Tumeona wenzetu wa Kahama na Shinyanga wananaufaika kwa kiasi kikubwa sana na mradi huu wa maji kutoka Ziwa Victoria. Ni kwa nini Serikali imeviacha vijiji hivi ambavyo viko karibu kabisa na Ziwa Victoria kuvipatia maji muda mrefu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, zoezi la usanifu limekuwa likichukua muda mrefu sana kabla miradi kuanza kutekelezwa. Je, ni lini usanifu wa mradi huu utakamilika? Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, nafahamu *concern* ya Mheshimiwa Mbunge kwa changamoto hii ya maji na ame-*compare* na mradi wa maji unaokuja Kahama sasa hivi unakwenda Tabora mpaka Sikonge. Ni kweli, katika nchi yetu na maeneo mbalimbali kuna changamoto ya maji lakini siyo kwamba watu wa vijiji vile wamesahaulika ndiyo maana katika jibu langu nilizungumzia mpango wa maji katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, nilipofika Musoma jambo ambalo tulielekezana na wataalam ni kwamba siyo vyema watu wa mji kwa mfano ukianzia hapa Bunda mpaka unafika kule Musoma ambako ukiangalia wana utajiri mkubwa wa Ziwa Victoria halafu wakaendelea kupata shida ya maji. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Maji Awamu ya Pili ni *commitment* ya Serikali katika kipindi hiki cha miaka hii, tutahakikisha usanifu unakamilika lakini siyo usanifu peke yake bali mradi mkubwa huu wa maji lengo ni kuwasaidia wananchi wa

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

eneo lile kwa sababu wakikosa maji hata huduma za uchumi zinakwama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Tatizo la maji salama na maji safi katika nchi hii ni kubwa sana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI na Naibu Waziri wa Maji hivi majuzi walikuwa kwenye semina maalum ya programu ya maji inayoitwa "Uko Tayari?" Takwimu zinaonyesha kwamba zaidi ya asilimia 70 ya wagonjwa katika hospitali wanaugua magonjwa yanayotokana na maji machafu. Je, Serikali kupitia Wizara zote (TAMISEMI na Maji) zina mkakati gani kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji safi na salama hasa katika Awamu hii ya Tano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake amedai kwamba kuna magonjwa mengi mahospitalini ambayo yanatokana na kutokuwepo kwa maji safi na salama. Kuanzia bajeti ya mwaka 2006/2007 tulianzisha Programu ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji ambayo ilikwenda kwa muda wa miaka mitano, imekwisha Juni, 2016 sasa hivi tumeingia programu ya pili. Malengo yetu ni kuhakikisha kwamba tunaweka fedha ya kutosha na miradi mingi sasa inatekelezwa kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji safi na salama na kwa karibu zaidi.

Kwa hiyo, tumeshaanzisha na tumelenga kwamba itakapofika mwaka 2020 vijijini tuwe tumeshakwenda zaidi ya asilimia 85 na mijini twende asilimia 95. Kwa hiyo, tupo na tumeshaanza siyo kwamba tumekaa, tunaendelea na tutahakikisha kwamba wananchi hawapati shida ya magonjwa yanayotokana na maji. (*Makofi*)

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ya hapo, sasa hivi tume-*centralize* kuhusiana na ununuzi wa dawa za kutibu maji. Utaratibu uliokuwepo ni kila Mamlaka inanunua dawa hizo kivyake sasa tutanunua kutoka *center* moja kwamba Serikali sasa itakuwa inafanya *bulk purchase* ya dawa za kutibu maji ili tuhakikishe kwamba maeneo yote tunakuwa na maji safi na salama. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba niilize Serikali, katika Wilaya ya Kwimba visima 188 vimeharibika, havifanyi kazi kutokana na kuzeeka lakini vingine vimechakaa na vimekauka.

Sasa naomba kuuliza, kwa sababu wananchi wa Kata za Mwabomba na hasa Nkalalo pale *center* wanashida kubwa sana ya maji kutokana na visima hivi kuharibika, je, Serikali sasa ina mpango gani wa kusaidia ili visima hivyo viweze kufanya kazi wakati tunasubiri mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hoja ya Mheshimiwa Ndassa inakwenda katika maeneo mbalimbali na tumekuwa na changamoto kubwa sana katika visima vya maji na ndiyo maana tumekuwa tukitoa maelekezo maeneo mbalimbali kwamba hivi visima vya maji *recharging capacity* wakati mwagine inashuka kutokana na uharibifu wa mazingira. Hata hivyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ndassa kwamba katika mpango wa Serikali wa sasa hivi kuna mashindano maalum tumeyatoa kwa kila Halmashauri ya jinsi gani mipango yao mikakati watakavyozindua kuhakikisha miradi ambayo mwanzo ilikuwa haifanyi vizuri wanafanya ukarabati wa visima hivyo na kuweza kuvisimamia. Kuna mpango maalum ambao tumepeata fedha kutoka *World Bank* ambapo zinasaidia sana

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

katika suala zima la kuongeza nguvu za Halmashauri. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba kuitia Halmashauri zetu, ni mpango siyo wa Halmashauri ya Kwimba peke yake isipokuwa ni katika Halmashauri mbalimbali tumewaelekeza wataalam wetu wahakikishe sasa wanavikarabati visima mbalimbali viweze kutoa maji, lakini hata hivyo kuweza kusimamia vizuri kwa sababu baada ya kufanya hivyo watapata fedha nyininge zaidi kwa ajili ya kuhakikisha wanakarabati vituo vyao vya maji. Kwa hiyo, naamini Wilaya ya Kwimba itafanya hili ili wananchi wa maeneo yale waweweze kuondokana na shida ya maji katika maeneo yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa sasa aulize swali lake.

Na. 279

### **Mradi wa Kuchimba Mabwawa Katika Vijiji vya Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Serikali ilikuwa na mpango wa kuchimba mabwawa katika vijiji vya Msagali, Bumila, Makutupa, Lupeta, Inzomvu, Vibelewele, Kimagai, Chunyu na Ng'ambi ambayo yatahudumia wananchi pamoja na mifugo na kilimo cha umwagiliaji.

Je, Serikali imefikia hatua gani ya utekelezaji wa mpango huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

### **NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuitia *TASAF III* imekamilisha uchimbaji wa malambo sita katika vijiji vya Bumila, Msagali, Lupeta, Chunyu, Kazania na Nzogole kwa gharama ya shilingi 83,194,200. Wananchi 19,304 watapata huduma ya maji kuitia vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu umefanyika katika kijiji cha Chunyu kwa ajili ya kujenga bwawa kubwa ambalo litahudumia vijiji vya Msagali, Berege, Kisokwe, Chunyu na Ng'ambi. Jumla ya shilingi bilioni 17 zitahitajika kukamilisha kazi hii. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuanza ujenzi wa bwawa hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lubeleje, swali la nyongeza kama unalo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri, niipongeze sana *TASAF* kwa kazi nzuri, sasa nina maswali mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ni kwamba kazi hii kweli imeanza Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado hajakamilika katika vijiji ulivyotaja. Ni lini kazi hii itakamilika ili maeneo haya yaweze kupata huduma ya maji kwa sababu kuna shida kubwa sana ya maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vijiji katika mpango wa kuchimbiwa mabwawa, katika vijiji vya Kisisi, Ngalamilo, Iwondo pamoja na Nana kwa sababu hawa nao wana matatizo makubwa sana ya maji. Ni lini wataanza shughuli hizi? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lubeleje, *Senior MP* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lini miradi hii itakamilika na kuweza kutoa huduma ya maji, kwanza naomba nimuahidi katika Bunge hili la bajeti linaloendelea nitaomba mimi na Mheshimiwa Lubeleje twende katika miradi hii tukaiangalie kwanza halafu tushauriane vizuri tukiwa *site* kwa sababu najua Wilaya ya Mpwapwa ina tatizo kubwa sana la maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile viji vingine ambavyo ameviorodhesha ni kweli, nafahamu maeneo kwa mfano hata kule Tambi hali ya maji ni mbaya mpaka wanakuja huku Chamkoroma kutafuta maji. Kwa hiyo, tuna kila sababu kuhakikisha kwamba Wilaya ya Mpwapwa tunaipa kipaumbele. Pia katika ziara yangu hii nikiwa na Mheshimiwa Mbunge tutaambatana na watalam kutoka kwenye Halmashauri tuweze kufika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Makutupa ambako Mheshimiwa alikuwa anapigia kelele sana muda mrefujinsi gani tutafanya kuweka mipango sahihi kusaidia shida ya maji katika Wilaya yetu ya Mpwapwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

Na. 280

### **Kuunganisha Miundombinu ya Barabara Wilaya ya Itilima**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI (K.n.y. MHE. NJALU D. SILANGA)** aliuliza:-

Wilaya ya Itilima ni mpya na ina eneo kubwa linalovutia kwa ajili ya makazi na shughuli za kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha miundombinu ya barabara ya Migato, Nkuyu, Longalombogo, Laini, Bulombeshi na Bumera ili kuvutia watu kufanya biashara za mazao katika maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Jimbo la Itilima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuunganisha maeneo ya Migato, Nkuyu, Longolombogo, Laini na Bulombeshi kwa uboreshaji wa mtandao wa barabara kama ifuatavyo:-

(i) Barabara ya Bumera - Bulombeshi na Bumera - Gaswa - Sagata - Laini ya kilometra 20, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 imefanyiwa matengenezo ya sehemu korofi kwa kunyanya tuta na kuweka changarawe kilometra 3 na kujenga Kalavati 9 katika barabara ya Bulombeshi - Bumera - Gaswa. Katika bajeti ya mwaka 2017/2018 zimetengwa shilingi milioni 99.6 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum urefu wa kilometra sita na matengenezo ya kawaida urefu wa kilometra nane katika barabara ya Bumera - Gaswa - Laini.

(ii) Barabara ya Migato - Ndoleleji - Nkuyu yenye kilometra 22.9, mwaka wa fedha 2016/2017 imefanyiwa matengenezo katika maeneo korofi kwa kiwango cha changarawe na kujenga makalvati matatu katika barabara ya Migato - Ndoleleji yenye urefu wa kilometra 6.5.

(iii) Lagangabilili - Muhuze - Migato mpaka unapofika Longolombogo yenye kilometra 40, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 barabara hiyo imefanyiwa matengenezo katika kipande cha Lagangabilili - Muhuze - Migato kilometra 11 na kujenga makalvati kumi. Katika bajeti ya 2016/2017 yamejengwa makalvati sita na kuwekwa changarawe baadhi ya maeneo korofi yenye urefu wa kilometra 15. Aidha, katika bajeti ya 2017/2018, jumla ya shilingi milioni 49.18

zimetengwa kwa ajili ya kufanya matengenezo mbalimbali katika barabara hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaki swal la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Serikali kuhusiana na barabara hizi, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swal la kwanza, kuna madaraja makubwa matatu kwenye barabara hizi ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amezitaja na Halmashauri ya Wilaya ya Itilima imekuwa ikileta bajeti yake ili iweze kuyajenga madaraja haya matatu lakini TAMISEMI wanapunguza bajeti hiyo kiasi kwamba Halmashauri imeshindwa kujenga haya madaraja matatu. Je, Serikali inasema nini juu ya madaraja haya kwa sababu yasipojengwa ni kikwazo kikubwa kwa usafiri kwa wananchi wa Wilaya ya Itilima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swal la pili, kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga daraja la Mwabasabi, ni ya mwaka juzi. Serikali inasema nini juu ya ujenzi wa daraja hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wakati mwingine bajeti zinakuja lakini kutokana na ukomo wa bajeti mapendekezo mengine ya Halmashauri yanakuwa yamekwama. Katika mchakato wa bajeti ya mwaka huu tulivyokuwa tukipitisha hapa, tuliona ni jinsi gani Ofisi ya Rais, TAMISEMI itahakikisha inaangalia vipaumbele katika maeneo korofi hasa kuondoa vikwazo na ndiyo maana tumepitisha bajeti ya shilingi bilioni 247.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi kuangalia katika mpango wetu wa kuondoa vikwazo maeneo mbalimbali pale ambapo kuna vikwazo vyataga msingi

katika ujenzi wa madaraja tutatoa kipaumbele. Naomba niwasih i wataalam wetu kule *site* waanze kufanya *designing* na *needs assessment* katika maeneo mbalimbali ili kuonyesha ni gharama kiasi gani zinahitajika katika ujenzi wa madaraja haya ambayo yatahusika. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba kama Serikali tunalichukua hili lakini katika mpango wetu wa kuondoa vikwazo tutatoa kipaumbele katika maeneo haya. Lakini suala la ahadi ya Mheshimiwa Rais, naomba niwahakikishie lengo kubwa la Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha kwamba ahadi hizi zote zinatekelezeka. Naomba nimhakikishie kwamba katika kipindi hiki cha utekelezaji wa llani 2015 - 2020 daraja hili ni mionganoni mwa maeneo ambayo tunaenda kuyajenga, lengo kubwa ni ili ahadi ya Mheshimiwa Rais iweze kutekeleza katika maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafo. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, sasa Mheshimiwa Jamal Kasim Ali, Mbunge wa Magomeni aulize swali lake.

Na. 281

### **Kuwasaidia Wazawa kwenye Viwanda**

**MHE. JAMAL KASSIM ALI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani katika kuwasaidia wafanyabiashara wa Kitanzania kuwekeza kwenye viwanda nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**  
aliibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jamal Kassim Ali, Mbunge wa Magomeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa viwanda nchini unategemea zaidi mazingira ya uwekezaji yaliyopo ikiwa ni pamoa na upatikanaji wa ardhi yenyé miundombinu wezeshi, sera mbalimbali, mifumo ya kodi na mifumo ya upatikanaji wa vibali vinavyotakiwa kisheria ambayo ni majukumu ya Serikali. Baada ya kuwepo mazingira wezeshi, Serikali inabaki na majukumu ya kuhamasisha wawekezaji wakiwemo wa Kitanzania kuweza kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara wa Kitanzania ili kuwekeza kwenye viwanda hapa nchini. Miongoni mwa mikakati hiyo ni mafunzo yanayotolewa kwa Watanzania wenye nia ya kuwekeza katika viwanda juu ya kuibua mawazo ya kibiashara, kuanzisha, kuendesha na kusimamia biashara kupitia *SIDO*, kutoa ushauri wa kitaalamu wa jinsi ya kuchagua teknolojia sahihi inayoendana na wazo la ujenzi wa kiwanda alilonalo Mtanzania kupitia *TIRDO*, *TEMDO* na *CAMARTEC* na namna ya kupata ama kukuza mtaji wa ujenzi wa viwanda kupitia *NEDF*, *SIDO* na *TIB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha utendaji, Wizara imeanzisha Dawati la Wepesi wa Kufanya Biashara (*Easy of Doing Business*) ambalo lina jukumu la kuondoa ugumu wa kuanzisha na kuendesha biashara hapa nchini. Vilevile, imeandaa mwongozo kwa Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji kutenga maeneo, kusimamia sheria, kanuni, taratibu na kutoa maelekezo kwa wawekezaji. Aidha, Watanzania wanaotaka ama walio na mitaji mikubwa wanaweza kuwekeza kupitia maeneo ya *EPZA* ambayo yametengwa mahsus kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi. Vilevile, wanaweza kuwasiliana na *TIC* kupata vivutio mbalimbali vilivyowekwa na Serikali kwa ajili ya uwekezaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jamal, swali la nyongeza kama unalo.

**MHE. JAMAL KASSIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la msingi amekiri kwamba moja ya mambo muhimu kabisa ya Watanzania hawa kwenda kuwekeza kwenye viwanda ni pamoja na kuwa na mitaji. Watanzania hawa wamefanya biashara kubwa sana na Serikali na wana madeni makubwa ambayo wanaidai Serikali.

Je, Serikali haioni ipo haja sasa madeni haya ambayo wamekuwa wakidaiwa kwa muda mrefu kuyalipa kwa haraka ili Watanzania hawa nao sasa wapate fursa ya kwenda kushiriki katika uchumi wa viwanda ambao Mheshimiwa Waziri ameeleza? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kuja na sera maalum ambayo itatoa *special incentive package* kwa wawekezaji wazawa Watanzania ili nao waweze kushiriki kikamilifu katika uchumi wa viwanda kutokana na kuwa nyuma kiteknolojia, kifedha na mambo mengine ambayo ukiwaweka na wenzetu wa mataifa mengine Watanzania hawa hawawezi ku-*compete?* Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

### **WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio wapo wafanyabiashara, wakandarasi ambao wamefanya kazi na Serikali na wanadai stahiki yao, Serikali itawalipa. Utaratibu wa Serikali unapitiwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekuwa akilisema mara kwa mara kwamba jambo kubwa ni kufanya uhakiki na kadri uhakiki unapofanyika hao watu wanalipwa na niwahakikishie kwamba Serikali itawalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na vivutio, sasa hivi kuna vivutio, suala la muhimu kwa wafanyabiashara wa Tanzania au kwa Watanzania ambao wangependa kupewa vivutio maalum waone hivi vivutio vilivyopo watuambie ni wapi sio vizuri. Hatuwezi kubadilisha vivutio, kwanza anza utuambie hiki siyo kizuri hiki ndiyo kizuri ndiyo tutabadiilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyongo na jirani yake Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona, naomba niulize swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna mfuko wa *NEDF* ambao Mheshimiwa Waziri ameutaja yaani *National Entrepreneur Development Fund*, kwa mwaka huu pesa hizo hazijatoka. Napenda kupata kauli ya Serikali, je, ni lini hizo shilingi bilioni 2.5 zitatolewa ili ziweze kuwawezesha Watanzania wanaotaka kufungua biashara ndogondogo au kufungua viwanda vidogo vidogo waweze kuwezeshwa na kufanya hivyo? Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa *NEDF* kama mlivyoona taarifa ambayo imekuja pekee ni mfuko ambao unawachangamsha wawekezaji ukitoa mikopo mbalimbali. Katika mwaka wa fedha tunaomaliza tulitengewa shilingi bilioni 2.4, pesa hizo hazijatoka, lakini mwaka huu haujaisha. Nina imani hizo pesa zitakuja katika mwaka huu wa fedha na nimemkumbusha Waziri wa Fedha kwamba fedha hizo Wabunge wanazihitaji haraka wazipeleke Majimbo. Nina imani kabla juu halijazama pesa hizo zitapatikana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa jirani yake Mheshimiwa Saumu.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa sababu tunataka tuingie kwenye Tanzania ya viwanda na Tanzania ya viwanda ni lazima iende sambamba na uwekezaji kwenye ardhi lakini uwekezaji kwenye ardhi unakumbwa na matatizo makubwa. Tatizo la kwanza vijiji vyetu vingi havijaingia kwenye matumizi bora ya ardhi,

matokeo yake mwekezaji anakosa nafasi na hata pale ambapo vijiji vimeshaingia kwenye matumizi bora ya ardhi kuna tatizo kwenye Makamishna wa Kanda katika upatikanaji wa ardhi lakini sio hivyo tu, hata kwenye Ofisi ya Rais ambapo nako kuna matatizo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba ufupishe swali tafadhali.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Je, nini kauli ya Serikali kwa wawekezaji wanaohangaika kutafuta ardhi ya kufanya uwekezaji katika kilimo? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa rafiki yangu Alhaj ametaka kujua kauli ya Serikali. Tunalitambua tatizo la upatikanaji wa ardhi, ndio maana si mara moja Mheshimiwa Waziri Mkuu na Ofisi ya TAMISEMI wametoa maelekezo kwa mamlaka za Mikoa na Wilaya, watenge maeneo kwa wale walio tayari waweze kuwekeza mara moja. Nirudie, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, tengeni maeneo yule anayetaka kuwekeza msimsbirishe.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua sasa aulize swali lake.

Na. 282

**Ajali za Pikipiki**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa lengo la Serikali kuruhusu vyombo vyombo usafiri wa pikipiki kubeba abiria na mizigo ni kusaidia kurahisisha usafiri na pia kutoa ajira kwa vijana hapa nchini lakini ajali zinazotokana na vyombo hivi kwa sasa ni nyingi kuliko vyombo vingine.

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni ajali ngapi za bodaboda zimetokea kwa miaka mitatu toka mwaka 2015 - 2017 na ni watu wangapi wamepoteza maisha kwenye ajali hizo na walemavu ni wangapi?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya uhakika ya kuokoa maisha na nguvukazi ya Taifa inayopotea kwa usafiri huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Kaliua, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitatu toka Januari, 2015 hadi Februari, 2017 jumla ya ajali 5,418 za bodaboda zilitokea na kusababisha vifo vya watu 1,945 na majeruhi 4,696.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inayo mikakati ya kukokoa maisha na nguvu kazi ya Taifa inayopotea kutohana na ajali za bodaboda. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kupitishwa kwa Kanuni ya Leseni za Pikipiki na Bajaji iliyopita mwaka 2009;

(ii) kutoa elimu ya Usalama Barabarani mashulenii na kupitia vipindi vya redio, televisheni pamoja na vipeperushi;

(iii) Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa waendesha bodaboda;

(iv) Kuimarisha usimamizi wa Sheria za Barabarani;

(v) Kusisitiza madereva wa bodaboda kuepuka kuendesha kwa mwendo kasi;

(vi) Kuchukua hatua kwa vitendo vyote vya ulevi na kuweka viakisi mwanga (*reflectors*) ili kuonekana kwa urahisi; na

(vii) Kusisitiza matumizi ya kofia ngumu ili kupunguza madhara punde ajali zinapojitokeza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Magdalena Sakaya, swali la nyongeza.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, suala la ajali hizi kutokana na jibu la msingi imekuwa ni hatari kubwa na ukiangalia idadi ya watu waliopoteza maisha, waliopata ulemavu na majeruhi ni wengi. Vilevile ajali hizi zinasababisha kuwepo kwa walemauvu, wategemezi, wajane na wagane wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua ambazo zinachukuliwa na Wizara na Serikali kuona kwamba ajali zinapungua lakini bado ajali zinaongezeka.

Je, Serikali haioni sababu kubwa ya ajali hizi ni kwamba madereva wa bodaboda hawafuati sheria za barabarani ikiwepo *ku-overtake* kushoto badala ya kulia? Serikali haioni sababu ya kuendesha masomo au mafunzo maalum kila Wilaya kwa bodaboda wote waweze kuelewa kanuni na sheria za barabarani na hivyo kuweza kupunguza ajali za barabarani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, baadhi ya maaskari barabarani badala ya kuwa elimisha bodaboda wamefanya bodaboda ni vyanzo vya mapato, kila wakiwaona wanakimbizana nao barabarani matokeo yake wao wanakuwa ni kisababishi cha ajali badala ya kupunguza ajali. Serikali inafanya nini na inachukua hatua gani kwa wale maaskari wote ambao wanakimbizana na bodaboda barabarani hajali amebeba abiria au hajabeba abiria ili kupunguza ajali hizi na kuokoa maisha ya Watanzania wanaopoteza maisha? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mbunge kwamba jambo hili linamgusa na ameongea kwa hisia kama mama na kama mwakilishi wa vijana wetu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu Serikali imefanya jithada kubwa kama ambavyo nimeelezea, jambo ambalo limesalia ni familia zetu kuanzia ngazi za familia na ngazi za vijiwe, kuliongea jambo hili kama moja ya jambo linalomaliza maisha ya vijana wetu. Kila tunapokaa tuambizane kwamba ukienda mwendo kasi, usipofuata taratibu za uendeshaji wa vifaa hivi nya moto, madhara yake ni kupoteza maisha ya mwendeshaji mwenyewe ama yule aliyebebwa. Kwa hiyo, hili jambo likienea elimu yake itakuwa kubwa kuliko hii tu ambayo mpaka sasa tunaendelea kuifanya ya kutoa semina Wilaya kwa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu vijana hawa kukimbizwa na askari, niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge ukichukulia kwenye sura moja unaweza ukaona kama vijana wanaonewa sana lakini niseme kuna utaratibu ambao unakuwa unakosewa. Moja, vijana wanakuwa wameshapewa leseni lakini inatokea wanapokuwa kule vijiweni wanakabidhiana bodaboda hizi kwa mtu ambaye hana leseni, mtu ambaye hana mafunzo yaani amejaribisha tu akaona pikipiki inatembea naye anabeba abiria, hili ni kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimewaelekeza viongozi wa vijiwe vile nya bodaboda kwamba na wenyewe watimize majukumu ya kiuongozi kwamba akitokea mwenzao aliyekosea na wenyewe wawe tayari kumwambia unatakiwa uripoti kistaarabu polisi ili uweze kumaliza jambo lako la kisheria. Kama hawatafanya hivyo, polisi itakuwa haina njia nyingine zaidi ya kumtafuta kwa nguvu na kuweza kumkimbiza popote pale ambapo yupo aweze kufikishwa katika mkono wa sheria.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tunawapenda sana vijana wetu lakini mapenzi yetu kwa vijana wetu ni kuhakkisha tunaokoa maisha yao. Kwa hiyo, huruma tunayoweza kufanya ni kuhakkisha tunadhibiti jambo hili na hamna njia mbadala zaidi ya kuweza kuhakkisha tunachukua hatua za kisheria kwa yule ambaye anaonekana anakiuka sheria. Kwa wale ambao kwenye vijiwe vyao watatimiza maelekezo haya, tumeelekeza askari wasikimbizane nao bali wamalize kistaarabu mambo ambayo yanahu. Sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma atafuatiwa na Mheshimiwa Waitara.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, napenda niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mashaka, matatizo, huzuni na gharama kubwa za matibabu zinaendelea kuwakabili vijana wetu hawa kutokana na hizi ajali za bodaboda. Je, ni lini Serikali itaongeza usimamizi na udhibiti wa kuhakkisha kwamba *helmet* na *reflector* zinavaliwa na vilevile kudhibiti upakianaji wa kimishikaki ambao unasababisha watu wengi zaidi kuumia kwa wakati mmoja? Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu maelekezo tulishatoa na tunachukua hatua kwa maswali yote mawili aliyoauliza. Moja likiwepo hili la kuva kofia ngumu, tumeweka hiyo ni sheria na tumeenda mbali zaidi tunataka si tu mwendesha bodaboda tunataka hata abiria naye atimize wajibu huo wa kuva kofia ngumu. Pamoja na hilo, hili lingine la ubebaji wa mishikaki kama alivyoita, abiria zaidi ya moja na lenyewe tumeelekeza popote pale yanapotokea lichukuliwe kuwa ni kosa.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo kwamba jambo hili ni vema likaongelewa kwa ngazi ya kijamii na familia kwamba tuendelee kuwaelekeza vijana wetu. Mara nyingi vijana wetu wakielekezwa kwa mkono wa Serikali wanaona kama wanaonewa lakini wakielekezwa kuanzia ngazi ya familia, tunapokaa tuwaambie vijana wetu tunawapenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe niliwahi kuwapa vijana bodaboda kule Jimboni, niliwahi kuwapa wadogo zangu, watoto wa dada zangu lakini jambo la kwanza nililowaambia, niliwaambia nawapa chombo hiki cha moto lakini chombo hiki kinauwa. Wakiambiwa mkono ambaao usio wa kisheria ambaao ni wa kifamilia linawaka zaidi kutambua kwamba ukikosea masharti ya uendeshaji ukaenda kasi, ukakosea sheria za uendeshaji barabarani, gharama yake ni kupoteza maisha ya mwendeshaji mwenyewe na abiria aliyebebwa kutoka kwenye hicho chombo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Jimbo la Ukonga lina kata 13 na kata zote zina bodaboda karibu vijiwe zaidi ya kumi kila kata moja. Ukonga tumechangishana fedha tukajenga Kituo cha Polisi kule Chanika na kingine kinataka kujengwa pale Kata ya Kivule, lakini kwa hali ilivyo sasa, wananchi wa Ukonga na hasa bodaboda nikiwaambia wachangie fedha hawatachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza usiku wa kuamkia leo, wanakuja askari zaidi ya 20 wana bodaboda, walikuwa wanakuja na gari wanaificha, halafu wanapiga watu mpaka na marungu, *wana-search* kwenye *wallet*, kwenye pochi kila mahali wanaomba fedha. Sasa wanaenda wanakusanya bodaboda zile wanaomba shilingi 10,000 kwa lazima, kama huna zinapakiwa kwenye gari zinapelekwa *central*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natakiwa nijue, ili kuleta mahusiano mazuri kati ya vijana wa bodaboda na polisi, Waziri anatoa kauli gani kuhusiana na jambo hili? Hata haya mambo ya mauaji kama watu wana uhasama hawatoi taarifa. Wanawakimbia kwa sababu ukikamatwa na polisi wala hakuulizi leseni, wala hakuelekezi, kama huna pesa unatembea. Naomba Waziri atoe kauli hapa kusaidia vijana wa bodaboda Mkoa wa Dar es Salaam na hasa Jimbo la Ukonga. Ahsante Mwenyekiti.

**MWENYEKETI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba maelekezo ya Wizara tulyotoa ni kwamba kuwa na bodaboda sio kosa na tumeelekeza watu wanaofanya makosa ndiyo wakamatwe. Kuwa tu na bodaboda haitoshi kuwa kosa kwa sababu hilo ni jambo ambalo lipo kisheria. Kwa maana hiyo nimepokea tu hiyo ya nyongeza aliyoisema ambayo yenye we imekaa kituhuma zaidi nitalifanya kazi, kama kweli lipo tutachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maelekezo yetu tumesema kama vijana wamekosea wafkishwe kwenye mkono wa sheria lakini kama hawajakosea waachwe wafanye kazi zao za kujitafutia maisha kwa uhuru na usalama na wala wasikimbia. Nilielekeza nikasema kuna wakati mwingine hata wanaweza wakawamata kwa bahati mbaya na ikafika mpaka vituoni, niliwaambia wasione aibu kumuachia yule ambaye walimkamata kimakosa ambaye alikuwa hausiki.

Nilisema hata wamuombe radhi kwamba wewe si tuliyekuwa tunakutafuta nenda kaendelee na shughuli lakini isiwe kosa kwamba yejote ambaye ameshakamatwa akifika kituoni basi inakuwa kazi kutoka, tuwatendee haki kufuatana na kosa kama amefanya ama hajafanya.

**MWENYEKITU:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tunaendelea na Wizara ya Maliasili

na Utalii na swalii la Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mbunge wa Ulanga litaulizwa na Mheshimiwa Sadiq Murad kwa niaba.

Na. 283

### **Wanyama Waharibifu wa Mazao**

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ (K.n.y. MHE. GOODLUCK A. MLINGA)** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la wanyama waharibifu kama vile viboko na tembo kwenye maeneo ya mashamba katika Kata za Ruaha, Chilombola, Ilonga, Ketaketa, Mbuga ya Lukande na Lupilo.

Je, Serikali ina mpango gani kuzuia uharibifu huo wa mazao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mbunge wa Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwepo na ongezeko la wanyama wakali na waharibifu katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo Kata ya Ruaha, Chilombola, Ilonga, Ketaketa, Mbuga ya Lukunde pamoja na Lupilo. Kutokana na madhara yanayosababishwa na wanyama waharibifu hususan tembo na viboko, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kunusuru maisha na mali za wananchi. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kufanya doria za wanyamapori wakali na waharibifu ili kudhibiti madhara ya wanyamapori hao kwa kutumia Askari Wanyamapori waliopo katika Pori la Akiba Selous eneo la Ilonga, Kikosi Dhidi ya Ujangili pamoja na Askari Wanyamapori katika Halmashauri ya Wilaya Mahenge;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(ii) Kutoa elimu ya uhifadhi kwa jamii kuhusu kuijukinga na wanyamapori wakali na waharibu wakiwemo tembo na viboko;

(iii) Kuendelea na mbinu mbalimbali za kupunguza madhara yatokanayo na uvamizi wa tembo na kukuza kipato kwa mfano matumizi ya mizinga wa nyuki, oil chafu na kilimo cha pilipili kuzunguka mashamba na kadhalika; na

(iv) Aidha, Wizara imekuwa inafanya majararibio ya kutumia ndege zisizokuwa na rubani yaani *drones* kwa ajili ya kufukuza tembo pindi wanapovamia makazi na mashamba ya wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saddiq Murad, swali la nyongeza.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa *Mikumi National Park* imepakana na Wilaya ya Mvomero na kata za Doma, Msongozi, Melela, Malaka pamoja na Mangaye; kwa kuwa wanyama waharibifu wanaingia sana katika mashamba ya wakulima na wanaharibu sana mazao ya mahindi, mpunga, nyanya na kadhalika na kwa kuwa tembo wengi sana wameshafanya uharibifu mkubwa, je, Serikali sasa iko tayari kuongeza Askari wa Wanyamapori katika maeneo hayo angalau kila kata kuwe na askari mmoja ili kuondoa tatizo ambalo wananchi wanakabiliana nalo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Wilaya ya Mvomero ina upungufu mkubwa wa vitendea kazi, je, Serikali iko tayari sasa kuisaidia Wilaya ya Mvomero vitendea kazi pamoja na masuala mengine ya usafiri ili tuweze kukabiliana na hali hiyo? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wanyama wakali na waharibifu wameongezeka katika maeneo mbalimbali hapa nchi na katika eneo la Wilaya ya Mvomero wanyama hawa wameongezeka sana katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saddiq Murad Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pamoja na Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Wilaya tumetembelea hayo maeneo ambayo yamezidiwa sana na uvamizi wa wanyama wakali na waharibifu. Wizara itaongeza askari kusaidiana na wale walio katika Wilaya ya Mvomero ili kupambana na kadha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Wizara itashirikiana na Halmashauri ya Mvomero kwa kuipa vitendea kazi zaidi pamoja na kuwasaidia katika usafiri ili waweze kukabiliana na tatizo hili ambalo limeongezeka sana katika Wilaya hiyo. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbaraka Dau hhalafu atafuata Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Tatizo la viboko lilitopo katika Jimbo la Ulanga linafanana sana na tatizo la viboko lilitopo Kisiwani Mafia. Wananchi wa kata za Ndagoni, Baleni na Kirongwe wameharibiwa mazao yao na ng'ombe wao wameuwawa na viboko waharibifu. Kutohana na ongezeko kubwa sana la viboko hawa na Kisiwa cha Mafia ni eneo dogo, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kutoa ruhusa tuanze kuwavuna viboko hawa kwa sababu kule ni kitoweo pia? Ahsante. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpa pole sana Mheshimiwa Dau na wananchi wake wa Mafia kwa kadhia hii ambayo imewakumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ambayo tutachukua ni pamoja kutuma wataalamu waende wakafanye sensa ili tujue kwamba kuna viboko wangapi katika eneo hilo na tuweze kuangalia kama kuna uwezekano wa kuweza kuwavuna hao viboko ili kupunguza madhara yake kwa wananchi wa eneo la Mafia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la wanyama waharibifu ni kubwa sana katika Jimbo langu la Bunda Mjini na Jimbo la kaka yangu Boni. Sisi wananchi wa Mkoa wa Mara hatuhitaji kuomba chakula na mwaka jana Mheshimiwa Waziri wa Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Jenista alikuja akaliona tatizo hilo na Mheshimiwa Waziri mwenyewe anajua, tatizo la tembo kuharibu mazao ya wananchi, kuua wananchi pamoja na mali zao. Sasa nataka kujua, ni lini Serikali mtahakikisha mnakuwa na mkakati wa kudumu wa kumaliza tatizo hili katika vijiji vyote vinavyozunguka hifadhi? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika Mkoa wa Mara na hasa Wilaya za Bunda, Serengeti, Tarime na Wilaya za maeneo yale kuna kadhia kubwa sana ya wanyama waharibifu wanaotoka hasa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kuingia katika mashamba na wakati huu ambapo mavuno yanakaribia ndio kadhia hii inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za muda mfupi, mwaka tutachukua hatua ya kuongeza askari na magari ya *patrol* ili kuhakikisha kwamba kama mwaka jana tunawaokoa wananchi na tatizo hili.

Pili, tunazungumza na washirika wetu wa maendeleo kuona ni namna gani tunaweza kuweka fensi ya kilometra 140 ili kuangalia kwa majaribio kama itakuwa ni suluhisho la tatizo hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 284

### **Kero ya Kadi za Kulipia Hifadhi ya Ngorongoro**

**MHE. ESTER A. MAHAWE** aliuliza:-

Kadi za kulipia Ngorongoro zimekuwa kero kwa wageni na wahudumu kwani muda mwingi umekuwa ukipotea wakati kufanya malipo.

Je, ni lini Serikali itafanya marekebisho ili kuwe na mfumo wa kadi kama za *TANAPA*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

### **WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imebadilisha mfumo wa malipo na utoaji wa vibali vya kuingia katika Hifadhi ya Ngorongoro.

Mfumo huu mpya kabisa ujulikanao kama *Ngorongoro Safari Portal* ulianza kutumika tarehe 01 Februari, 2017 na umeonyesha ufanisi mkubwa ikiwa ni pamoja na kuondoa kabisa msongamano wa wageni katika malango ya kuingia kwenye hifadhi na kuongeza ufanisi katika makusanyo ya mapato.

### **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu mpya uko kwenye mtando wa *internet* na hivyo huwezesha wakala wa utalii kulipa na kupata vibali moja kwa moja kwa njia ya mtando bila kulazimika kufika katika ofisi, kwenda benki au malango ya kuingia katika Hifadhi za Ngorongoro.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mahawe, swalii la nyongeza.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri baada ya kero hiyo kurekebishiwa lakini bado *driver guides* wanapofika pale getini wanatakiwa kuandikisha majina ya wageni ambao wanawapeleka Ngorongoro ama Serengeti. Kwa hiyo, hilo nalo bado linaleta usumbufu mkubwa kwa sababu *counter* inayotumika katika uandikishwaji pamoja na ku-*submit* zile risiti ni moja. Je, Mamlaka haioni kwamba kuna ulazima sasa na umuhimu wa kuongeza madawati yale ya kutolea huduma hiyo ili kuokoa muda wa wageni unaopotea pale getini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kwa kuwa biashara yoyote inahitaji huduma bora kwa wateja yaani *customer care* na hili limeonekana likikosekana maeneo ya geti la Lodware na *Naabi Hill*. Je, Mamlaka haioni kwamba wafanyakazi wale wanahitaji kupatiwa *indoor training* ya mara kwa mara ili kuweza kufanya utalii wa ushindani na nchi jirani ambako *customer care* iko juu? Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru sana kwa maswali mazuri ambayo Mheshimiwa Mahawe ameyauliza. Maswali haya ni *relevance* kabisa kwa kazi ambayo tunaifanya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza suala la kuongeza madawati tumeliona na pale kwenye lango kuu kutoka Karatu unavyoingia Ngorongoro tumeongeza watendaji kazi kwa ajili ya kuwatambua watu ambao wanataka kuingia ndani ya hifadhi. Shughuli hii ni muhimu kwa sababu za

usalama, lakini pia kwa sababu ya kuweza kukagua mapato tuliyokusanya na watu ambao wameingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda nimueleze Mheshimiwa Mahawe kwenye swali lake la pili kwamba ni kweli wafanyakazi wanahitaji kupatiwa mafunzo ya mara kwa mara ili kuongeza ubora wao katika *customer care*, lakini pia katika kushirikisha na kutoa maelekezo kwa wageni. Kwa hiyo, shughuli hii tutaendelea kuifanya kila siku na tunategemea kwamba itaongeza ufanisi wa eneo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omary Badwel atafuatiwa na Mheshimiwa Gidarya.

**MHE. OMARY H. BADWEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa utozaji huu wa ushuru na kodi mbalimbali kutoka Wizara hii ya Maliasili na Utalii katika maeneo mbalimbali mahali pengine umekuwa ama haukufikiria vizuri au umekuwa kero. Kwa mfano katika mazao ya ubuyu na ukwaju, mazao ambayo yana bei ndogo sana kwa maana ya shilingi 100 kwa kilo na katika masoko ya Dar es Salaam na maeneo mengine ya miji yanauza kwa shilingi 200. Mazao haya yamekuwa yakivunwa ama na kina mama wenye kipato cha chini au vijana na watu wengine ambao wanapambana na umaskini.

Hata hivyo, Wizara hii kupitia Maliasili wanatoza shilingi 350 kwa kilo na imewafanya sasa wafanyabiashara hawa washindwe kabisa kufanya hii biashara kwa sababu bei yenye ni ndogo na sasa inafikia shilingi 500 baada ya ushuru huu.

Je, Mheshimiwa Waziri anafikiria nini juu ya kufuta ushuru huu ili kuwasaidia wale wafanyabiashara wadogo wadogo waweze kupambana na umaskini? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika tozo za mazao ya misitu na mazao katika sekta ya utalii zingine ni kero sana kwa wananchi. Moja ya tozo hizo ambazo ni kero kwa wananchi ni tozo ya matunda ya ubuyu na matunda mengine ya misituni ambayo wananchi wanakusanya na kupeleka kuuza. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tozo hizi ambazo ni kero zitafutwa pamoja na hii ya kutoza kodi ya ubuyu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gidarya.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa pia na kero katika sekta ya uwindaji katika utoaji leseni hasa kwa wazawa. Soko hili limemilikiwa zaidi kwa wageni kuliko wazawa. Kwa mfano, leseni ya uwindaji kwa mwaka unalipa dola 600 na tena unalipa dola 200.

Je, Wizara haioni umuhimu wa kuwapa wazawa zaidi ili pia waweze kulinda hifadhi zetu? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka uliopita wa uwindaji unaoishia mwezi Juni, 2017 vitalu vilivyokuwa vimetolewa asilimia 85 walipewa wazawa na ni vitalu asilimia 15 tu ambavyo walipewa wageni. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba utoaji wa vitalu unawapendelea wageni.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini sasa aulize swali lake.

## **Ujenzi wa Barabara ya Nyololo- Igowole - Mtwango**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara ya kilometra 40 ya kutoka Nyololo - Igowole - Mtwango kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Nyololo-Igowole hadi Mtwango au hadi Kibao yenye urefu wa kilometra 40.4 ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*). Maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami yanaendelea ambapo upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii yamekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuifanya matengenezo ya aina mbalimbali barabara hii ili iweze kupitika katika majira yote ya mwaka wakati ikiendelea kutafuta fedha kwa ajilli ya ujenzi wa kiwango cha lami. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 450.077 na katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 160.511 kwa ajili ya kuifanya matengenezo ya aina mbalimbali barabara hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigola, swali la nyongeza.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini hii barabara ina miaka minne sasa tangu upembuzi yakinifu kukamilika. Naibu Waziri wa Ujenzi aliyejita aliwahi kuja kule akaongea na wananchi akasema kwamba ujenzi wa kiwango cha lami utaanza mara moja. Naibu Waziri naomba awaambie wananchi ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu upembuzi yakinifu ulishakamilika? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wananchi wa Kijiji cha Nyololo, Nziwi, Igowole, Mninga, Kibao, Lufuna na Mtwango waliwekewa alama ya 'X' kwenye nyumba zao na Serikali iliahidi kwamba alama ya 'X' ambayo ni ya kijani watapewa fidia. Wananchi wameshindwa kuendeleza nyumba za biashara kwa sababu zimebekewa alama ya 'X'. Ni lini Serikali italipa fidia wananchi wale ambao wanasubiria mpaka leo? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyo sema kwenye jibu la msingi barabara hii tutaanza kuijenga mara tutakapoanza kupata fedha. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Kigola kwamba Serikali itatumia kila aina ya nguvu zake kuhakikisha kwamba inapata fedha na kutekeleza ahadi au dhamira ambayo Naibu Waziri aliyejita allionyesha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kwamba ni kweli wote waliwekewa alama ya 'X' za kijani watalipwa fidia na zitalipwa tutakapoata hizi fedha za ujenzi. Ulipaji wa fidia unaenda sambasamba na ujenzi wa barabara husika. Kwa hiyo, fedha hizi tunazozitafuta tunazitafuta zote, za ujenzi na za kulipa fidia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devotha Minja na Mheshimiwa Martha Mlata.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. DEVOTH A M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara ya Kichangani - Tubuyu katika Manispaa ya Morogoro ambayo ina urefu wa kilometra nne imejengwa kwa kilometra moja kwa shilingi bilioni tatu yaani kilometra nne imejengwa kwa shilingi bilioni 12. Je, Serikali iko tayari kupeleka wataalam kwenda kubaini ubadhirifu wa ujenzi wa barabara hii ambayo imejengwa kwa Mfuko wa Benki ya Dunia? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata concern hii kutoka kwa Wabunge hasa wa Mkoa wa Morogoro na hasa barabara hizi zinazojengwa *under Strategic Cities Project* pamoja na barabara zingine ambazo zinajengwa katika Manispaa. Bahati nzuri kwa taarifa za Morogoro tunazifanya kazi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaenda kufanya *verification* kuangalia *value for money* katika eneo lile lakini zoezi hilo tutalifanya maeneo mbalimbali ikiwemo katika Mji wa Hai, Mkoa wa Kilimanjaro. Lengo letu ni kwamba thamani ya fedha ipatikane ili wananchi waweze kupata huduma inayolingana na thamani ya fedha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kilio chake kimesikika tutaenda kulifanya kazi eneo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Serikali itoe tamko hapa kuwaeleza wananchi wa Iliongelo, Mdida, Singa, Mtinko, Nkungi hadi Haydom kwa ahadi yao waliyoahidiwa na Rais wa Awamu ya Nne kwamba barabara ya lami itajengwa kutoka Singida kupita maeneo hayo hadi Haydom lakini sasa hivi hakuna kinachoendelea. Naomba Serikali iwaambie wananchi hao. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la nyongeza ya Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Singida na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa huo, kama ifuatavyo:- (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba juhudizake za kufuatilia ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami hatimaye zitazaa matunda kwa sababu ahadi ambayo ilitolewa na Rais wa Awamu ya Nne tunayo na nimhakikishie kwamba ahadi hiyo tutaitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda kutekeleza ahadi hizi awamu kwa awamu kama ambavyo nimekuwa nikimueleza yeye pamoja na Wabunge wenzake wanaofuatilia sana barabara hii, barabara hii inaunganisha Wabunge wengi sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda sasa aulize swalii lake.

**MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Busanda hasa kule Nyamalimbe ambako wamepatwa na maafa, kwa watu kufukiwa na vifusi kwenye mgodi wa Nyamalimbe pale Magenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa swalii langu namba 286 lipatiwe majibu. (*Makofi*)

### **Umememe wa REA Busanda**

**MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa umeme wa *REA* utaanza kutekelezwa katika Jimbo la Busanda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Lolesia Jeremia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijiji Awamu ya Tatu umeanza rasmi nchi nzima tangu mwezi Machi, 2017. Mradi huu unajumuisha vipengele-mradi vya *densification, grid extension* na *off-grid renewable*. Mradi huu unalenga kuongeza wigo wa usambazaji umeme katika vijiji vyote vilivybaki nchi nzima, vitongoji vyote, taasisi zote za umma na sehemu za pembezoni ikiwa ni pamoja na maeneo vya visiwa. Usambazaji wa umeme katika Jimbo la Busanda utafanyika kupitia vipengele-mradi vya *densification* na *grid extension* utakaokamilika mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme katika Jimbo la Busanda pamoja na Wilaya yote ya Geita itajumisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometra 184.7; ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometra 582 na ufungaji wa transfoma 109. Mradi huu utaunganisha wateja wa awali 8,834. Gharama za mradi huu ni shilingi bilioni 25.6. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bukwimba, swalii la nyongeza.

**MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimwia Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa kwa muda mrefu sana kuna baadhi ya sehemu kwa mfano ndani ya Jimbo la Busanda wana umeme, lakini katika Taasisi za Serikali na za Umma hazijaweza kufikiwa na umeme huo. Nikitoa mfano, Kituo cha Afya Bukoli, Kituo cha Afya Lwamgasa, Shule ya Sekondari ya Bukoli, Shule ya Sekondari Lwamgasa, Shule ya Sekondari Chigunga na kwenye Zahanati ya Chigunga umeme huu haujafika.

Je, Serikali inasemaje sasa kuhusu mpango wa kuhakikisha kwamba Taasisi zote za Umma pamoja na sehemu za kuabudia zinafikiwa na umeme wakati utekelezaji unapoendelea? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumeona katika vyombo vy ya habari katika mikoa mbalimbali umeme ukizinduliwa ili Awamu ya Tatu ya REA iweze kuanza kufanya kazi lakini katika Mkoa wa Geita sijaona jambo hili likifanyika. (*Makof*)

Je, ni lini sasa Serikali itazindua rasmi umeme wa *REA* Awamu ya Tatu katika Mkoa wa Geita ili wananchi waweza kuanza kuona utekelezaji wake? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kumpa pole sana Mheshimiwa Bukwimba kwa wananchi wake wanne walioangukiwa na kifusi kwenye machimbo ya kule Nyamalimbe, pole sana Mheshimiwa Bukwimba kwa niaba ya wananchi wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyouliza Mheshimiwa Bukwimba, nianze kwanza kumpongeza anavyouatilia maendeleo ya umeme kwa wananchi wa Jimbo la Busanda. Hata hivyo, mradi kabambe wa *REA* Awamu ya Tatu, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi unalenga kupeleka umeme katika vijiji vyote vilivyobaki lakini katika vitongoji vyote vilivyobaki na taasisi za umma. Nisisitize katika hili, Taasisi za Umma ninamaanisha vituo vya afya, shule, misikiti, masoko na kadhalika, haya yote yatafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Bukwimba, vijiji vyake vya Nyalyuyeya ambavyo vituo vya afya havina umeme sasa vitawekewa umeme. Kule Nyamalimbe vituo vya afya pamoja na shule vitawekewa umeme. Shule za Bukoli, shule za Kamena, Kaseme pamoja na vituo vya kwa Mheshimiwa Musukuma, kisiwa chake cha Izumachele tutaenda mpaka huko.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa wa Busanda kwamba vitongoji vyote ambavyo vina zahanati tutawekeza zahanati umeme pamoja na shule. Umeme mwingine mbadala, kwenye taasisi za umma tutawewekeza pia umeme wa *solar*. Hii ni kwa sababu ikitokea kuna hitilafu ya umeme basi umeme wa *solar* uweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı lake la pili, ni lini sasa tunazindua, nitumie nafasi hii kusema kwamba ni kweli tumezindua mikoa kumi tu nchi nzima, tunaendelea kuzindua mikoa yote 15 iliyobaki ya Tanzania Bara, mkoaa mmoja hadi mwingine na mahali pengine ikilazimika tutazindua kila wilaya ili wananchi waweze kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumueleza Mheshimiwa Lolesia Bukwimba kuanzia mwezi wa saba tutaanza uzinduzi, kwa hiyo, mwezi wa saba Mheshimiwa Bukwimba tufuatane ili tukazindue umeme wa *REA* Awamu ya Tatu katika Jimbo lako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Bulembo halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wilaya ya Kyerwa Mkoani Kagera kuna vijiji ambavyo vimewekwa katika mpango wa Rea Awamu wa Pili, vijiji kama Songambele, Kitwe, Mulongo lakini havikupatiwa umeme. Vijiji hivi hivi pia vimewekwa katika Mpango wa *REA* Awamu ya Tatu. Je, Serikali itahakikisha katika Mpango huu wa *REA* Awamu ya Tatu, vijiji hivi havitakosa umeme? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vya Kyerwa ambapo vimebakia 27 vitapelekewa umeme vijiji vyote na siyo tu vijiji ambavyo umetaja vya Mulongo pamoja na Songambele lakini viko vijiji na chuo vya ufundu pale Kyerwa na chenyewe tutakipelekewa umeme. Kwa hiyo vijiji vyote 27 vilivyobaki vitapelekewa umeme katika mradi wa *REA* Awamu ya Tatu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Natambua katika Mkao wa Mbeya tayari *REA* Awamu ya Tatu imeishazinduliwa, lakini kuna changamoto kubwa sana katika Wilaya ya Rungwe katika vijiji vya Lupoto, Katabe na Ibungu mpaka sasa hawajapata umeme na hatujajua ni lini watapata. Naomba majibu ya Serikali tuweze kujua ni lini Wilaya hizi zitapata umeme wa *REA*? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa Mheshimiwa Mbunge nakushukuru ulivyouliza, hapa tunapoongea katika kijiji cha Lugota wakandarasi wanaendelea na kazi, kwa hiyo wanaendelea kupata umeme, lakini vijiji vya jirani pia tutavitembelea ambavyo bado lakini vijiji vyote ulivyotaja kwenye eneo lako

vitapata umeme wa REA na umeanza mwezi wa tatu na kwako wewe utakamilika mwakani mwezi wa saba.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na swali la mwisho, Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, Mbunge wa Buyungu sasa aulize swali lake.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaauliza swali langu naomba nitoe pole kwa raia wa Burundi waliopigwa na wanajeshi wa Jeshi la Wananchi Tanzania katika Soko la Kabare, Kata ya Mwarama, Jimbo la Buyungu. Naomba sasa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Buyungu swali namba 287 lipate majibu.

Na. 287

### **Uwepo wa Madini katika Wilaya ya Kakonko**

**MHE. KASUKU S. BILAGO** aliuliza:-

Maeneo mengi ya Wilaya ya Kakonko yanaonyesha kuwepo kwa madini yenye thamani kama dhahabu na almasi.

(a) Je, kuna tafiti zozote zillizofanyika kuhusu upatikanaji wa madini Wilaya ya Kakonko?

(b) Kama zipo, je, ni madini gani yanapatikana na ni katika maeneo yapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, Mbunge wa Buyungu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia miaka ya 1970 Serikali kupitia Wakala wa Jilojia Tanzania (*GSt*) imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali za kubaini uwepo na upatikanaji wa madini katika Wilaya ya Kakonko. Baadhi ya tafiti zilizofanyika ni pamoja na upimaji na uchoraji wa ramani za kijolojia katika eneo la Kakonko. Maeneo mengine yaliyofanyiwa kazi hiyo ni Kalenge na sehemu ya Kibondo. Aidha, kati ya mwaka 1980 na 1985, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *UNDP* walifanya utafiti mwingine wa madini ya chokaa katika eneo la Bumuli Wilayani Kakonko.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti hizo zilibaini uwepo wa madini ya dhahabu katika maeneo ya Mwironge, Mwiruzi na Nyakayenze; chokaa katika eneo la Bumuli na katika eneo ya Keza, Kibingo, Nkuba pamoja na maeneo ya Kasanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti za kina zinahitajika ili kujua kina cha madini yaliyogunduliwa. Serikali inaendelea kuhamasisha makampuni mbalimbali binafsi ili kufanya utafiti wa kina na kuendeleza uchimbaji katika Jimbo la Kakonko.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape atafuatiwa na Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MBUNGE FULANI:** Wewe si una maswali mawili.

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**MWENYEKITI:** Ndiyo, Mheshimiwa Bilago halafu Mheshimiwa Nape. (*Kicheko*)

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ultaka kupanua goli. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri aliyotoa kwa swali hili, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, katika eneo hili ambalo lina chokaa linaloitwa Bumuli maarufu Ngongogwa liko katika Hifadhi ya Moyowosi - Kigosi. Wafanyabiashara wanaotaka kuchimba hiyo chokaa wamekuwa wakikwamishwa na shughuli zinazofanyika katika hifadhi na Mamlaka ya Hifadhi kuwazuia kufanya shughuli hiyo. Je, Serikali inaweza ikatoa utaratibu mahsus watakaofuata wananchi wa Kaknoko ili waweze kuchimba chokaa hiyo ambayo ni *grade two? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo dhahabu ambayo imepatikana sehemu za Nyamwilonge na Nyakayenze na maeneo ya Ruhuli inayoeendelea kuchimbwa na wachimbaji wadogo wadogo kwa kutumia zana hafifu. Je, Serikali iko tayari kutoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo hayo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Bilago lakini pia namshukuru kwa sababu anafuatilia sana maeneo ya wachimbaji katika maeneo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua nyingi sana, lakini kulingana na Sheria ya Madini na Sheria ya Hifadhi ya Mazingira, kifungu cha 95 cha Sheria ya Madini kinatoa utaratibu na utaratibu unaotumika hivi sasa kuchimba madini katika maeneo mengine kwanza kabisa mtu anaruhusiwa kupata leseni lakini akishapata leseni ya uchimbaji anawaona watu wa maliasili ili apate kibali cha maandishi na huo ndiyo utaratibu unaotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshatoa leseni 70 katika maeneo karibu na Hifadhi ya Moyowosi na hizo leseni wananchi wanachimba na kuna vikundi viwili vyta ushirika ambapo wanafanya kazi hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bilago utaratibu upo lakini ni vizuri tukaa zaidi ili nikueleweshe ili wananchi wa Jimbo lako wanufaike zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la nyongeza la pili, maeneo ya Nyamwilonge na Nyakayenze pamoja na Makele na maeneo ya mbali, maeneo haya tumeshatoa leseni kwa sababu kuna uchimbaji mzuri wa dhahabu. Mwaka 2012 kuligunduliwa dhahabu na tukalitenga eneo hilo na hivi sasa kuna leseni 76 katika maeneo hayo. Nimuombe Mheshimiwa Bilago awahamashe wananchi wa Jimbo lake ili eneo lilitobaki tulilolitenga pia walitumie kwa manufaa ya maisha yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa chanzo kikubwa cha migogoro kati ya wananchi na wawekezaji wanaoenda kuwekeza kwenye sekta hii ya uchimbaji wa madini ni utaratibu unaotumika wa kumalizana na wawekezaji kitaifa na kutowashirikisha vizuri wale wa Wilayani na pale kijiji ni penyewe ambapo utafiti au uchimbaji unakwenda kufanyika na mfano mzuri ni katika Jimbo langu la Mtama, Kata ya Namangale kuna utafiti unafanyika wa *graphite* na Kampuni ya *Nachi Resources* lakini mgogoro uliopo ni kwamba wananchi wa eneo lile hawaelewii kinachoendelea na hivyo kubaki na malalamiko mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lini Serikali itabadilisha huu utaratibu na kuwasaidia wananchi wangu wapate uelewa wa kinachoendelea ili waone ushiriki wao utakuwaje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Nape tumekuwa tukishirikiana sana katika hili na wananchi wa Mtama nadhani ni mashahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nisema utaratibu unaotumika ni kwamba mwekezaji yeoyote anayepata leseni, hatua ya kwanza akishapata leseni ni kuonana na uongozi wa Halmashauri au uongozi unaohusika wa wilaya na kama hilo halifanyiki ni uvunjivu wa sheria na sisi tutalismamia.

Lakini pia nichukue nafasi hii kusema kwamba tutapita katika maeneo ya kero, tumeshapanga utaratibu, kuanzia tarehe 02 Agosti, 2017 tunashughulikia matatizo hayo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Nape hata kwake tutafika. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rhoda.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Isulamilomo, Jimbo la Nsimbo katika Mkoa wa Katavi kuna mwekezaji yuko pale, hana leseni na kuna vijana zaidi ya 4,000 hawana leseni, lakini mwekezaji huyu sijui anapata nguvu gani ya kuwazuia hawa wachimbaji wadogo wadogo zaidi ya 4,000 kuchimba lakini zaidi wanapigwa na wananyanyaswa kwenye huu mgodi mpya ulioko katika Jimbo la Nsimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini tamko la Serikali sasa ili tujue nani ni halali kuchimba katika mgodi huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru kwa kutupa taarifa, lakini atusaidie zaidi mwekezaji huyu ni nani, utatusaidia sana Mheshimiwa Mbunge. Hebu tupatие huyo ni nani halafu tukafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la msingi ni kwamba maeneo yote ambayo wawekezaji wameyashikilia bila

kuyafanya kazi Serikali sasa inayatwaa kwa mujibu wa sheria ili iwagawie wananchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tutakaa pamoja tuone kero hiyo tuitatue kwa mujibu wa sheria, ikiwezekana kabisa tutachukua hatua za kisheria. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri na Waheshimiwa Wabunge, muda wetu leo hautoshi, kwa hivyo tumefikia mwisho katika maswali.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ambao ni wanafunzi 25 na walimu watano wa sole ya msingi *Compassion* kutoka Mkoa wa Njombe ambao ni wageni wa Mheshimiwa Lucia Mlowe (Mbunge) karibuni sana.

Pia kuna wageni 40 wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni wachezaji viongozi wa benchi la ufundi la timu ya *Simba Sports Club* wakiongozwa na Mussa Hassan Mgosi ambaye ni Meneja wa Timu hiyo.

Aidha tuna wanafunzi 60 wa Chuo cha Biblia Sanjaranda kutoka Mkoani Singida ambao pia ni wageni wa Mheshimiwa Yahaya Massare Mbunge, wakiongozwa na Mkuu wa Chuo ndugu John Tuu. (*Makof*)

Wapo wanafunzi 24 wageni wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambao ni wanachama wa Shirikisho la Vyuo vya Elimu ya Juu kutoka Mkoa wa Arusha karibuni sana. Pia tunao wanafunzi 30 wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) kutoka Mkoa wa Dodoma karibuni sana wanafunzi wetu, pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliokuja kutembelea hapa Bungeni wote kwa pamoja tunawakaribisha sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tunalo tangazo kutoka kwa Emmanuel Mpanda - Msaidizi wa Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa kuna maonyesho ya vifaa na teknolojia ya kisasa ya upimaji ardhi yanayoratibiwa na wanachama wa Chama cha Wapima

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Ardhi Tanzania (*IST*) katika viwanja vya Bunge, nyuma ya jengo la Utawala, hivyo Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kufika katika viwanja vya maonesho ili kujifunza jinsi ya kupunguza gharama za upimaji kwa kutumia vifaa na teknolojia ya kisasa.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee. Katibu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Katibu naomba tuendelee muda leo hautoshi kwa hiyo hatutakuwa na miongozo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Katibu naomba tuendelee.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi,  
Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa  
Mwaka wa Fedha 2017/2018**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza na wachangiaji wetu ninamkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, aweze kutengua Kanuni.

### **HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo ya hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jana wakati natoa hoja ya kutengua Kanuni, nilieleza kwamba sababu ya utenguzi wa Kanuni hizo ni mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambao unatarajiwa kuanza hivi karibuni na ni muhimu sana kwa Waheshimiwa Wabunge waumini wa dini ya kiislamu kufanya maandalizi ya kuanza mfungo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi ninaomba tena kutoa hoja ya kwamba Kanuni ya 28(2) na (4) itenguliwe ili katika kikao cha leo, badala ya Bunge kusitishwa saa saba mchana liendelee na mjadala wa hotuba ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na liahirishwe saa nane Mchana, hadi siku ya Jumatatu tarehe 29 Mei, 2017 saa tatu asubuhi. Sababu zikiwa ni zile ambazo tulizitoa jana na Waheshimiwa Wabunge waliziunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa, Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono.

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi,  
Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa  
Mwaka wa Fedha 2017/2018**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tunaanza na wachangiaji wetu ambao jana tuliwataja tunaanza na Mheshimiwa Yussuf atafuatia Mheshimiwa Martin tutaendelea na Mheshimiwa Mbowa.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bismillah Rahman Raheem*, nakushukuru kunipa fursa ya kuwa

mchangiaji wa mwanzo kwa siku hii ya leo kwenye hotuba ilio mbele yetu. Nisiwe mwizi wa fadhila nami niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Ardhi. Pongezi hizi zinatolewa kwa usimamizi mkuu wa wawili hawa au watatu hawa lakini wameshirikiana vizuri na watendaji wao ndiyo maana wakaweza kupongezwa na kila Mbunge anayesimama leo hii. Ni ombi langu kwao isije ikawa sifa ya mgema.

**MBUNGE FULANI:** Tembo akatia maji. (*Kicheko*)

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la migogoro ya ardhi, kuna migogoro mingi sana ya ardhi hapa nchini, sina haja ya kuitaja lakini nataka nimshauri tu Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake sasa hizi sifa zao basi ziende katika kutatua haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama eneo la ardhi ndani ya nchi hii liliopimwa ni asilimia 15 ndiyo eneo ambalo limepimwa na kupangiwa matumizi ni dhahiri kwamba mna kazi kubwa ya kufanya ili kuweza kupima eneo kubwa zaidi na kupangiwa matumizi ili kupunguza hii migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa faida za kupima ardhi na kupanga matumizi zimeonekana wazi, mimi kama Mjumbe wa Kamati nilipoenda Kilombero pale imeonekana tumejifunza, tumeona na wananchi wanafaidika sana, kwa sababu ile faida ya kupata Hati Miliki ya yale maeneo yao inawafanya wao sasa kuenda mbele kiuchumi na kufaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili sasa tatizo liko wapi, sasa hapa Mheshimiwa Waziri nadhani utanielewa wewe unaelewa vizuri zaidi lakini kwa mtazamo wangu mimi ninawaomba katika Serikali ni vizuri Waziri Mkuu leo yupo mkae katika Serikali, huu mkanganyiko wa kwamba watumishi wengi wa ardhi wako kwenye Halmashauri au wako chini ya Halmashauri ama TAMISEMI wako kule, na wewe sasa unataka kuipima ardhi ili wananchi wapate hati

miliki pamoja na kupanga mipango ya ardhi na hawa watu sasa hawajibiki moja kwa moja kwako, nani atawapatia vifaa nya kufanya hiyo kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri bajeti hii iko kwako, bajeti hii iko TAMISEMI, bajeti hii iko wapi? Sasa hili kama Serikali mkae ili kusiwe na *conflict of interest* hapa kwenye hii Wizara ama katika eneo hili ili vifaa nya kupimia ardhi vipatikane, wataalam wapatikane, ardhi ipimwe ili kuondoa matatizo. Serikali mpo Waziri Mkuu yupo mkae kama Serikali muondoe haya mambo ya kupeleka hawa TAMISEMI, hawa wapi, hawa wapi, mimi kwa mtazamo wangu ni mipango ya kiujanja ujanja iliyokuweko hapo, wekeni wazi hii Serikali ya Hapa Kazi Tu mfanye kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili niendelee kukupongeza kwa namna ambavyo umeweza kutumia busara na hekima kubwa kuwahamasisha wamiliki wa ardhi wakaweza kulipa kodi ya pango, ni kitu kimoja kizuri sana kimeleta tija na kila mmoja ameona faida yake. Tunakuomba uendelee kutumia *approach* hii ya kuwaelimisha na siyo nguvu, wanaomiliki ardhi kama ambavyo unatumia waendelee kulipa kwa faida ya nchi hii na pato la Taifa liongezeke. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa utakapokuja kujumuisha utuambie wale ambao wanamiliki mashamba makubwa, wanamiliki ranchi lakini hawajaziendeleza, hawazifanyii kazi ni wangapi na je Serikali ina mpango gani? Pamoja na hayo nipendekeze kabisa kwamba mashamba yale makubwa ambayo hayajaendelezwa pamoja na ranchi yatumike sasa kuwagawia au kuwaazima kwa muda hawa wafugaji wakati mkiendelea kufikiria ili kupunguza migogoro na vita nya wakulima na wafugaji wakati kuna maeneo kama haya ambayo hayajaendelezwa na watu wanayamiliki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuongelea suala la Kigamboni, ni takribani miaka tisa sasa wananchi wa Kigamboni kwenye ule mradi wa Kigamboni nyumba zao

hawawezi kuziua, hawawezi kutengeneza, hawawezi kufanya kitu chochote wanasubiri mradi, lakini ni miaka tisa mradi haujaanza, Mheshimiwa Waziri hatujui kwamba huu mradi utaendelea kuwepo au hautakuwepo. Kama hautakuwepo wananchi wale kwa muda wa miaka tisa mmewazuia kufanya chochote mtawafidiae na kama utakuwepo katika kipindi chote hiki mtawafidiae. Naomba Serikali ijpange hapa ili wananchi wale muwaondoe katika ugumu ule ambaa mmewapa hivi sasa, wanakaa wanasubiri mradi, miaka tisa ni mingi sana kwa maendeleo ya mtu binafsi, kwa Serikali ni kidogo, lakini kwa maendeleo ya mtu binafsi ni miaka mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *National Housing*, ninaomba Serikali pia ipo, *National Housing* inafanya kazi moja kubwa sana na kila Mtanzania leo hii anaona kazi inayofanywa na *National Housing*, wanastahili sifa kweli, wanajitahidi sana. Kuna nyumba za gharama nafuu ambazo wananchi maskini wanatakiwa wanunue zile nyumba lakini ukiziangalia siyo za gharama nafuu kulingana na patol mwananchi wa Tanzania uwezo wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba hizi siyo za gharama nafuu kwa sababu ya mambo mengi, moja kama kodi ya VAT kwa vifaa vyta ujenzi itaondolewa kwa watu hawa wa *National Housing* wataweza kujenga nyumba hizo na Mtanzania ye yote ataweza kununua, lakini kama kodi ya VAT haitaondolewa basi suala hili litaendelea kuwa gumu kwao. Vilevile gharama nyingine zinaongezeka wao wanapojenga zile nyumba wanaweka gharama za kuweka maji, umeme, barabara ambazo wao wanapaswa kuweka wenywewe. Sasa Serikali ipo, kama mmeamua kujenga nyumba hizo sehemu fulani, kwa nini Serikali haipeleki maji, ikapeleka umeme, ikapeleka barabara kwenye eneo lile kabla ya watu wa *National Housing* hawajaanza kujenga? Serikali ni moja lakini kwa nini kunakuwa na *conflict of interest?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nchi za wenzetu wanafanya hivyo, ukienda nchi zote za Arabuni na Ulaya kabla ya lile eneo kuendelezwa huduma muhimu za barabara

maji na umeme zinapelekwa kwanza, barabara, maji, umeme, shule, masoko yanapelekwa kwanza halafu ndiyo nyumba zinajengwa wananchi wanaenda kuhamia pale ikiwa huduma zote muhimu zipo. Kwa nini kwenye nchi yetu inashindikana?

Kwa hiyo, nikuombe tu Mheshimiwa Waziri kwamba hili nalo mliangalie katika Serikali ili watu hawa wafanye hiyo kazi kwanza kabla ya kupeleka ujenzi katika eneo basi huduma hizi muhimu ziende ili kupunguza gharama. Mkiendelea kwamba watu wa *National Housing* walipe gharama za kuvuta maji, walipe gharama za kuvuta umeme, walipe gharama za kutengeneza barabara, wananchi wa Tanzania kwa kipato chao wataendelea kushindwa kuzinunua nyumba hizi na mtazijenga mtaziweka zitakuwa hazileti ile faida iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani, lakini niendelee kukupongeza Mheshimiwa Waziri nikuambie kaza kamba, narudia isije kuwa sifa ya mgema, tunategemea kipindi kijacho tuendelee kukusifu zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yussuf, tunaendela na Mheshimiwa Martin Msuha ambaye atagawana dakika zake na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na baadae Mheshimiwa Mboge ajiandae.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ninayo mambo machache nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wake wote katika Wizara kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili la upimaji wa ardhi, upangaji na urasimishaji wa makazi, wananchi wengi walikuwa wanalisubiri kwa muda mrefu sana uliopita. Kule

kwetu Wilayani Mbinga zoezi hili limepokelewa kwa mikono miwili kiasi kwamba ukiangalia kwenye makadirio ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga wametoka kwenye shilingi bilioni tatu mpaka shilingi bilioni tisa, lakini makusanyo yao mengi yanatoka kwenye upimaji wa mashamba, muitikio ni mkubwa kiasi kwamba tunategemea pia kuboresha uchumi wetu wa Mbinga kuititia mpango huu wa upimaji ardhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kumpongeza Mkurugenzi wangu Gombo Samandito Gombo ye ye ni mtaalamu pia wa Mipango Miji na ndiyo maana zoezi hili linakwenda vizuri kule Mbinga. Ziko changamoto, changamoto ya kwanza ni elimu, mapokeo ya zoezi lenyewe wananchi wengi walidhani wakipimiwa mashamba yao Serikali inakwenda kunyang'anya mashamba hayo, inakwenda kumiliki mashamba hayo. Changamoto ya pili ni ada za ardhi za mwaka, changamoto ya tatu ni namna ya kugharamia upimaji mpaka watu wakapata hati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mara nyingine Mkurugenzi wangu alifanya hesabu, Mbinga tunapima kipande cha heka moja kwa shilingi 100,000 lakini bado kuna changamoto namna ya kwenda, mtu ana mashamba ya heka kumi ishirini, tumeshirikisha sekta binafsi wale ni wafanyabiashara wamepata *tender*, wangependa wapime kiasi kikubwa ili wapate zaidi. Kwa hiyo, unakuta wale wakulima wamelimbikiziwa madeni katika eneo hili la upimaji. Nitoe shilingi milioni tatu kwa mkupuo hapana, tunaongeza umaskini kwa upande mmoja kwa hiyo iratibiwe namna ya kutengeneza malipo ya gharama hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika zoezi hili yako maeneo ambayo watu waliona kama wanaonewa, kwa maana kwamba mapokeo yalikuwa watu wavunjiwe nyumba baadhi ya maeneo, kwa hiyo likaleta shida. Pale Mbinga Mjini maeneo ya Tangi la Maji kulitokea na Mkanganyiko huo mlanjenga holela kwa hiyo inabidi tuwavunjie kabla ya mipango miji kuwafikia, ikawa shida, mtu huyu amekaa hapa miaka yake hamsini unamvunjia leo nyumba

anakwenda wapi? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri hili litolee maelekezo vizuri. Kama mnaamua kurasimisha makazi ya watu basi elimu ishuke wale Watendaji kule chini waelewe ili, zoezi lenyewe litekelezwe namna gani, vinginevyo kuna kauonevu ndani yake na pengine utekelezaji wake sasa unasuasua kwa sababu hiyo watu wanasita kwa sababu wanahisi sasa hapa nitavunjiwa, hapa nitahamishwa. Mheshimiwa Waziri kwa upande wa Mbanga mimi nilikuwa nataka kusema hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko changamoto kwa upande wa upangiliaji, upimaji na urasimishaji wa miji, mimi ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Msingwa kule Dar es salaam Kata ya Msigani. Tunalo zoezi hili, tunayo kampuni binafsi ambayo imepitia kwenu Wizarani, imepitia Halmashauri, tumeshafanya mikutano kadhaa, mapokeo ni mazuri sana na nitumie pla fursa hili kukualika Mheshimiwa Waziri baada ya kumaliza mikutano hii nitakualika kwenye mtaa wangu tukazindue mpango wa upangiliaji miji kule Kata ya Msigani, tutaleta barua rasmi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapokeo ni mazuri, changamoto iliyoko kubwa ni gharama hizi za upimaji, bei elekezi ni kweli Serikali imetoa lakini gharama za umilikishaji ni tatizo, Wizara hamjaziweka wazi, kuna tozo pale zipatazo tisa mpaka uje upate hati mjini, ndio maana hati nyingi hazijatolewa kwa sababu ya hizi gharama za umilikishaji. Ziko gharama pale zinahesabika, ziko tisa. Iko gharama ya kuchukua *form, premium*, ada ya hati miliki, lakini iko ada ya uandaaji wa hatimiliki, hati ya usajili na tunayo ada ya uandikishaji. Sasa tulifanya ukokotoaji pale kwenye Mtaa wangu wa Msigani Dar es Salaam...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia sentensi yako, dakika zako zimeisha.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye kiwanja cha *square metre* 600 kinagharimu shilingi 873,000 ada ya umilikishwaji, acha ile ya upimaji kwa kampuni binafsi.

Kwa hiyo naomba Wizara muangalie upande huu, huo utatukwamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Christine Ishengoma dakika tano.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na Wafanyakazi wote wa Wizara hii. Pili, naomba kutoa pongezi kwa kazi wanayoifanya nzuri hasa Mkoa wa Morogoro kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyote mnafahamu kuwa Mkoa wa Morogoro ulikuwa na matatizo sana hasa kwa upande wa wakulima na wafugaji mpaka mapigano na mauaji yakatokea kwa upande wa watu na mifugo. Nashukuru Serikali kwa sababu Mawaziri walifika kwa kusaidiana na uongozi wa Mkoa pamoja na Wilaya waliweza kufanya kazi kadri walivyoweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa sababu dawa muhimu ya kumaliza hii migogoro ni upimaji wa ardh. Upimaji wa ardh ambao sasa hivi umefanyika kwenye Wilaya ya Malinyi, Ulanga pamoja na Kilombero kwa baadhi, nashukuru kwa sababu wametoa hata hati miliki na hiyo ndiyo ingekuwa mkombozi. Tufahamu kuwa hawa wanaopewa hati miliki ni wachache, naomba kwa sababu tumepata ufadhili kutoka Serikali ya Uingereza pamoja na Sweden na Denmark kupitia kwenye mashirika yao ya maendeleo ya *DANIDA*, *DFID* pamoja na *SIDA* nashauri Wizara kama inawezekana waweze hata watu wengine kupimiwa kwa sababu hata *registryambayo* ni masjala wameweza kujenga lakini watu wangeweza kumilikishwa wote ingekuwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mkao wa Morogoro ifahamike kuwa ni Wilaya zote zilikuwa na matatizo ya mifugo. Wilaya zote Mvomero nashukuru mmeweza kupima kiasi, Kilosa mmeweza kupima kiasi, lakini mfahamu kuwa watu walikufa Mabwerekere, watu walipigwa na hasa wanawake ambao walikuwa wanalima mpunga wao, wengi walikimbizwa hawawezi kulima.

Naomba sana tena sana kwa kusaidiana jinsi mlivyoweza kupata ufadhili kutoka kwa mashirika hayo, Mheshimiwa Waziri una wataalam wazuri ambao wanaweza kuandika maandiko ya kuweza kuomba *project* pamoja na kusaidiana na Halmashauri zetu za Wilaya ya Gairo, Kilosa, Mvomero, Morogoro Vijijini hata Manispaa pamoja na kule ambako tayari mmeshaanza kupima tuweze kupata kupimiwa ardhi kwa sababu ni majaribio yaweze kuwa majaribio ya Mkao mzima watu wote mlikuwa mnajua kuwa Mkao wa Morogoro ndiyo umeweka historia kwenye migogoro ya wakulima na wafugaji, kuweza kupimiwa ardhi kusudi tupate hatimiliki watu waweze kumiliki pamoja na tuweke historia ya kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri kuwa kwa Wilaya zingine Mikoa yote ya Tanzania ambayo inajulikana kwa migogoro hii ya wakulima na wafugaji pamoja na migogoro ya ardhi, dawa ni kupima ardhi, kupata hati miliki, hati miliki ambayo inaweza kukusaidia hata kupata mikopo lakini kujua kuwa ni ardhi gani mifugo itaweza kuwa, ni ardhi gani wakulima wataweza kuwa na ni ardhi gani wafugaji wataweza kuwa na hii tutakuwa tumepanga mipango mizuri ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua kuwa kwa sababu wataalam ni wachache na kuna vyuo, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo cha Ardhi Morogoro pamoja na Chuo cha Ardhi Tabora, udahili uweze kuongezwa ili kusudi tuweze kupata watumishi wengi wataalam wa ardhi huko kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niongelea kuhusu mipango ya miji. Bila ya kupanga miji itakuwa kuna ujenzi holela kama tunaoushuhudia watu wanajenga mpaka milimani na ninyi Wizara mpo, naomba na hilo mliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kushukuru sana nyumba za *National Housing* zimejengwa pamoja na nyumba za watumishi ardhi hata Mkao wa Morogoro tumepata lakini tatizo kama wenzangu wanavyosema gharama bado ni kubwa. Naomba muiangalie hiyo gharama ili kusudi hata wale vijana wanaoanza kazi sasa hivi, waweze kupata nyumba zao wakalipia kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunamkaribisha Mheshimiwa Mbewe sasa na baadae Mheshimiwa Saddiq Murad na Mheshimiwa Nsanzugwanko wajiandae.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Na mimi nafikiri nisiwe mchawi, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Lukvi na Naibu wake. Kwa kweli ni Wizara ambayo inafanya kazi bila itikadi za kisiasa, inasimamia wajibu wake vizuri. Mheshimiwa Waziri sifa unazopewa wewe na Naibu wako zinawastahili pamoja na Wizara yako yote, endeleeni kufanya kazi na tutawapa ushirikiano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo manne tu ya kuzungumza siku ya leo na yote naelekeza katika Jimbo langu la Hai. Kwanza, japo nafahamu ni suala linalohusu Wakala wa Barabara yaani *TANROADS* lakini kwa sababu linagusa ardhi nalizungumza ili Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, na nina hakika Mheshimiwa Profesa Mbarawa yuko hapa naye atanisikiliza, kwa pamoja mnaweza mkaona mnaweza kutupa vipi watu wa Hai ufumbuzi wa tatizo hili ambalo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili linahusu barabara

ya *Kilimanjaro Machine Tools* - Machame Girls'. Barabara yenyе urefu wa kilometra 26, barabara ambayo ilijengwa wakati wa ukoloni na ni barabara kuu inayohudumia eneo lote la Machame lenye wakazi zaidi ya 200,000. *TANROADS* wame-declare kupanua wigo wa barabara hii na waka-declare kwamba eneo la mita 60 linahitajika liwe reserved kwa ajili ya barabara. Sasa sisi hatuna tatizo na ulazima wa kupanua na kuimarisha miundombinu yetu ya barabara. Ni kweli sheria hizi inawezekana kuna sheria ambazo zinasimamia mambo haya, lakini sheria hizi zinatungwa na Bunge na tukitunga sheria mara nyingi tunatunga sheria kwa kuangalia nchi nzima bila kuangalia mazingira mahsus ya eneo moja baada ya jingine.

Mheshimiwa MWenyekiti, kwa eneo la Kilimanjaro ambako makazi yana watu wengi sana, mashamba hakuna. Watu wenye miaka 50 kushuka chini hawana ardhi, kuchukua eneo la barabara ya mita 60 ambayo inakwenda kwenye forest pamoja na *Kilimanjaro Gate (Machame gate)* kwenda kwenye National Park ni eneo kubwa sana. Tutambue kwamba kuna wakazi wamekaa kwenye maeneo haya kwa zaidi ya miaka 100 iliyopita na kupanua barabara kwa upana huu maana yake ni kwamba tutabomoa misikiti, shule, makanisa, makaburi, tutapoteza kabisa flow ya Mto Weruweru, tutakata mashamba ya wananchi, hili ni jambo lenye ugomvi mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upanuzi huu unazungumziwa kufanyika bila kulipa fidia. Ningependa kuishauri Serikali katika kutekeleza sheria lazima tuangalie mazingira ya maeneo na historia ya maeneo. Hii barabara ni muhimu ndiyo, lakini hajengwi reli, wala hatutegemei kwamba kweli mita zote 60 zitatumika katika kuipanua barabara hii, kwa sababu inakwenda ndani kwa kilometra 13 tu kuanzia maeneo ambayo wanakaa wakazi unaanza kukuta Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali, Waziri wa Barabara, Waziri anayeshughulika na mambo ya miundombinu pamoja na Waziri wa Ardhi tutafute ufumbuzi

na ikiwezekana tafadhali m-*visit* Wilaya ya Hai, mkaangalie hali halisi ninayoizungumzia mahali hapa, muelewe namna ambavyo vijiji nya Nshara, kijiji cha Uduru, Warisinde, Warindoo na Foo katika Kata ya Machame Kaskazini mpaka kwenye Mronga na Mkuu wote hawa wanaathiriwa. Kwa hiyo ni jambo ambaao kwa kweli linawakwaza sana wananchi. Bomoabomoa hii japo mnaona ni kilometra 13 kwa Hai, inagusa zaidi ya wananchi 6,000, zaidi ya kaya 800 zinaguswa katika jambo hili bila kuzungumzia hizo taasisi ambazo nimezizungumzia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni jambo la kwanza ambalo ningependa kushauri Serikali na ningeomba sana Waziri katika majibu yako, na pengine niombe Waziri Mheshimiwa Mbarawa na timu yake nao vilevile pengine washirikiane katika kutupa ufumbuzi, tungependa tumalize hill tatizo bila kuleta mgogoro wa ziada na usumbufu usio wa lazima sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili Mheshimiwa Waziri ni kuhusu hali nzima ya ardhi katika Mkoa wa Kilimanjaro. Tatizo kubwa la Mkoa wa Kilimanjaro ni ardhi. Tuna uhaba mkubwa sana wa ardhi, nitakiri kwamba ni Mkoa ambaao idadi ya wakazi kwa kilometra za mraba ni kubwa kuliko kijiji chochote katika Afrika Mashariki na ya Kati.

Tunapozungumzia Kilimanjaro, kilomita moja ya mraba sehemu za milimani zina watu kuanzia, ikipungua sana ni 650 mpaka  $1,800 \text{ per square kilometer}$ , hii *density* ni kubwa kuliko eneo lolote katika Afrika ya Mashariki na Kati. Watu wenye umri wa miaka 50 kushuka hawana ardhi kabisa sasa hivi na watu wameendelea kujenga, *population* imendelea ku-*increase* kwa *rate* ya  $1.9 \text{ people per annum}$  ambayo siyo kubwa sana ukilinganisha na maeneo mengine ya nchi, lakini kwamba kuna tatizo kubwa la ardhi ambayo inahitaji *special management* hili ni la lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namuomba Waziri wa Ardhi mfanye *land auditing* ya Mkoa wa Kilimanjaro, siyo Hai peke yake, Mkoa mzima wa Kilimanjaro. Kwa sababu

katika maeneo mengine sasa watu wamejenga nyumba mpaka kumekuwa *squatters*, kuna *squatter* za vijijini. Sasa siyo kawaida sana kukuta *squatter* vijijini, kuna *squatter* za vijijini, kuna shida ya kupitisha huduma za barabara hizi *feeder roads*, kuna tatizo kubwa sana ambalo linahitaji kwa kweli kufanyiwa *intervention*. Ningombwa Serikali Kuu ifanye *intervention* na kama kawaida Mheshimiwa Waziri nakukaribisha ili uje na wengine kuangalia mnaweza kufanya jambo gani katika kutatua tatizo hili la wakazi wa Hai. (*Makofii*)

Jambo la tatu nizungumzie mashamba ya ushirika. Huko miaka ya nyuma wakati wa utawala wa Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Nyerere alitaifisha mashamba makubwa yaliyokuwa ya wawekezaji wa kizungu na akakabidhi kwa vijiji kadhaa vya Wilaya ya Hai na maeneo mengine ya Mkoa wa Kilimanjaro. Baadae yale mashamba yakahamishwa kupelekwa kwenye Vyama ya Msingi vya Ushirika, lakini baada ya Sheria ya Ushirika kubadilishwa yale mashamba hayakuwa tena miliki za vijiji yakawa ni washirika wale wanaushirika ambao ni kundi katika kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mashamba yame-*hold* uchumi mkubwa sana wa Wilaya ya Hai na katika Mkoa mzima wa Kilimanjaro. Ni ombi langu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Waziri wa Ardhi mje tuyafanyie tathmini mashamba haya. Hivi kweli kuna *economic value* tunayopata kwenye mashamba yale ama yanatumika tu bila kutengeneza kile ambacho kilikusudiwa. Kama ni lazima tubadilishe matumizi yake yeweze kurejeshwa kwa wananchi, yeweze kuwa na tija zaidi katika kukuza uchumi wa Mkoa wa Kilimanjaro hasa ukizingatia namna ambavyo ardhi imekuwa nijambo adimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mashamba makubwa yamekodishiwa watu, hawalipi katika Vyama vya msingi vya Ushirika, wananchi hawafaidi chochote wakati wananchi wengine wa kawaida hawapati hata robo eka ya kulima. Kwa hiyo ni jambo ambalo linatakiwa kupatiwa ufumbuzi, ningombwa sana Waziri hili uliangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia liko pale pale katika masuala ya ardhi ni kuhusu mgogoro wa *KIA*. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anisikilize vizuri kwa sababu Waziri Mkuu hili jambo amelisikiliza kwa muda mrefu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba Mkuu unisikilize sana katika hili unisaidie vilevile. Mheshimiwa Waziri Mkuu, unakumbuka bado mgogoro wa *KIA* tumeushughulikia, nakushukuru sana kwa *effort* yote uliyofanya, lakini bado hatujapata ufumbuzi, kwa sababu lile eneo la mgogoro wa *KADC O* uwanja wa Kilimanjaro wa *KIA* umegusa maeneo ya wananchi wa vijiji vitano vya upande wa Wilaya ya Hai na vijiji kadhaa katika Wilaya ya Arumeru kwa ndugu yangu hapa Mheshimiwa Nassari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vya Hai kama Mtakuja, Tindigani, *Sanya Station*, Rudugal, Chemka vimeathirika, kwa kipindi chote hiki chenye mgogoro wananchi wamenyimwa kufanya shughuli zozote za maendeleo katika maeneo yao mpaka mgogoro huu utakapotatuliwa.

Kwa hiyo, kuchelewa kutatua mgogoro huu na kuwapa wale wananchi haki ya kuendelea kuishi katika maeneo yao kunakwaza sana maendeleo na ujenzi wa huduma za kijamii kama shule, barabara, miundombinu nyingine, umeme, maji na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ningeomba sana tusaidiane tumalize tatizo hili, kwa sababu kuna suala la mgogoro wa ardhi na kuna suala la *KIA*. Suala la *KIA* hilo ni suala lingine na Waziri Mbarawa naye amekuwa anashughulika na Waziri Mkuu, nawashukuru sana, lakini ardhi kwa wale wananchi waliozunguka eneo hili inakuwa ni tatizo kubwa kweli kweli. Kwa miaka kadhaa sasa wananchi hawawezi kufanya chochote wamekaa kwenye vijiji vyao, hawaruhuswi kujenga, kupanua mashamba, hawaruhuswi kufanya chochote cha maendeleo ya kudumu. Sasa jambo hili ni gumu kidogo hasa inapogusa wananchi wengi sana katika Wilaya ya Arumeru na Wilaya ya Hai ambayo wote wanagusa eneo la *KIA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu nikucombe ile juhudini uliyokuwa umeianza uimalizie, Waziri Mbarawa atusaidie tumalizie jambo hili na Waziri Lukuvi nae vilevile aje tuwa-*relieve* hawa wananchi. Kama tutaendelea na mazungumzo kuhusu uwanja wa *KIA* tuendelee, kuhusu uwekezaji wa uwanja wa *KIA* na *KADCO* tuache wananchi katika maeneo yao waweze kufanya shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani Waziri Mkuu umelifanyia kazi vema jambo hili na nina hakika ukiamua wewe na Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa Mbarawa mlimalize tatizo hili, mnao uwezo wa kulimaliza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuruni sana na nawatachia kheri. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbewe. Tunaendelea na Mheshimiwa Saddiq Murad, dakika tano na Mheshimiwa Nsanzugwanko dakika tano. Baadae Mheshimiwa Millya na Mheshimiwa Nassari wajialandae.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo. Na mimi naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wao, lakini salamu za kipekee kwa Mheshimiwa Waziri, amefanya kazi kubwa sana katika Mkoa wa Morogoro na Wilaya ya Mvomero. Mheshimiwa Waziri kazi uliyofanya Morogoro ni ya historia, migogoro ya ardhi imepungua, migogoro ya wakulima na wafugaji inaendelea kupungua. Tunaomba jicho lako la huruma liendelee kutusaidia wananchi wa Morogoro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekeze matatizo yafuatayo kwa sababu muda wenyewe ni mdogo. Mheshimiwa Waziri, suala la kwanza tuna mgogoro wa mipaka ya kiutawala kati ya Manispaa ya Morogoro na Wilaya ya Mvomero, huu mgogoro ni mkubwa sana, naomba sana utusaidie. Halmashauri ya Mvomero imeanzishwa kwa *GN* yake, Manispaa ina *GN* yake, lakini tunaomba sasa hivi

Mheshimiwa Waziri, Ofisi yako, wataalam wako waje watoe tafsiri ya *GN*. Mgogoro unazidi kuendelea, mipaka inaingiliana na wananchi wa Mvomero wanakosa haki kwasabbau Manispaa wanaingilia eneo la Mvomero na wanaanza kugawa ardhi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba kauli ya Serikali katika suala hili na tunaomba sana uje utusaidie Mkuu wa wilaya, wataalam wa Mvomero na wananchi pia tumeanza zoezi hili lakini halina mafanikio kwa sababu tunahitaji nguvu kubwa ya Serikali.

Mheshimiwa Waziri, jambo la pili ambalo ningependa sana kulizungumza kwa sababu ya muda nao unakwenda ni kuhusu ardhi kubwa. Mvomero kuna ardhi ambazo hazijaendelezwa, kuna ardhi inaitwa *Katenda Group* hawa wana heka 12,500 tangu mwaka 2002 mpaka leo ardhi haijaendelezwa. Mheshimiwa Waziri tunaomba ofisi yako sasa itusaidie kutupatia ardhi hili ili wananchi wa Mvomero na Watanzania wengine waweze kufaidika na ardhi yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu Mheshimiwa Waziri ni upungufu wa wataalam. Mvomero tuna upungufu mkubwa wa wataalam. Nimpongeze Mheshimiwa Rais amevunja *CDA*, wataalam wa *CDA* nawakaribisha Mvomero. Tusaidiane wataalam waje Mvomero, tunahitaji baadhi ya wataalam katika maeneo yafuatayo. Tunahitaji Maafisa wa Mipango Miji wawili waaminifu, huo ndiyo upungufu wetu wa kwanza, wa pili tunahitaji Mthamini, na Mrasimu wa Ramani. Tunaomba Mheshimiwa Waziri kwa kuwa haya mambo mengine nitakuwa nayo kwa maandishi nitakuletea, tunaomba tupate watumishi hawa ili Mvomero sasa isonge mbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ni kutopata gawio la asilimia 30. Mvomero tunadai zaidi ya shilingi milioni 178, gawio hili hatujalipata bado. Mheshimiwa Waziri, kuna ahadi za Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa William Lukuvi alizozitoa Mvomero. Naomba kuzitaja ahadi zake, ahadi ya kwanza aliahidi kutuletea vifaa vya upimaji (*RTK*) vifaa hadi leo Mvomero hatujavipata. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaomba utusaidie ahadi yako, tekeleza, tuletee vifaa vya

upimaji. Ahadi ya pili tunaomba kukamilisha uandaaji wa mipango na matumizi ya ardhi kwa vijiji 52 kati ya vijiji 130. Ahadi ya tatu Mheshimiwa Waziri tunaomba ukamilishaji wa upimaji wa mipaka ya kiutawala vijiji 32 kati ya vijiji 130. Mheshimiwa Waziri tunaomba sana utusaidie vifaa vya upimaji ili Mvomero tusonge mbele zaidi na zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mvomero hatuna ofisi ya ardhi, tunatumia ofisi ya Idara ya maji. Sasa umetoa ofisi tatu na unaendelea na mipango mizuri kwa maeneo mengine Mvomero umeisahau, tunaomba kwenye mipango yako mizuri uweze kutusaidia ili na sisi tuwe na ofisi ya ardhi. Mwisho ni kuhusu Ofisi ya Kanda ya Mashariki ambayo baada ya kutoa tamko rasmi sasa kwamba Kanda ya Morogoro inaondoka na badala yake tunahamia huku Dodoma. Mheshimiwa Waziri kwanza nikupongeze ulianzisha Kanda mwaka 2015, ukajenga ofisi nzuri Morogoro, ofisi imefanya kazi nzuri wananchi wa Mikoa ya Pwani na Morogoro wamepata Hati zaidi ya 5,000; sasa kuondoa Kanda leo na kurudisha tena Dodoma kwa kweli naona unaturudisha nyuma.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Murad.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri masuala yangu mengine nikuletee kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nsanzugwanko, hayupo. Tuendelee na Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naomba nichukue furasa hii kwanza kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Ardhi kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya na kuleta

matumaini makubwa. Migogoro mingi imeendelea kupungua na tunaendelea kuomba kwamba waendelee kufanya kazi hiyo kubwa ili migogoro ya ardhi sasa hapa nchini iishe. Tunaomba ile migogoro hasa ile ya Babati ambayo Wabunge wenzangu wote tumekubaliana kila anayepata fursa asemee, ile ya vijiji vya Ayamango, Gedamar na Gidejabug wale wananchi wapatiwe maeneo mbadala kuna mapendekezo tumeshaleta, Serikali kuitia Ofisi ya Waziri Mkuu ifanyie kazi ili Wizara ya Ardhi iweze kutoa vibali, lakini pia ile migogoro ya mashamba ya kule Kiru yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu Mheshimiwa Waziri ninaomba utuletee sheria mpya hapa ndani ya hii Sheria ya Ardhi kipengele cha kuzuia matumizi ya ardhi ya kilimo ilindwe kisheria ili ukitaka kubadilisha matumizi ya ardhi ya kilimo ije hapa Bungeni kwa sababu maeneo mengi yenye rutuba Tanzania yamebadilika matumizi sasa yamekuwa makazi, viwanda na matumizi mengine ambapo hayo matumizi mengine tungeweza kuyapangilia yakawa katika maeneo mbadala na italinda ardhi yetu ya kilimo, kwa sababu hatuna uwezo kama Serikali kuandaa maeneo mapya ya kilimo katika maeneo ya jangwa au maeneo ambayo hayana rutuba kuwa ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeomba kwamba la Wabunge wote wamelalamikia suala la kupatiwa vifaa, mpango wenu mzuri wa kuweka vifaa vya kupima kwenye Kanda haitoshelezi, tunaomba muwe na mpango, mtukopeshe wala hatuhitaji kwamba Serikali iweke bajeti ituletee bure, kila Halmashauri tukopeshwe vifaa ili sisi tutaendelea kulipa hilo deni la vifaa vya kupimia ardhi zetu, ili tupime viwanja vya watu, mashamba ya watu lakini pia vifaa vya kutolea hati miliki zile za kimila huko katika Halmashauri zetu. Hiyo itatupunguzia sehemu kubwa ya matatizo ili wananchi wote waweze kupata huduma ile muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hapo naomba kwamba kuna ile asilimia ambayo kodi ya ardhi inapolipwa

ile Wizara basi iwe badala ya kufika Hazina na huko Halmashauri iweze kukata moja kwa moja ili tuweze kuyapangia matumizi ya ile fedha ambayo tunawasaidia Wizara kukusanya ile kodi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna migogoro mingi ambayo sasa hivi kwa sababu Serikali haijatoa tamko maalumu kwamba watu kuvamia maeneo ya hifadhi, kuvamia maeneo mbalimbali na katika mali za watu Serikali iweke msimamo kwamba nini maamuzi ya Serikali na mahali ambapo Serikali huko nyuma tayari ilishakosea kwa kuanzisha vijiji ndani ya maeneo ambapo ni hifadhi au ni mashamba mengine ya *lease*, basi mgogoro huo utatuliwe mapema ili kila mmoja aweze kuishi kwa amani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine pia naomba iangaliwe namna kwa wale wallikuwa Watanzania ambao sasa wamebadilisha uraia wao kwenda nchi zingine ili huko wapate haki, pawe na mpango maalum. Najua Wizara ya Ardhi mnao mpango masuala ya *derivative rights*, lakini waweze kurudi nyumbani angalau kama wanataka kuwekeza kujenga nyumba na kadhalika, waweze kuwa na haki hiyo kwa sababu kuna *diaspora* kubwa ambao wana uraia wa kule lakini ni Watanzania kiasili na wao waweze kupata haki yao kuja kuwekeza hapa nyumbani bila kuwa kupitilia *TIC*. Labda anataka kuweka nyumba tu ya kuishi na nini na wengine wana ndugu zao ambao wapo hapa, lakini wakirithishwa ile mali ni haki yake kurithi ya mzazi wake au baba yake au babu yake, akija hapa inakuwa ni mgogoro kwa sababu yeye tayari anao uraia wa nchi nyingine. Watanzania wengi wanakosa fursa hiyo naomba muangalie namna kwa wale ambao walikuwa Watanzania wameenda wamebadilika sasa kuwa raia wa nchi nyingine aendelee kuwa na haki maalum, kuna haki zingine wasipewe lakini angalau hii ya kwao ya kuja kuwekeza humu nchini basi pawe na mfumo mzuri waweze kuja na kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu na ninaendelea kusisitiza kwamba hivi vifaa tumeona pale nije mmetuletea aina nyingi, pawe na mpango maalum tuweze kukopa kila

Halmashauri kwanza itakuwa fursa ya kumaliza migogoro ya watu kupatiwa hati miliki na hati za kimila, lakini pia maeneo mengi yatakuwa yamepimwa, muhimu ni *coordination* baina ya Halmashauri zetu na Wizara, namna ya kuelekeza Maafisa Mipango Miji na namna ya kupanga makazi hata huko vijijini tunahitaji kupanga matumizi bora ya ardhi ili huko mbele tunakoelekea migogoro isiendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni, tunaendelea na Mheshimiwa Millya, baadae atafuatia Mheshimiwa Nassari, Mheshimiwa Daniel Mtuka, Mheshimiwa Joram Hongoli na baadaye Mheshimiwa Moshi Kakosi ajiandae

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa dakika tano ni mdogo sana nifanye mambo mawili, moja nimkaribishe sana Mheshimiwa Lukuvi Simanjiro, matatizo ya Simanjiro Wizara ina takwimu inaongoza Tanzania kwa kuporwa kwa ardhi yake, lakini la pili kwa sababu Wizara yako imesogezwa tarehe, wananchi walikuwa wapo tayari kuja kukuletea matatizo yao, ninaomba hata baada ya kupitisha bajeti yako wananchi wachache waje kukusalimia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mwaka 2005 nilikuwa kijana peke yake wa Wilaya nzima aliye *graduate degree* ya kwanza, baada ya miaka mitatu baadae ndio mwingine mmoja anapatikana. Kwa nini ninasema hivyo, Wilaya ya Simanjiro imejaa watu wengi ambao hawajasoma, wale wachache wanaojua kuandika na kusoma waliopewa Tarafa; waliopewa kuwa Wenyevitii vya Vijiji wame-take advantage ya hali ile na kuwaumiza wananchi na kuwachukulia ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Waziri fika Simanjiro hali ni mbaya kweli kweli, lakini niseme tu kitu kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mashamba makubwa, shamba namba 24 Lorbosoit ya aliye kuwa Katibu Tarafa ya Emboreet Mzee Brown ambaye bahati mbaya au nzuri ni Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, amechukua heka 8,000 lakini kama haitoshi, baada ya kushindwa kulima na kufugia amebadilisha shamba lile anataka kufanya ni la wanyamapori na kuwauzia Wazungu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri umetoa *directives* nakumbuka kama Waziri ulisema hakuna kubadilisha ardhi yoyote, kubadili matumizi yake bila idhini yako, huyo Mzee anafanya ujanja kutumia nafasi yake ya CCM kubadilisha mazingira hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Muhindi mwiningine Kata ya Loiborsiret, Kijiji cha Loiborsiret eneo la Motio, ameamua kuchukua ardhi kubwa ya wananchi kununua moja, moja heka mia, mia mbili lakini sheria zipo wazi, haiwezekani kijiji kikawa na uwezo wa kugawa zaidi ya heka 50 haiwezekani, Mheshimiwa Waziri nakuomba usaidie hilo. Kuna kijiji kingine cha Narakauwo mtu anaitwa Jerry Hoops amekuja ameingia kama mbia mwenzake na Mtanzania mmoja, alichukua heka 2,000, shamba lile lipimwe lina zaidi ya hekta 10,000 mpaka sasa hivi naomba uliingilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Kilombero kuna zaidi ya mashamba 50,000, maelfu na maelfu ya hekari ambayo yamechukuliwa. Mheshimiwa Waziri tatizo hili hatuwezi kukusaidia kwa dakika hizi tano ninakuomba Mheshimiwa Waziri ninakukaribisha uje Simanjiro, umeenda Arumeru, umeenda Monduli, umeenda Babati naomba uje Simanjiro wanakusubiri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Naberera kuna Mwenyekiti wa Kijiji amekuwa ni mtu wa ajabu naomba uangalie, kwa kweli mimi kwa ufupi niongee kwenye hilo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo pale Wizarani kwako una watu mahiri kweli, kuna mtu anaitwa Ndugu Lwena ninamfamu ni mwanasheria mahiri kweli hali rushwa ni mtu ambaye sijawahi kuona, nimeishi naye

nimefanya naye kazi mwaka 2009, anaweza kukusaidia. Kuna kesi ya Lekengere, Faru Kamunyu *and others versus Minister of Natural Resources and Tourism* ya mwaka 2002, Mahakama ya Rufani ilisema huwezi ukachukua ardhi inayomilikiwa kimila bila kupata idhini ya Rais. Rais peke yake ndiye mwenye uwezo wa kufanya hivyo. Ukiti pamoja na Sheria ya *Land Acquisition Act* ya mwaka 1967, pamoja na kuwapa wananchi fidia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri naomba utusaidie Simanjiro imeoza, walio tutangulie wengine kwenye madaraka hayo hawajatumia vizuri, ninaomba tusahihishe historia, watu wangu wanaumia, ardhi inaumia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nirudie kwenye suala la ardhi Mkoa wa Arusha kwa ujumla. Kuna watu walioletwa na Mwalimu Nyerere kwa nia njema ya kuwekeza, baada ya kumaliza uwekezaji na kuchukua ardhi yao, sasa wanayageuza mashamba yale kama mtaji. Inawezekanaje Tanzania akanunua ardhi yake peke yake, sana Serikali muingile, kuna watu wakubwa wana mashamba makubwa pale Arusha, Arumeru na unafahamu. Mzungu anataka kwenda ulaya kwenda *ku-retire* kukaa kwenye nyumba ya wazee, anabadilisha ardhi yetu kama sehemu ya kiinua mgongo chake, badala ya ninyi kusimamia arudishiwe *machinery* na gharama ambazo ametumia kwenye shamba lile, anatuuzia mashamba yetu, *NHC* walinunua kule Kisongo, ninampongeza Ndugu Msechu ni kijana mzuri mwenzetu anafanya kazi kubwa ninaomba tembelea Angola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mniamchanganya kama Serikali, hamjui kama mpo kwenye ubepari, hamjui mpo kwenye ujamaa *you just confuse, philosophy* mnachanganya mpeni afanye biashara ili atakapopata faida aendelee kusaidia watu maskini wengine, lakini mniamchanganya ni mtu mzuri mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mungu awabariki sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nawashukuru waliotangulia kuchangia Mheshimiwa Mboge na Mheshimiwa Millya angalau wamegusa kidogo masuala yetu na hili suala la *KIA* na wananchi wa vijiji vinavyozunguka nashukuru leo limesemewa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwa hiyo nina uhakika limechukuliwa kwa uzito mkubwa zaidi kuliko ningelisema mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana niliongea sana hapa Bungeni, nillia sana, Mheshimiwa Lukuvi unakumbuka ombi langu kubwa kwako likuwa ni kama ikiwezekana uje Meru nikuambie nini cha kufanya kwenye mashamba yaliyoko Meru ambayo yaliachwa tangu enzi za walowezi wallokuwepo Meru kwa wale mnaojua historia, nllisema hapa mwaka 1952 watu wa Meru walimtuma Umoja wa Mataifa Ndugu Kiliro Japhet Ngura Ayo, miaka tisa kabla ya Uhuru alikuwa ni Mtanganyika wa kwanza aliyekwenda Umoja wa Mataifa kwa sababu ya kudai ardhi la Meru, *Meru land case*.

Sasa nishukuru tu kwa Waziri Mkuu kwanza, pili kwa Waziri wa Ardhi ambao wote mlikuja kwa pamoja na Waziri Mkuu alitoa yale maelekezo na Waziri ukaja na tukafanya kazi nzuri sana kwa pamoja, kwa kweli nikushukuru mno na niseme tu kwamba unapokuwa mpinzani siyo unapinga kila kitu kinapofanyika kitu kizuri huwa tunasema na leo mmeona kwa Waziri Lukuvi hapa amesifiwa mpaka na Kiongozi wa Upinzani, kwa wale Mawaziri wengine ambao mna-ego, huwa mnajisikia na huwa hamsikii, jifunzeni kwa Mheshimiwa Lukuvi, nafikiri mtawenza kutengeneza Serikali nzuri sana, na niliwakumbusha nikasema nikasema kuwa hii dunia inazunguka leo Mheshimiwa Profesa Muhongo naye anauliza maswali ya nyongeza humu ndani, juzi alikuwa huko.

Kwa hivyo *ego* siyo kitu kizuri sikilizeni Wabunge wanaleta vilio gani kwenu, halafu muende kusikiliza msaidie Watanzania, kwa sababu dunia inazunguka kwa kasi niliwahi kusema. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, niseme tu baada ile baada ya ziara yako Mheshimiwa Waziri kule Meru, tulikubaliana kwamba Baraza la Madiwani na hususani Kamati, tufanye ziara kwenye mashamba yote na kujionea halafu tuandike mapendekezo ambayo yatakuwa na *consensus* ili yaweze kupita Mkoani kuja kwako ili uweze kufanyia kazi. *It is very unfortunate* na nilikuambia siku ile nikiwa jukwaani pale nikasema kunaweza kuwa na mashaka kwamba kusitokee *consensus* au siasa za kipuuzi ambazo zimekuwa zikiendelea kwenye Wilaya nyingi nchi hii, zikafanyika na pale Meru zimefanyika kwenye ziara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mapendekezo ambayo yamekuja kwako nashukuru Mungu yamerudishwa nyuma kuja kuanza upya hayakuwa na *consensus* hata kidogo na yatakayoletwa tena nakuomba ufanye *verification* utuulize wawakilishi wa wananchi, uwaulize Madiwani uwaulize Wenyeviti wa Vijiji, kwamba haya mapendekezo yamekuwa na *consensus* au yametoka kwenye ofisi moja pale Wilaya kuja moja kwa moja kwenye ofisi yako bila kuzingatia nini wawakilishi wa wananchi kwa maana ya Madiwani walichokipindekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo ripoti ya kwanza iliyokuja kwako utaona ndani yake, vile vilio ambavyo nimekuwa nikiongea hapa ndani havijasikilizwa, havijaainishwa ndani yake kabisa, utaona kabisa inaandikwa ripoti ya kuja kumnyang'anya mtu shamba heka 10, heka 18, Meru hatulillii heka 10 na 18 tunalilia *thousands of acres, hundred of acres*. Mashamba ambayo yalikuwa yanamilikiwa na Walowezi ambayo yalipata kibali cha Rais pia miaka ya mwanzo ya tisini kufutwa, lakini usajili haukufanyika ambapo imerudi kwenye mikono ya baadhi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nilikukumbusha nafikiri unafahamu vizuri kwa mfano, shamba la *Tanzania Plantation* kwanza nikushukuru kwamba ulikubali kutoa hata fedha kutoka Wizarani kwako kwa ajili ya upimaji na yule mtu alikuwa ameshakubali, mkakubaliana kwamba anabaki na kiasi gani na kiasi gani kiende kwa wananchi, *it*

*is very unfortunate kwamba amekwenda Mahakamani kufunga mikono.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya watumishi wa ardhi kwenye Mkoa wetu Arusha siyo watu wazuri kwako naomba nikuambie na ndiyo wanaokwenda kuwashawishi hawa Wazungu kwamba nendeni mkafungue kesi Mahakamani mfunge Wizara mikono, mfunge Halmashauri mikono, hakuna kinachoweza kufanyika. Ukweli ni kwamba huyu Mhindi wa *Tanzania Plantation* na sijui polisi wetu wa *Interpol* wanafanya kazi gani hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu huyu bwana ana *passport* mbili, ana *passports* ya Tanzania na ana *passport* ya Uingereza, na nchi hii haijaruhusu *Dual Citizenship*, tumefanya uchunguzi kabisa mara nyngi akiondoka nchini huwa anakwenda Nairobi anaruka na *passport* yake ya Uingereza, na huyu amekufunga mikono Mahakamani, naomba watu wa Mambo ya Ndani wakusaidie. *It is very easy kum-capture* huyu bwana, kwa sababu unaangalia rekodi zake za safari na unaangalia kwenye *passport* yake ziligongwa mihuri lini na lini na tarehe gani kwa sababu kuna tarehe ambazo ameondoka ambapo *passport* yake ya Tanzania haina hiyo mihuri kabisa, kwa hiyo huyu bwana anatuibia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Waziri anakumbuka kwenye ile *list* tuliweka hiyo *list* ambayo imekuja kwako ambayo nimesema haikuwa na *consensus* liliandikwa na shamba la Karamu, shamba la Karamu tumefanya mazungumzo na Halmashauri pamoja na mmiliki tumembana na amekubali kuingia kwenye *terms* ambazo Halmashauri kwa maana wananchi wa Meru wanafaidika, vijiji vinavyozunguka kwa maana vijiji vya Ndato na Mkwaranga wanapata *share* yao na Halmashauri inapanga ule Mji na ule ni Mji ambao ukiangalia *master plan* ambayo unakuja kuizundua mwezi wa Agosti Arusha, imependekeza lile eneo liwe ni eneo la *residential, low density* na hilo ndilo lengo letu tunakoelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema tulete kwako ufute atakwenda Mahakamani atakufunga mikono tena tutafanya nini, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninaomba tu kwamba hilo liweke kwenye kumbukumbu zako. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kengele niseme tu mengine nitayaleta kwenye maandishi ikiwemo mgogoro wetu ikiwemo na wa Hifadhi ya Arusha na vijiji vinavyozunguka na Momela na mingine pia na *issue ambayo ameiongea* Mheshimiwa Mbewe lile shamba la Valeska tuende kwa staili aliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunisikiliza. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nassari. Tunaendelea na Mheshimiwa Daniel Mtuka baadaye Mheshimiwa Joram Hongoli na Mheshimiwa Moshi Kakoso ajiandae.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi hii fupi nitazungumzia mambo mawili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Wizara, nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, niseme tu kwamba Wizara hii mmeibadilisha mmeitoa mbali mmeibadilisha, wataalam wa ardhi tunajivunia sana kwa kweli kazi mnayoifanya mko *aggressive*, lakini pia mna-*confidence* na lakini la mwisho ni wachapakazi, tunawapongeza kwa hilo sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maombi mawili mafupi, ombi la kwanza niunge mkono pia Wabunge wenzangu, *retention scheme* ile asilimia 30 ya makusanyo ya kodi ya ardhi, naomba ibaki kwenye Halmashauri isiende huko Hazina, kwa sababu ikienda kule hairudi haraka mnatuchelewesha sisi tunataka tupime viwanja, *squatter zinatusumbua*, ninaomba sana hilo Mheshimiwa Waziri wakati una *wind up* hebu liweke vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unalia hapa kwamba malengo hayakutimia kwenye kupima viwanja na wataalam umeshawasambaza kwenye Kanda, acheni tupime ardhii Wilayani huku kwenye Halmashauri mnazipeleka hizo pesa za nini huko, nilikuwa nataka kulisisitiza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tuna ombi Manyoni, tunao upungufu wa watumishi. Wataalam wa ardhii tulionao pale Halmashauri wanatakiwa wawe 21 lakini wapo wa wanne tu, watafanya kazi gani? *Squatter* hizi zitaendelea pamoja na hayo tunajitahidi kweli tangu mwaka juzi mpaka sasa ninavyozungumza tumepima viwanja karibu 991 ambavyo tayari tunavigawa kule, kwa shida kwa kujibana bana lakini viwanja 1,400 tumevipima viko kwenye hatua za mwisho tunakamilisha *cadastral survey* kwa ajili ya kupata *approve*.

Mkeshimiwa Mwenyekiti, 220 tumefanya *regulazation* tunaanda hati tupo kwenye hatua za mwisho, watumishi wanne hawa tunajitahidi. Kama haitoshi tumejibana fedha kwa shida, tume-order GPS RTK sisi watu wa Manyoni inakuja na tumeshailipia, tunaomba basi mtusaidie mtuunge mkono, hatuna gari kwa hawa watalaam wa ardhii, Mheshimiwa Lukuvi tusaidie gari kama juhudii zote hizi tumejitahidi si mtuunge mkono jamani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunayo Sheria Namba 8 ya Mipango Miji ya mwaka 2007, tangu mwaka huo imetungwa lakini haina *regulations* hazijatungwa, inatekelezwaje hii sheria bila *regulations*? Naomba m jitahidi hii sheria itungiwe *regulation* zake. Tunasema kwamba *planning* ndiyo inayoanza, sasa mnafanyaje kazi bila *regulations* tangu muda wote ule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni hili la ujumla, hebu tuitumie ardhii vizuri, ujezi wa *horizontal* ambaao wa mtawanyiko siyo mzuri tunamaliza ardhii hii, ardhii itaisha Dar es Salaam kama tunge-*opt vertical development* tungekuwa tumeishia Magomeni tu pale. Ile *population* ya Dar es Salaam siyo watu wengi, lakini kila mmoja anataka amiliki kiwanja

na eneo afuge mpaka kuku, siyo rahisi ardhi itaisha hii, tuende juu tusitawanyike tubakishe na maeneo ya kulima, tatalima wapi? Sasa kila mahali ni kujenga tu, haiwezekani lazima tu-plan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi *National Housing* wanavyojenga, kwa mfano nimeona ghorofa za Wanajeshi hapa Dodoma hapa, ziko vizuri, na *scheme* zingine za kujenga hebu waende ghorofa mbili tu juu watoe mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja, lakini *retention scheme*, ile fedha ibaki kwenye Halmashauri ili iwasaidie kupima viwanja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi nami kuchangia kwenye Wizara hii, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayofanya kuhalakisha kwamba wananchi wanapata makazi bora lakini pia kutatua migogoro ya ardhi nawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niseme mambo machache hassa kuhusu watumishi wa Idara ya Ardhi. Halmashauri nyingi hasa hizi Halmashauri za Wilaya, Halmashauri za vijiji hizi hazina watumishi wa kutosha wa idara hii ya ardhi, hasa Maafisa Ardhi wateule. Wilaya ya Njombe mpaka sasa hatuna Afisa Ardhi Mteule, tukitaka kusaini hati tunamtumia Afisa Ardhi Mteule wa Halmashauri ya Mji, kwa hiyo, mara nyingi tunapotaka kusaini hizi hati zimekuwa zikichelewa kwa sababu na yeye ana majukumu ya Halmashauri yake. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri ukishirikiana na TAMISEMI tuweze kupata Afisa Ardhi aweze kutusaidia kuweza kupata hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hati za viwanja zimekuwa zikichelewa na kwenye Halmashauri yangu tuna wananchi wengi ambao wana mashamba ya chai na wangependa wapate hati ambazo zingeweza kutumika kwa ajili ya kupata dhamana kwenye mikopo na sehemu mbalimbali, lakini zimekuwa zikichelewa kwa sababu tu hatuna Afisa Ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonyesha kwamba maeneo yote ambayo yana Maafisa Ardhi Wateule ndio maeneo ambayo migogoro inapungua sana, kwa hiyo, wanafanya kazi kubwa sana za kupunguza migogoro, lakini maeneo ambayo yanakuwa hayana Maafisa Ardhi Wateule migogoro inakuwa mingi. Kwa hiyo, tukiajiri Maafisa Ardhi Wateule wa kutosha katika Halmashauri zetu naamini migogoro mingi itapungua. Mfano ni pale Halmashauri ya Mji wa Njombe, tulikuwa na migogoro sana ya ardhi miaka ya nyuma, lakini sasa hivi imepungua na inaendelea kupunguza kwa sababu tuna Afisa Ardhi ambaye anafanya kazi vizuri sana. Tunaomba Halmashauri zetu zote ziwe na Maafisa Ardhi Wateule na maafisa wengine wawepo ili kasi ya upimaji wa ardhi na kasi ya utoaji wa hati iweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu mikopo ya nyumba. Nampongeza Waziri kwamba kuna mpango wa kuanza kukopeshaa nyumba kwa wenyewe vipato vidogovidogo, mpango huu umejkita sana kwenye maeneo ya mijini, tuende vijijini ambako kuna wakulima wadogo wadogo na vijana ambao wanafanya kazi za bodaboda na shughuli ndogondogo waweze nao kumiliki nyumba. Tufuate utaratibu ule wa VIGUTA ambao wanajenga nyumba za bei rahisi sana. Wanajenga nyumba mpaka za shilingi milioni 15, shilingi milioni 25 lakini wanajenga nyumba za ghorofa moja mpaka za milioni 60 na wamejenga maeneo ya Kibaha pia sasa hivi wanajenga maeneo ya Dodoma.

Kwa hiyo, twende vijijini hawa wakulima wetu wadogo wanahitaji nyumba, naamini kwamba kuititia shughuli zao za kilimo, kuititia shughuli zao za bodaboda na

ujasiriamali mdogomdogo wakiwekewa utaratibu mzuri wanaweza wakamiliki hizi nyumba, wanaweza wakajenga nyumba na wakarudisha hizo fedha kuititia hizo shughuli zao za kila siku kwa maana ya bodaboda au ujasiriamali na kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia juu ya bei viwanja. Bei ya viwanja bado iko juu kwenye baadhi ya maeneo. Kuna maeneo hasa viwanja vile ambavyo vinapimwa na makampuni au mashirika mbalimbali kwa kushirikiana na Halmashauri, viwanja hivi vinauzwa bei ya aghali sana. Kwa mfano, utakuta kiwanja kinauzwa shilingi milioni 10, shilingi milioni 20 eti kwa sababu tu barabara imetengenezwa au maji yamepelekwa. Ukiangalia utakuta kwamba wananchi wa kipato cha chini ambao wana uwezo mdogo wa kupata hizi fedha hawawezi kumiliki hivi viwanja kwa sababu ni vya bei ya juu sana. Tuweke utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba tunathibiti bei za hivi viwanja, tukiacha hivi makampuni haya kama hali iliyopo utakuta kwamba wananchi wa chini watashindwa kumiliki viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wanaoweza kununua hivi viwanja shilingi milioni 10, shilingi milioni 20 ni wale watu wenye uwezo tu, ni wale watu wenye kipato cha juu. Utakuta hawa wananchi wenye kipato cha chini wanazidi kwenda pembezoni, wanaondoka katika maeneo yale kwa sababu hawana uwezo wa kumiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hongoli, Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Ruth Mollel na Mheshimiwa Susanne Maselle waijandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii. Awali niipongeze sana Wizara hii kwa jitihada za kazi wanazozifanya ndani ya Wizara hii. Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake pamoja na wasaidizi wake wamefanya kazi nzuri

sana. Tunawapongeza hasa kwa kutatua migogoro mingi ambayo kimsingi ilikuwa inawagusa sana wananchi. Tunawapongeza na kuomba tuwaombee heri sana waendelee kutenda haki na misingi iliyowekwa ya kisheria juu ya kuwasaidia wananchi hasa walalahoi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia tatizo la migogoro ya ardhi ya vijiji vya Kabage, Sibwesa, Mkungwi, Kagunga na Kapanga vilivyoko kwenye Wilaya ya Mpanda. Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ina mgogoro wa muda mrefu sana wa vijiji hivi, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri apange ziara aje amalize tatizo hili, akishirkiana na Wizara ya Maliasili. Wananchi wengi wanataabika hawana ardhi ya kufanya kazi wakati ni vijiji halali ambavyo kimsingi kama vitasimamiwa tatizo hili tutakuwa tumelipunguza na kuwafanya wananchi waendelee kufanya shughuli zao. Naomba sana Waziri husika aje atatue matatizo ya Mkoa wa Katavi hasa Wilaya hii ya Tanganyika iliyoko kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni tatizo la kupata hati za kimila kwenye Wilaya ya Tanganyika. Karibu maeneo yote ya vijijini tuna tatizo kubwa sana la kukosa huduma ya kupata hati za kimila. Kuwasaidia wananchi hawa wanapopata hati za kimila tunawajengea uwezo wa kiuchumi, kwani watapima mashamba yao na watakuwa na nafasi ya kutumia dhamana ya hati miliki ili waweze kwenda kwenye taasisi za fedha, huduma hiyo kwetu sisi hatuna. Naomba Waziri aone kwamba ni wakati muafaka sasa kupeleka huduma hii kwenye maeneo yote ya nchi yetu hasa maeneo ya pembezoni kwenye Wilaya hasa zile ambazo ni changa. Tunahitaji huduma hii ili iweze kutatua matatizo yanayoikabili Wilaya kwa kukosa huduma ya hati miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni uhaba wa wafanyakazi. Wataalam wa ardhi hasa Wilaya mpya, naamini na nchi nzima bado kuna tatizo kubwa sana. Tunaomba Mheshimiwa Waziri anapokuja aje na majibu sahihi yatakayosaidia kutoa

suluhisho hasa wataalam hawa ambao kimsingi wanahitajika ili waweze kufanya kazi ambazo zitawasaidia wananchi na kutatua migogoro mingi ambayo iko kwenye Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunahitaji kupata vitendea kazi, wataalam ambao wapo hata huko kwenye Wilaya hawana vitendea kazi vya shughuli ya upimaji ambavyo ni pamoja na magari. Unakuta Halmashauri haina gari, haina vifaa ambavyo vinahitaji kwa shughuli za kupima hivyo viwanja, matokeo yake wanaenda kwa miguu kitu ambacho hawawezi kutekeleza na kwenda na kasi ambayo ipo. Tunaomba sana hasa kwenye Wilaya yangu tupate wale ambaao wana uwezo wa kufanya hiyo kazi ili tuwasaidie Watanzania. Kimsingi tukitekeleza hili tutakuwa tumetoa kero kubwa ambayo inawakabili wananchi kwa kukosa huduma. Tukipata hao watalaaam nina imani kwamba eneo zima la suala la ardhi na migogoro ambayo tunaizungumzia itapungua kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucia Mlowe.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kuwapongeza Waziri na Naibu wake pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Pamoja na kazi hii nzuri mnayoifanya naomba nielezee matatizo yaliyoko hasa katika Mkoa wangu wa Njombe nikianza na migogoro ya wananchi na watu wa *TANAPA*. Kwa mfano, nikiangalia maeneo ya Wanging'ombe, Kijiji cha Ruduga kuna tatizo la wananchi na watu wa *TANAPA*, mara kadhaa wamekuwa wakiwasumbua sana na kuna kipindi waliwakatia mazao yao.

Kwa hiyo, nimuombe Waziri kufika maeneo yale kutusaidia kutatua tatizo hili kwa sababu limekuwa ni tatizo la muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa sasa wametishiwa kwamba watatakiwa kuhama kwenye kile Kijiji cha Mpanga. Sasa wanakaa kwa wasiwasi wana hofu kubwa kwamba watahama na wana shida kwa sababu ya hofu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la migogoro katika Wilaya ya Makete. Katika Wilaya ya Makete kumekuwa na migogoro kati ya Hifadhi ya Kitulo na wananchi wa kijiji cha Misiwa. Watu wa hifadhi wameweka *beacons* kwenye mashamba ya wananchi wa maeneo yale ya Kitulo, wanasema kwamba wanapanua hifadhi. Hivyo, nimuombe Waziri kutusaidia suala hili angalau hawa wananchi kuwaondoa hofu maana yake nao sasa hivi wanashindwa kufanya uzalishaji kwa sababu wanaona wanaendelea kuingiliwa, mwisho wa siku hata mashamba yote yatachukuliwa, ninawaomba sana mtusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niongelee suala la migogoro Makete na Wanging'ombe. Kuna tatizo la mipaka kati ya Wanging'ombe na Makete, vilevile kuna tatizo kati ya shamba la Ludodolelo, kuna mwekezaji ambaye yuko katika shamba la Ludodolelo ambaye anawasumbua sana wananchi, sasa wanavutana kati ya wananchi na yule mwekezaji. Kwa hiyo, niwaombe Serikali mtusaidie mfike maeneo yale kusudi tuweze kutatua tatizo hili. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Susanne Maselle na baadaye Mheshimiwa Mchengerwa ajiandae.

**MHE. SUSANNE P. MASELLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii. Kabla sijaanza kuchangia napenda kutoa pole kwa wananchi wa Mwanza kwa tetemeko ambalo

limetokea jana na pia nitoe pole nydingi kwa askari wetu Joyce ambaye alifariki kwa kupata mshituko na majeruhi wengine ambao wamepelekwa hospitali, natoa pole sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ulikuja Mwanza najua ulifanya mambo mazuri sana kama alivyoongea Mbunge wa Nyamagana, lakini kuna migogoro ambayo hukupitia, kuna migogoro ambayo iko llemela. mwaka 2009 Jeshi la Wananchi ilifanya utambuzi wa maeneo yake na iligundulika eneo la Mlima wa Nyagungulu Kata ya llemela ilikuwa inafaa kwa makazi ya Jeshi. Sasa utambuzi huu baada ya kufanyika ilionekana kuna kaya 448 ambazo zilikuwa na makazi ya kudumu na tarehe 04 Novemba, 2014 ilifanya tathmini ambapo Serikali ya Mkoa pamoja na Jeshi la Wananchi waliona kwamba wananchi hao wanapaswa kulipwa, na waliamuwa kwamba baada ya tathmini hiyo walisema kwamba ndani ya miezi sita wananchi hao wangkuwa wameshalipwa, lakini mpaka sasa bado hawajalipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nyumba zingine ambazo ni za udogo mpaka zimeanza kuanguka hawawezi kufanya marekebisho yoyote au kuzikarabati kwa sababu wanaogopa eneo hilo linachukuliwa na Jeshi. Sasa Mheshimiwa Waziri ninaomba umalize huu mgogoro kwa sababu hawa wananchi wanateseka na wananchi wengi wamekuwa wakilalamika, wameandika barua nydingi sana. Wameandika barua kwa Mkuu wa Mkoa, barua hizi hapa nitakuletea, wameandika kwa Mbunge...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Susanne, tunaendelea na Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Pia nimshukuru sana

mzalendo namba moja nchini ambaye ni Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kufanya kazi nzuri sana siku tatu zilizopita za kusimamia rasilimali za nchi yetu hii Tanzania. Niliwahi kusema hapa kwamba, Dkt. John Pombe Magufuli ni mzalendo namba moja, na uzalendo wake tunauona hapa kwa namna ambavyo anawatetea watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri wote wa Wizara hii, kwanza kwa Mheshimiwa Lukuvi, Naibu wake pamoja na Wasaidizi wao wote, kwa kweli Wizara hii ni ngumu lakini Mheshimiwa Lukuvi amefanya kazi nzuri sana kwa kipindi kifupi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia umaskini uliopo katika Jimbo langu la Rufiji. Jimbo la Rufiji lina *square kilometer* 13,600 na eneo la Bonde la Mto Rufiji ambalo linafaa kwa ajili ya kilimo ni zaidi ya hekta 500,000. Kutokana na utapeli wa madalali na kutokana na wawekezaji matapeli ambao wameingia Rufiji, leo hii ukifika *TIC* hauwezi kupata eneo la uwekezaji Rufiji. Nimuombe Mheshimiwa Waziri kuliangalia hili na kuangalia uwezekano wa kunyanganya maeneo yote ambayo wawekezaji matapeli wamechukua ardhi yetu ya Rufiji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini tulionao ni kwa sababu matapeli hawa wamehodhi maeneo haya na hawayafanyii shughuli yooyote. Leo hii Rufiji tusingekuwa maskini kwa sababu ardhi ndio utajiri wa hali ya juu. Nikuombe Mheshimiwa Waziri sasa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, Serikali yetu ya Awamu ya Tano iweze kupambana na matapeli hawa. Yako maeneo yaliyochukuliwa na watu wa *RUBADA*, pia yako maeneo yaliyochukuliwa na watu wanaojifanya ni wawekezaji lakini siyo wawekezaji wa kweli. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri maeneo hayo uyarudishe ili sasa wale wawekezaji wanavyopita *TIC* waweze kuelekezwa na kufika Rufiji wapatiwe maeneo ya uwekezaji. Kwa sababu, maeneo tuliyonayo ni ya kutosha, ardhi ipo tupu, wananchi wanashindwa kushiriki kwenye shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namwomba Mheshimiwa Waziri, kama sio yeye au Waziri anayehusika, atakapofika hapa atupe taarifa ni kwa nini mwaka 2006 Serikali iliamua kuhamisha mifugo kutoka Bonde la Ihefu na kuleta mifugo katika Bonde la Mto Rufiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tufahamu sababu ya kuhamisha mifugo Bonde la Ihefu. Tunafahamu kabisa kwamba uhamishwaji wa mifugo kutoka Bonde la Ihefu kupelekwa maeneo mbalimbali ya nchi ultokana na uharibifu mkubwa wa Bonde la Ihefu. Sasa nataka nifahamu, je, Serikali ilidhamiria kuleta mifugo katika Bonde la Rufiji ili sasa na bonde hili liweze kuharibika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu hayo Mheshimiwa Waziri; kama sio yeye au Waziri ye yeyote anayehusika atakapofika hapa atupatia majibu haya, ili Warufiji wawewe kufahamu kiini cha matatizo haya, kwa sababu wakulima leo hii wanashindwa kushiriki katika shughuli za kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba Warufiji walikuwa na ndoto za kupatiwa kiwanda katika eneo la Muhoro pamoja na Chumbi. Mheshimiwa Waziri atakapofika hapa, naomba atuambie, je, ardhi ile ambayo ilitengwa kwa ajili ya mwekezaji, bado ipo? Je, mwekezaji huyu anaifanya utaratibu gani ili sasa tuweze kupata majibu ya jambo hili? (*Makofi*)

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba...

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchengerwa naomba ukae. Kuhusu Utaratibu.

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nipate Mwongozo Kuhusu Utaratibu, hasa kuhusu Kanuni ya 149(3)(b) ya Uvaaji Ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge anayechangia hajavaa mavazi ya Kibunge. Mavazi ya Kibunge kama unavaa hiyo baraghashia ya Kiislam, lazima uvae na kanzu. Yeye amevaa hiyo na suti. Ni kinyume kabisa na kanuni. (*Kicheko/Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea huo utaratibu. Ni kwamba kofia hiyo, inaweza kuvaliwa na nguo yoyote kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, naomba umalizie dakika zako. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msemaji alini-*miss tu*. (*Kicheko*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchengerwa, naomba umalizie ukavae kanzu. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 3 Machi, 2017, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alifika Rufiji na katika maeneo aliyofika, alifika Ikwiriri na katika kauli alizowahi kuzitoa Mheshimiwa Rais aliwaambia Watanzania wa Rufiji, hususan Wenyeviti wa Vijiji kutouza maeneo yao. Aliwaambia wawe makini sana na madalali na matapeli wanaotaka kuchukua ardhi yetu pale Rufiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 9 Septemba, 2016 Waziri Mkuu pia alifika Rufiji, lakini pia katika maeneo ambayo yana mgogoro mkubwa wa ardhi ni eneo letu la Kata ya Chumbi. Tarehe 4 Mei, 2017 Waziri wa Ardhi aliniandikia barua ya kutatua mgogoro wa ardhi pale Chumbi. Kwa bahati

mbaya, Mheshimiwa Waziri hakuweza kufika Chumbi, lakini wananchi wa Kata ya Chumbi wanaamini labda mimi ndio nimemzuia Mheshimiwa Waziri kufika Kata ya Chumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama hapa, atoe majibu, ni kwa nini hakufika katika Kata ya Chumbi ambako kuna mgogoro mkubwa wa ardhi? Miongoni mwa malalamiko ya wananchi ni kwamba, Mwenyekiti wa Kijiji ameuza ardhi ambayo ina ukubwa wa takriban zaidi ya ekari 2,400 kwa Sh. 9,700/= kwa ekari moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Mheshimiwa Rais alishatoa tamko la Wenyevitii wa Vijiji kutouza maeneo yao, naomba Mheshimiwa Waziri akifanya majumuisho, basi atupe majibu ya jambo hili. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunamalizia uchangiaji wetu kwa Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu nilikuwa na mgogoro wa Kazimzumbwi kwa kweli yeye na Mheshimiwa Waziri Mkuu waliingilia kati. Nawashukuru sana Waheshimiwa hawa, kwani walifunga safari kutoka hapa mpaka Ukonga na wakahakikisha kwamba jambo hilo linajadiliwa kwa manufaa ya watu wa Ukonga. Kwa hiyo, nawashukuru sana, nawatachia kazi njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Waheshimiwa Mawaziri wapo humu. Hizi pongezi ambazo Mheshimiwa Lukuvi anapewa na wengine, nadhani Mawaziri wangefanya kazi kama hiyo tungkuwa hatuna mgogoro mkubwa. Kwa hiyo, ni muhimu wakajifunza mambo mazuri kama haya. Anapokea simu na Naibu wake, wanakusikiliza, wanakupa majibu, wanatembelea Majimbo; na kama jambo haliwezekani, anakwambia hili kwa mujibu wa sheria haliwezekani. Mheshimiwa Lukuvi nafikiri kwa sababu ya uzoefu wake, anaweza akatoa *tuition* kwa wenzake ili tukaenda vizuri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Mheshimiwa Lukuvi naomba anisaidie kumaliza migogoro maeneo yafuatayo Ukonga. Moja, kuna mgogoro wa UVIKIUTA, nyumba zimevunjwa zaidi ya mara tatu, anaufahamu vizuri. Tunahitaji watu wale wapate amani, wapate maelekezo ya kisheria waishi kwa amani katika eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgogoro upo pale Pugu Kajiungeni. Ni eneo la wazi, hakuna eneo lingine, vijana walikuwa wanacheza mpira, akinamama wanafanya kazi zao; nyumba zilivunjwa usiku wa saa 9.00. Ofisi ya Mkoa tumeenda mara nydingi sana, lakini hatuna majibu mpaka leo. Kwa hiyo, tunaomba atusaidie tupate majibu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kipunguni haina Shule ya Sekondari, haina huduma za kijamii, ni kata mpya. Eneo pekee ambalo lilikuwa limebaki, limevamiwa na watu, hawana *documents* zozote zile, lakini majibu hayapatikani mpaka sasa. Kwa hiyo, tunaomba atusaidie pia, kupata majibu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro mwingine mkubwa wa ardhi ni wananchi ambao walihamishwa kutoka eneo la Uwanja wa Ndege wakapelekwa maeneo ya Buyuni, Zavala na maeneo mengine kule. Wale watu

wameondolewa kutoka hapa Uwanja wa Ndege Kipawa, kule hawakupewa ardhi, lakini bahati mbaya pia wakapewa maeneo ya watu. Kwa hiyo, kuna ugomvi kati ya watu ambao wametoka Kipawa na wale ambao ni wenyeji waliokutwa katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lukuvi kwa sababu yupo tayari, akutane na watu hao awasikilize, kwani ni kilio cha muda mrefu na kweli wana shida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni bomoa bomoa. Eneo la Kata ya *Pugu Station*, Kata ya Ukonga na Kata ya Gongo la Mboto, maeneo yaliyobomolewa kupisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha *standard gauge*; hatupingi, lakini wale watu wengine walikuwa na hati, wamechanganywa kule kule na hakuna fidia yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mambo kama haya wakiyafanya ni muhimu watu wafahamu sheria zinasema nini? Haki zao ni zipi? Wakati mwingine kutoa taarifa *in advance* ili kama kuna mtu ana-vacate, aweze ku-vacate ili asipoteze mali zake zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno la mwisho ni upimaji wa maeneo ya umma. Migogoro mingi iliyopo katika maeneo yetu hayapimwi...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa  
muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Lukuvi, achukue hatua mahususi kupima maeneo haya ili kuondoa migogoro kati ya wananchi na maeneo ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umeshafahamika. Ahsante sana. Tunamalizia na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii adimu sana. Naungana na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siri kubwa ya mafanikio ya Wizara hii, wanasiliza tatizo, wanakwenda *site*, wanalishughulikia na wanaweka mifumo ya kuhakikisha kwamba tatizo halijirudii. Hongera sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri *spirit* aliyotumia ya kuweza kutatua migogoro maeneo mbalimbali, aje Kaliua akishirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii atatue migogoro ambayo inawasumbua wananchi wa Kaliua kwa muda mrefu na kuondokana na mateso na maumivu wanayopata wananchi wa Kaliua kwa sababu ya migogoro ya ardhi ya kati ya wananchi na hifadhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la upimaji wa ardhi. *Speed* ya kupima ardhi bado ni ndogo, asilimia 25 ni ndogo sana. Tunatamani kwamba mwananchi anapohitaji ardhi aweze kupewa kiwanja ambacho tayari kimepimwa. Kwa hiyo, naomba sana kwenye Mfuko wa Kupima Ardhi lazima kuhakikisha kwamba kuna fedha ya kutosha. Iwepo fedha ya kutosha na vifaa vyaa kupima ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ardhi imeweka kipengele kwamba Waziri atatenga eneo la mifugo; eneo litapimwa, litakuwa *gazetted* na pia litalindwa. Kwa hiyo, naomba wakati wa kupima ardhi kwenye maeneo mbalimbali, Mheshimiwa Waziri ahakikishe anatenga maeneo ya mifugo na pia maeneo yawe *gazettedna* yawezee kulindwa. Ndiyo inayosababisha migogoro mikubwa sana ndani ya nchi yetu kutokana na migogoro ya ardhi kwa wakulima na wafugaji na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba ahadi ya *National Housing*; pamoa na kazi nzuri wanayoifanya, wafike Kaliua. Ni Wilaya ambayo ni mpya, lakini inakwenda *speed*

sana kwa maendeleo, waje wawekeze ndani ya Wilaya ya Kaliua, kujenga nyumba nzuri nasi tuweze kuwa wa kisasa kama ambavyo Wilaya nyingine wameweza kujengewa nyumba na *National Housing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hawa watu wa Mfuko wa Kujenga Nyumba za Watumishi (*Utumishi Housing*), usambae uende maeneo mengi, ufile mpaka Kaliua. Watumishi wetu hawana nyumba, wamepanga nyumba ndogo ndogo za vijiji huko. Tunaomba na wenyewe waje Kaliua wapanuke katika maeneo mengi; sasa hivi wame-concentrate kwenye maeneo machache sana. Mfuko uongezwe ili watumishi wetu wa maeneo mengi wawewe kupata nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine. Migogoro mikubwa ya ardhi inasababishwa na uelewa mdogo pia wa Wenyeviti wa Vijiji na Watendaji wa Vijiji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Naomba umalizie sentensi yako ya mwisho.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri atoe elimu kwa Viongozi wa Vijiji. Viongozi wa Vijiji wanatoa maeneo makubwa sana. Sheria inaruhusu ukomo wa kutoa eneo la kijiji, lakini wanatoa mpaka hekta 1,000 au 2,000 na wanapokea rushwa, wanaleta watu bila hata wananchi kujua. Kwa hiyo, naomba itumike busara viongozi wapewe semina na mafunzo waweze kutumia Sheria ya Ardhi kugawa maeneo ndani ya vijiji vyao ili kuondokana na migogoro inayosababishwa na kugawa ardhi bila kufuata Sheria ya Ardhi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa William Lukvi pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Angeline Mabula, sambamba na timu nzima ya Wizara chini ya Jemadari Kayandabila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe malalamiko yangu kuhusu hatua ambazo zinachukuliwa na Idara ya Ardhi Kanda ya Kaskazini; tunalo shamba letu la Mnazi *Sisal Estate* ambalo kwa sasa linamilikiwa na mwekezaji wa Kenya kuitia kampuni ya *Le-Marsh Enterprises* ambayo inamiliiki mashamba matatu yenye hati zifuatazo; *tittle No.44144*, ekari 562; *tittle No. 17146*, ekari 1188, pamoja na *tittle No. 11247*, ekari 2442.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Lushoto ilitoa barua ya *Notice of Revocation* yenye Kumb. Na. *LDC/L.10/VOL.111/245-09/12/2016* kwenda kwa Kamishna wa Ardhi Kanda ya Kaskazini. Naomba nitoe masikitiko yangu kuwa barua hii inakaribia kumaliza mwaka lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikichukua hatua za ufuatillaji mara kwa mara kwenye Ofisi ya Kanda, lakini mara zote nilikuwa napata ushirikiano hafifu, ikiwemo mara ya mwisho, Mheshimiwa Waziri tulivyofanya mazungumzo, walitujibu kuwa kuna matatizo ya kiufundi kwenye taarifa ya notisi. Hili kwetu tunalionna kama ni hujuma kwa kuwa barua za Kiserikali hujibiwa kwa taratibu zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyo wawekezaji wote wababaishaji huyu *Le Marsh Enterprises* ni miongoni mwao na amekuwa akiwahadaa wananchi, Halmashauri na sasa anaonekana na baadhi ya Maafisa wa Ardhi Kanda, wanamlinda hivyo kusababisha chuki kubwa kwa wananchi husika wa Kata za Mbaramo, Mnazi, Lunguza ambao wanazungukwa na mashamba hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna nia ya kumuonea mtu lakini tunahitaji kuona wananchi wanafaidika na rasilimali zao na pia kuona mapato ya Halmashauri yanapatikana bila kikwazo chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; mwekezaji katika Mashamba ya Katani ya Mnazi ameshindwa kwa kiasi kikubwa kuyaendeleza mashamba anayoyamiliki. Kati ya ekari 4192 ni ekari 500 tu ndizo ambazo ameziendeleza kwa kupanda mkonge na kuvuna, ekari 1942 mkonge upo porini, kwenye vichaka hautunzwi kabisa. Ekari 1023 ni msitu mtupu ambaao unatumwa na wafugaji wa jamii ya kimasai kama malisho ya mifugo yao. Pia mmiliki huyo hajalipia kodi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ya bajeti. Nianze na mgogoro wa shamba la Tumaini lenye ukubwa wa ekari 4,000 ambalo Mheshimiwa Waziri, kwa uzalendo wa hali ya juu wa kuthubutu alifuta hati miliki ya shamba lile. Hicho ni kitendo cha Kijasiri kabisa na chenye kuendana na utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuwa suala hili lipo mahakamani, lakini wananchi wa Mafia wanaunga mkono uamuza wa Mheshimiwa Waziri wa kuifuta hati na kulirejesha shamba miliki kwa wananchi. Ombi letu ni mara baada ya shauri lililopo Mahakamani kumalizika tunaombwa mgao wa shamba hili ufanywe na Halmashauri yetu ya Mafia kulingana na vipaumbele vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumwomba Mheshimiwa Waziri alifute shamba la ng'ombe ambalo limebaki pori kubwa na ongezeko la watu limepelekea ongezeko kubwa la mahitaji ya ardhi kisiwani Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*); Halmashauri ya Mafia tumetenga eneo kubwa la kutosha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kupitia Shirika hili. Nimwombe sasa Mheshimiwa Waziri, aagize uongozi wa Shirika hili kuanza mradi huu haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ni kitu muhimu sana katika nchi yetu na dunia nzima kwani kila kiumbe kinachoishi duniani kiko chini ya ardhi ambapo kumekuwa na changamoto nyingi ambazo zinaikabili Wizara hii ambayo ni lazima kuwepo na mikakati ya makusudi kumaliza changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wakulima na wafugaji; suala hili limekuwa ni changamoto kubwa kwa nchi yetu ambayo imesababisha madhara makubwa sana ikiwemo vifo kwa wakulima na wafugaji na pia kwa wawekezaji hasa kama hakukuwa na ushirikishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mipaka, ni vyema Wizara ikawa na utaratibu madhubuti wa kupitia upya mipaka ya maeneo mbalimbali ikiwemo vijiji na vitongoji lakini maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji pamoja na maliasili zote ili kuondoa migogoro mbalimbali inayoweza kujitokeza katika maeneo yetu. Upatikanaji wa hati miliki, suala hili limekuwa na changamoto kubwa hasa kwa wananchi wa vijiji ambao makazi yao hayajapimwa, na kumekuwa na urasimu mkubwa kwa maafisa wa ardhi katika Halmashauri mbalimbali nchini ikiwemo Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Maafisa Ardhi kwenye Halmashauri ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga; nashauri Serikali kuongeza Maafisa Ardhi kwenye Halmashauri mbalimbali nchini ili kuondoa migogoro isiyu ya lazima. Kutolewa mafunzo kwa Maafisa Ardhi na Maafisa Mipango Miji ili kuweka ufanisi katika maeneo na kazi zao ambao hazitaleta usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upimaji wa ardhi, suala hili limekuwa na changamoto kubwa, lakini linatokana pia na maafisa ambao sio waaminifu kwa kujipatia viwanja ambavyo Halmashauri na Serikali kwa ujumla hazinufaiki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa hati kuchukua muda mrefu na kupelekea mianya ya rushwa suala hili limekuwa likiwakatisha tamaa wananchi ambao hawana hati miliki. Nashauri Serikali kufuatilia suala hili kwa ukaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba; kuna changamoto kubwa hasa kwa suala la gharama kwani gharama za nyumba zinazojengwa ni kubwa ambazo wananchi wakiwemo wa Mkoa wa Rukwa hawawezi kumudu kabisa nyumba zijengwe kulingana na jiografia husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji wapewe ramani ili wayajue maeneo yao. Hii kwa kiasi kikubwa itachangia kuondoa migogoro isiyo na sababu.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Wizara na Mheshimiwa Waziri kwa juhudni wanazofanya katika kuyapatia ufumbuzi masuala ya migogoro ya ardhi nchini ikiwemo Monduli. Mheshimiwa Waziri anakumbuka mwaka jana 2016 Machi alipokuja Monduli alikabidhiwa mashamba 13 yaliyofutwa na Rais kwa ajili ya wananchi lakini mpaka sasa wananchi wamezuiwa kutumia ardhi pamoja na kwamba wao wameshapanga matumizi na kubainisha maeneo ya malisho na eneo la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko wamiliki wa awali waliyapeleka malalamiko kwa *DC* na *DC* kuzuia wananchi kutumia ardhi hiyo, mpaka itakapoenda tume ya kuchunguza kama mchakato wa kufutwa ulifuatwa. Masikitiko yetu ni kwamba Rais ameshafuta mashamba je, kuna mtu mwingine mwenye mamlaka zaidi ya Rais? Naomba kauli ya Mheshimiwa Waziri kuhusu mashamba

ambayo Rais ameshayafuta lakini bado wananchi wananyimwa kuyatumia. Naomba Ofisi yake itoe waraka wa kuelekeza namna bora ambayo wananchi wanaruhusiwa kutumia ardhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Mheshimiwa Waziri alitoa agizo kuhusu Ndugu Olemilya Mollel aliyejichukulia ardhi kinyume na taratibu ambapo pia aliagiza ye ye kuondoa walini wa jeshi wenyewe silaha wanaolinda ardhi yake ambayo ni pori tu, miti na majani, (agizo lake halikutekelezwa) badala yake wananchi sasa wanakamatwa na kutozwa hadi milioni moja kama faini na mwenye shamba (naomba kauli yake ili kunusuru wananchi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa Baraza la Ardhi Wilaya ambapo sisi tumetoa jengo tayari. Tunaomba kupatiwa Afisa Ardhi Mteule. Tunaomba wananchi wapewe angalau miaka mitano ya kulipia nyumba za NHC.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Ardhi katika maisha ya mwanadamu ndiyo rasilimali msingi katika maendeleo ya mwanadamu kwa vile miundomisingi yote hufanyika juu ya uso wa nchi. Uso wa asili, maji, barabara, Maziwa, reli, makazi na shughuli za kilimo, wanyama wa kufugwa pamoja na pori la akiba na hifadhi zote ziko juu ya uso wa nchi na kwa ajili hiyo basi ni vema Serikali kupitia Wizara hii ikajipanga kikamilifu kupata mipango miji iliyosanifiwa kikamilifu na kuendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Ardhi nchini ikiwemo kubwa kabisa uhaba wa wataalam pamoja na vitendea kazi hali inayopelekea kutokuwepo kwa matumizi bora na endelevu ya ardhi mjini na vijijini. Ongezeko la watu pamoja na mifugo ni changamoto nyingine kubwa inayopelekea mwingiliano wa shughuli za kibinadamu kwa maana ya wakulima na wafugaji pamoja na changamoto ya ucheleweshwaji wa malipo ya fidia kwa wananchi ambao ardhi yao inatwaliwa kwa ajili ya shughuli za uwekezaji. Katika sekta mbalimbali

ikiwemo kilimo, viwanda maeneo ya kimkakati kama vile, *special economic zone* na kadhalika. Uharibifu wa mazingira vile vile hufanyika juu ya uso wa nchi. Hivyo basi, ipo haja kwa Wizara hii kuwezesha kiutendaji kwa kuongezewa bajeti yake ili iweze kuajiri wataalam wengi zaidi pamoja na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yetu ya Mbogwe tunayo nafasi nzuri sana ya kuweza kujipanga vizuri katika Sekta hii ya Ardhi kwa vile wilaya yetu ni mpya kabisa hata ujenzi holela haujawa wa kiwango cha juu. Tunachohitaji Wilaya na Halmashauri ya Mbogwe ni kuunga mkono katika jitihada za kuipima ardhi yetu. Hivyo basi, tunaiomba Wizara ituangalie wananchi wa Mbogwe kutupatia Afisa Mipango Miji ili asaidie katika kupanga kitaalam wilaya yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jitihada za kupata maendeleo katika shughuli za upimaji Wilayani Mbogwe Mfuko wa Jimbo umechangia ununuzi wa kifaa cha upimaji kiitwacho *Total Station*, kinachotakiwa kingine kiitwacho *differential* ili tuweze kukamilisha uchapishaji wa upimaji wa ardhi hasa viwanja na mashamba ya wananchi na hatimaye waweze kumilikishwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalipongeza kwa dhati Shirika la Nyumba NHC kwa kazi nzuri sana linazozifanya. Naishauri Serikali kuliwezesha Shirika hili ili liweze kujenga nyumba nyingi zaidi nchini ikiwepo Wilayani Mbogwe. Naunga mkono juhudhi na jitihada zinazoendelea kufanywa na Wizara hii. Ombi, letu Mbogwe ni kupewa Afisa Mipango Miji katika Halmashauri ya Wilaya Mbogwe pale Wizara itakapoanza kuajiri watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara, kwa kazi nzuri mnayoifanya kutatua migogoro ya ardhi katika nchi yetu. Naiomba Serikali, kuendelea na juhudhi ya kutatua migogoro ya ardhi katika Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji. Kuna migogoro ya kugombania

mipaka kati ya wilaya na wilaya nyingine, mipaka ya kata na kata, kuna migogoro ya kijiji na kijiji. Ili kumaliza kabisa migogoro hii naishauri Serikali kupima ardhi yote ili kupata matumizi bora ya ardhi nchini. Kuna tatizo la ujenzi holela katika miji yetu naishauri Serikali, kusimamia upangaji wa miji yetu, kuwa na *master plan* ya miji na kuwaelimisha watu kufuata sheria ya mipango miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwapimie mashamba wakulima ili kila mkulima kuwa na shamba ambalo limepimwa na analipia. Katika upimaji naiomba Serikali iwapimie wananchi kwa bei nafuu ili hata watu wenye vipato vidogo, waweze kusajili mashamba yao na kupimiwa. Serikali ipunguze bei ya upimaji wa viwanja, wananchi wanashindwa kununua viwanja vya Serikali sababu bei ipo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Uongozi mzima wa Wizara. Ni jambo lisilo na shaka hata kidogo Wizara hii ni mionganoni mwa Wizara chache sana zinazochapa kazi hasa chini ya uongozi wa Mheshimiwa William Lukuvi, pamoja na Naibu Waziri, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie hotuba hii katika maeneo yafuatayo:-

Migogoro ya Ardhi, kila kona ya nchi utasikia migogoro hii. Nipongeze tena jitihada zinazofanywa na Wizara katika kutatua migogoro mfano ni upimaji wa maeneo ya wafugaji na wakulima katika Mkoa wa Morogoro. Bila shaka mfano huu utakwenda maeneo yote nchini mfano katika Jimbo langu la Kilindi lenye nusu wakulima na nusu wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mfumo huu pia uelekezwe huku kwa sababu migogoro inaongezeka kila siku. Suluhu ni kupima tu. Wizara imeelekeza Halmashauri zitenge fedha kwa ajili ya kupima, lakini ni ukweli usiofichika bado Halmashauri zetu hazina uwezo wa kupima kwani baadhi

ya Wilaya zina maeneo makubwa sana mfano wilaya yangu ina vijiji 102, vitongoji 650, hivi itachukua miaka mingapi kupima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Migogoro ya Ardhi, (mpaka kati ya Kilindi na Kiteto). Mimi binafsi nichukue fursa hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu; Waziri wa Ardhi; na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ambao walifika mpakani na kujiona mgogoro uliodumu zaidi ya miaka 30 ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza Wizara kuitia wapimaji kuitia *GN* 65 ya mwaka 1961 inayotenganisha Mkoa wa Tanga na Arusha kwa sasa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zake wapimaji walifika na kufanya kazi kubwa ya kubainisha mpaka huu, gharama za fedha za umma zimetumika kwa watumishi hawa lakini cha kusiklitisha ni kuona zoezi hili limesimama alama (*Beacons*) hazijawekwa, wananchi wanataka wapate majibu ya Wizara hii, tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekwishatambua wapi mpaka wao upo kwa mujibu wa taarifa ya wapimaji ambapo, mimi, Mkuu wa Wilaya na Mkoa wa Tanga tunazo, nadhani zoezi hili ni vema lingekamilishwa ili wananchi wa wilaya hizi mbili, (Kiteto na Kilindi) ambao wanaishi kwa hali ya wasiwasi na kutofanya shughuli za kilimo na mifugo wanachoomba kupata suluhu ya kudumu ambayo ni kuweka alama za kudumu (*Beacons*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Wizara juu ya jambo hili ambalo linabeba mustakabali wa maisha ya wananchi wa Kilindi na Kiteto, kutowaona wapimaji kumalizia zoezi hili kunatoa picha isyoleta matumaini. Wananchi wana imani kubwa na Mheshimiwa Waziri kwani utendaji wake bila shaka umemletea sifa kila kona ya nchi hii, ni imani yangu hatapata kigugumizi katika hili ili kuleta haki kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba nianze kwa kukushukuru wewe na Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama na kutoa mchango wangu katika sekta ambayo, ili kuendelea katika mambo manane, ardhi ndiyo ya kwanza; bila kuwa na ardhi hatuwezi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa sababu nne (4) zifuatazo:-

Kwanza, kitabu cha hotuba kimeandaliwa vizuri sana, maneno machache, takwimu kwa wingi.

Pili, Mheshimiwa Waziri William Lukuvi, Naibu Waziri Mheshimiwa Angelina Mabula, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na timu yake, wanafanya kazi nzuri sana ya (kupigisha mfano). Ni ukweli usiopingika kuwa, watendaji walio wengi wa Wizara ya Ardhi wamebadilika, hongereni sana, ongezeni bidii zaidi ili muwakomboe Watanzania hasa wanawake.

Tatu, mipango ya kusikiliza kero za wananchi; naunga mkono kwa sasa, Wizara imeweka mipango mizuri ya kutatua kero za wananchi kupitia Mabaraza ya Ardhi, Mahakama za Ardhi, Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Mikoa na Halmashauri za Wilaya.

Nne, Hati zilizofutwa/kurudishwa kwa wananchi; naunga mkono kwa sababu Serikali imefuta baadhi ya hati ambazo zilimilikiwa na watu wachache kwa muda mrefu bila kuendelezwa na kurudishwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushauri ninayo mambo ya kuishauri Serikali katika, sehemu chache nilizochagua kuzitilia mkazo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mpangilio wa Matumizi ya Ardhi, Wanawake na kumiliki Ardhi, pamoja na kuishukuru Serikali kwa kuhakikisha wanawake na wanaume wanapata fursa, katika umiliki wa ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Kijiji ya 1979 kifungu cha (4-5). Katika kutoa nafasi

ya umiliki wa ardhi kwa akinamama bado taratibu za kimila hazitoi fursa kwa wanawake hasa wa vijiji kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, Serikali itazame upya taratibu za kimila kwa kuzifanya marekebisho ili kutoa fursa kwa akinamama kumiliki ardhi. Ningependa Waziri atakapokuja hapa kuhitimisha Hotuba yake atuambie na wanawake wasikie kwamba, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha taratibu za kimila ambazo ni kandamizi zinazowanyima wanawake fursa ya kumiliki ardhi sambamba na wanaume zinaondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, migogoro ya wakulima na wafugaji, hifadhi na wananchi; pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya kutatua migogoro ya ardhi, bado tatizo ni kubwa. Ushauri wangu, Serikali itafute fedha ya kupima ardhi yote ya Tanzania. Ni muhimu sasa Serikali Kuu itafute fedha hata kwa njia ya mkopo kwa ajili ya kupima ardhi yote ya Tanzania na kupanga matumizi bora ya ardhi. Kila eneo lipangiwe matumizi yake ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imekuwa ikigharimu maisha ya Watanzania wengi. (Suala la kupima ardhi lisachwe kwa Halmashauri iwe ni ajenda ya Kitaifa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, utoaji wa Hati za Viwanja; pamoja na kazi nzuri ya utoaji wa hati kwa wakati, bado wananchi wanaotumia ardhi karibu asilima 80 hawana hati miliki. Mfano; katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali iliahidi kutoa hati miliki za ardhi 400,000 lakini hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2017, Serikali ilikuwa imetoa hatimiliki 33,979 tu, sawa na asilimia 8.5 ya lengo zima (ukurasa 18). Kiwango hiki ni kidogo sana ukilinganisha na uhitaji wa hatimiliki hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri, Serikali iweke mipango itakayohakikisha wananchi wote wanaotumia ardhi wanapata hati miliki. Matokeo ya mipango hii ni kwamba, viwanja vyta wananchi vitawaletea tija kwa kutumia hati zao kufikia fursa za kiuchumi. Pia Serikali itapata mapato ya uhakika; sasa wananchi watakuwa wanalipia kwa mujibu wa sheria (kodi ya kila mwaka). Swali langu, je,

Serikali imejipangaje kwa mwaka 2017/2018, kuhakikisha lengo la utoaji wa hati miliki ili kuendana na kasi ya ongezeko la idadi ya watu na mifugo inafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Mipango Miji; pamoja na kuipongeza Serikali kwa kuhakikisha Miji na Maji yanapangwa. Naomba niishauri Serikali, kuhakikisha Miji yote inakuwa na *master plan* ili kuondoa tazito la kuwa miji holela ambayo haikupangwa halafu baadaye tunapotaka kujenga miundo mbinu tunalazimika kuhamisha wananchi walijenga kabla ya miji kupimwa na kusababisha hasara kwa Serikali, kulipa fidia pia ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme na zinapotokea ajali za moto tunashindwa kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Ujenzi wa Nyumba unaofanywa na *National Housing* na Kampuni ya Watumishi *Housing*: Pamoja na kulipongeza Shirika la Nyumba na Kampuni ya Watumishi *Housing* kwa kujenga nyumba na kuwakopesha wananchi. Swali langu ni kwamba, je Mashirika haya yana mkakati gani wa kujenga nyumba za bei nafuu zaidi ambazo wananchi wengi hasa watumishi wa umma wa kipato cha chini wataweza kumudu kununua? Ujenzi wa nyumba za milioni 40 bado hii ni gharama kubwa sana kwa Watanzania ambao bado ni maskini hasa wale wanaoishi vijijini na wafanyakazi wenye kipato cha chini hasa wanawake ambao ndio walezi wa familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, Mabaraza ya Ardhni na Nyumba ya Wilaya, Mabaraza ya ardhi na Nyumba ya Wilaya bado hayapo kwenye wilaya nyingi. Kwa hiyo, wananchi wengi wanakosa haki zao kutokana na mabaraza haya kutokuwepo. Pia utengenezwe utaratibu wa kuendesha kesi ambao ni rahisi kwa wananchi kuweza kuandika maandiko juu ya matatizo hayo. Nauliza, Serikali ina mpango gani kuhakikisha mabaraza haya yanakuwepo katika kila Halmashauri/Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, Kodi ya majengo kwa sasa inakusanywa na *TRA*, Serikali iweke utaratibu mzuri wa

*TRA* kuwafikia wananchi au kushuka kwa wananchi ili kukusanya kodi hizi na aidha, Serikali ifanye tathmini kwa kiasi gani imeweza kukusanya mapato yanayotokana na kodi ya majengo ili kuona kama kuna mafanikio mara baada ya kazi hii kukabidhiwa *TRA* badala ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane ni kuhusu mashine za kufyatua matofali. Pamoja na shukrani nyingi kwa Shirika la Nyumba la Taifa chini ya Mkurugenzi Ndugu Mchechu, kutoa mikopo ya mashine za kufyatua matofali kwa vikundi vyta vijana katika Halmashauri. Je, Shirika la Nyumba la Taifa limejipangaje kwa mwaka 2017/2018 kuhakikisha kuwa mikopo ya mashine za kufyatua matofali inatolewa kwa vikundi vyta akinamama ili kuweza kujipatia kipato na kujenga nyumba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Mabaraza ya Ardhi; mojawapo ya malengo ya kuanzisha mabaraza haya ni kupunguza migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali hapa nchini na pia kuharakisha usuluhishi wa kesi za ardhi. Pamoja na malengo haya mazuri mabaraza haya haiwezekani kutekeleza majukumu yake, ufanisi umekuwa mdogo kwa kukosa vitendea kazi, watumishi wachache wenyewe maslahi duni na kutopelekewa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa zaidi ipo katika Mabaraza ya Kata ambapo ndipo kuna kesi nyingi na hawapatiwi fedha za kuendesha shughuli zao. Serikali kuwaachia Halmashauri wawezeshe mabaraza haya ni kuzidi kuyadumaza mabaraza haya kwani Halmashauri zenyewe vyanzo vyake ni vyta kusuasua na wakati mwengine hazina fedha kabisa kwani mahitaji ni mengi zaidi ya fedha hizo za *own source* katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ifanye yafuatayo:-

Kwanza, kuyawezesha mabaraza ya Ardhi ya Wilaya ikiwa ni pamoja na kuongeza watumishi ili mabaraza haya yatimize majukumu yao kwa mujibu wa sheria; na

Pili, Wizara ichukue jukumu la kuyawezesha Mabaraza ya Kata kuliko kuziachia Halmashauri, kwani mapato ya Halmashauri hayatoshelezi. Sehemu ya fedha za kodi ya ardhi katika Wilaya husika kiasi fulani zibaki ili kuyawezesha Mabaraza ya Kata katika Wilaya husika.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Ardhi. Pili, nampongeza Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano yao yaliyopelekea kutayarisha hotuba hii na kuiwasilishwa kwa utaalalm mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Ardhi, hivi sasa nchi yetu inakabiliwa na ongezeko kubwa la watu. Watu kutoka nje ya nchi yetu wanafika nchini kuomba umilliki wa ardhi kwa matumizi mbalimbali. Hivyo, Serikali yetu ni lazima iendelee kuweka utaratibu mzuri wa ugawaji wa ardhi ili kuepuka kutoa fursa kwa wageni na kuwanyima wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi inaendelea kuongezeka siku hadi siku hasa kati ya wafugaji na wakulima. Hii inatokana na ongezeko kubwa la wafugaji na upungufu wa maeneo. Nashauri Serikali kuweka mpango maalum wa kutofautisha maeneo ya wafugaji na yale ya wakulima ili kuondosha migogoro hii ambayo inaendelea kupelekea watu wa makundi hayo kuuawa. Aidha, Serikali iweke kima maalum cha ufugaji kuwa na kima maalum cha wanyama ili kuepuka matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ulinzi wake kwetu sisi sote. Pili, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Mawaziri hawa wanafanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuhakikisha wanaondoa kero zote zisizo za lazima, hasa migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Miaka michache iliyopita tulishuhudia mapigano na uvunjifu wa amani baina ya wananchi mbalimbali kwa sababu ya ama kuingiliana kimipaka ama wasio na uwezo wengi kunyang'anywa ardhi zao na matajiri wachache. Hata hivyo, tangu Mheshimiwa Lukuvi pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Angelina Mabula waingle kwenye Wizara hii, kero hiyo imepungua kwa asilimia kubwa sana. Hivyo, naomba tena kutumia fursa hii kuwapongeza sana kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote penye mafanikio hapakosi changamoto. Niendelee kuiomba Wizara hii kuendelea kupanga mijji yetu na kutoa elimu juu ya matumizi mazuri ya ardhi. Kwani ardhi haiongezeki bali watu ndiyo wanaongezeka sasa ni wakati muafaka wa Serikali yetu kuweka mipango madhubuti ya kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya ardhi ili kiliondosha Taifa letu lisiingie kwenye migogoro isiyo ya lazima huko tuendako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunayo Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na kwa mujibu wa sheria No.6 ya mwaka 2007 inayoipa Tume hii mamlaka ya kupanga Ardhi kwa matumizi endelevu ili kuondoa umaskini wa wananchi wetu. Basi niliombe Bunge lako Tukufu litenje bajeti ya kutosha ili kuwezesha Tume hii kuweza kutekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote tunafahamu kuwa wanaochangia uchumi wa nchi hii kuititia kilimo ni

wanawake, lakini kwa bahati mbaya sana sheria za kimila zinamnyima mwanamke haki ya kumiliki. Katiba ya nchi pamoja na Sheria ya Ardhi zote zinatambua mwanamke kumiliki ardhi lakini sheria za kimila zinamfanya mwanamke ku-access ardhi na siyo ku-own ardhi. Hii inafanyika kuitia mumewe au wazazi wake. Pale owner ambaye ni mume au mzazi anapofariki mwanamke huyu hunyang'anywa ardhi hiyo kwa kuonekana ardhi ni mali ya mwanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika hili ni kwamba, tunaomba sheria hizi za kimila ziletwe Bungeni, zitazamwe upya ili ziweze kumpa haki mwanamke kumiliki ardhi. Naomba pia nizungumzie kwa ufupi migogoro baina ya wakulima na wafugaji. Tatizo hili bado ni kubwa sana katika maeneo mengi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ningeshauri Serikali iweke mpango mkakati ili kuweza kutenganisha maeneo ya kilimo na ufugaji. Pia, wafugaji wetu wapatiwe elimu ya kutosha ili waweze kuacha kufuga kizamani bali waweze kufuga kisasa na kibashara zaidi. Hii itasaidia sana kupunguza migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niipongeze Ofisi ya Rais kuitia MKURABITA. MKURABITA wamesaidia sana kushirikiana na Halmashauri mbalimbali nchini kurahisisha ardhi na kuwapatia wananchi hati za kimila. Hati hizi zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza migogoro ya kimipaka baina ya wananchi. Vile vile, wananchi wameweza kutumia hati hizo kukopa fedha katika benki mbalimbali na kuwasaidia kufufua wajasiri amali. Hali hii imepunguza sana kwa kiasi kikubwa umaskini kwa wananchi wetu. Hivyo basi, naomba sana Wizara hii ya Ardhi iweze kushirikiana na MKURABITA ili wananchi wengi hasa wasio na uwezo waweze kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa maandishi kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufanya kazi hii ya kuwawakilisha wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji ardhi, ili kuiona Tanzania ya viwanda ni lazima upimaji wa ardhi upewe umuhimu wa kutosha. Kwani hivi sasa uwekezaji wa mashamba makubwa ni mgumu sana kwani vijiji vingi hivi sasa bado havijaingia kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi. Jambo linalofanya Halmashauri kukosa wawekezaji kwenye mashamba makubwa ya mazao ya kilimo na ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika Halmashauri ya Liwale yuko Mwekezaji mmoja toka Japan. Huyu ni mzaliwa wa Liwale, mwaka 2015 aliamua kurudi nyumbani na mradi wa kilimo cha alizeti lakini hadi leo anahangaika kupata shamba japo Halmashauri ilishafanya maamuzi ya kumpatia ardhi mwekezaji huyu mzawa. Hatua ya uhaulishaji ardhi ndio kikwazo kikuu kilichobakia katika kukamilisha mradi huu. Namwomba Mheshimiwa Waziri, mwenye dhamana kuhakikisha Mwekezaji huyu anapata ardhi kwa ustawi wa Wanaliwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali isiziachie Halmashauri shughuli za upimaji wa Vijiji ili kuviingiza katika matumizi bora ya ardhi. Kwani Halmashauri nyingi hazina mapato ya kutosha kumudu kazi hii. Hivyo kuvifanya vijiji vingi kukosa wawekezaji, kwani kigezo cha kwanza cha uwekezaji vijijini ni kijiji kuwa na matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa watumishi, Wizara hii ina tatizo kubwa sana la upungufu wa watumishi hasa kwenye Halmashauri zetu. Jambo hili linaongeza makazi holela katika Halmashauri nyingi kutokana na uhaba wa viwanja na Halmashauri kushindwa kupima viwanja kwa wakati na jambo linaloongeza rushwa kwa ugawaji wa viwanja na makazi yasiyopimwa. Mfano, katika Halmashauri ya Liwale hatuna Afisa Ardhi mwenye taaluma ya kutosha

na hatuna wapimaji wa ardhi tunategemea toka katika Halmashauri ya Nachingwea. Jambo hili linafanya gharama kubwa za upimaji wa viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gereza la Liwale limechukua ardhi ya wananchi tangu mwaka 1982 lakini hadi leo wananchi wenye mashamba yaliyotwaliwa bado hawajalipwa fidia ya mashamba yao. Naomba Wizara ya Ardhi wakishirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani wamalize mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mgogoro wa mpaka kati ya wanakijiji cha Kikulyungu na Wizara ya Maliasili na Utalii. Ni bora sasa Wizara zote mbili wakashirikiana katika kutatua mgogoro huu. Mgogoro wa Kikulyungu na hifadhi ya *Selous* ni wa muda mrefu sana.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi ya Ardhi, maelekezo yalitoka kwenye hotuba ya ardhi kwamba wananchi wote wanaomiliki ardhi iwe imepimwa au haijapimwa lazima walipe kodi, sasa ardhi hiyo ambayo haijasajiliwa kisheria italipiwa je kodi? Je akilipia kodi atawea kutumia *receipt* hiyo kwa ajili ya dhamana yoyote? Serikali ifuate sheria ndio maana tulizitunga ambapo wananchi hulipa kodi kwenye ardhi iliypimwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba (*NHC*), Shirika hili limekuwa likifanya kazi nzuri kujenga nyumba za biashara na makazi lakini madhumuni ya kuanzisha *NHC* yalikuwa ni pamoja na kujenga nyumba za bei nafuu ili kila Mtanzania aweze kuishi kwenye nyumba kwa haki. *NHC* imeshindwa kujenga nyumba kwa bei nafuu kutokana na vifaa vya ujenzi kuwa na bei ya juu sana na kupelekea ujenzi kugharimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuwasaidia wanyonge, lakini kwa mtindo huu wa bei za nyumba wanazozita ni za bei nafuu za milioni 60 ni mfanyakazi/Mmachinga yupi wa kawaida atakayeweza kulipia bei hiyo? Ushauri, Serikali ishushe kodi kwenye vifaa

vya ujenzi kwa nyumba zinazojengwa na *NHC* ili waweze kuendeleza kazi nzuri wanayojitahidi kuifanya kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa vitendea kazi na wataalam, pamekuwepo na uhaba mkubwa wa vitendea kazi na wataalam kwenye kitengo cha kupima ardhi ambako kunapelekea wananchi kwenda kutumia wapima ardhi binafsi na wanatoza pesa nyingi ambapo inapelekea wananchi wengi kutopima ardhi zao. Serikali inapoteza fedha nyingi kwa kutopokea kodi ya ardhi. Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya vifaa kwa nchi nzima ikiwa ni pamoja na kuajiri wataalam wa kutosha kwa nchi nzima? Mfano pale Moshi Vijiijini (Wilaya ya Moshi) hawana vitendea kazi kabisa hata usafiri haupo. Ni kwa nini hata kwa kuanzia wasiwe hata na pikipiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya kwa kujaribu kupunguza migogoro ya ardhi. Nawashauri mjaribu kutatua matatizo yaliyobaki kuna uhaba wa wataalam na vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mategememo yangu watachukua maoni ya Upinzani na wayafanyie kazi kwa faida na maendeleo ya nchi yetu na wananchi wetu.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mabaraza ya Ardhi; migogoro mingi ya ardhi inachangiwa sana na muundo wa Mabaraza haya ya Kata hasa kutokana na kutawaliwa sana na rushwa. Hii inasababishwa na kukosekana kwa mafunzo ya mara kwa mara na hivyo wajumbe kukosa weledi katika kutafsiri sheria hata kufikia maamuzi jambo ambalo linaishia kugombanisha jamii. Pia wajumbe wa mabaraza haya hata Makatibu wa Mabaraza kutokuwa na pato lolote kunapelekea vitendo vya rushwa. Hivyo nashauri yafuatayo:-

(a) Kutolewe mafunzo ya mara kwa mara kwa mabaraza haya (semina) ili kuwaongozea uelewa na uzoefu

Wajumbe wa Mabaraza ya Kata. Jambo hili litawawezesha kukabili kesi zinazojitokeza kwenye maeneo yao.

(b) Kutolewe ruzuku kwa ajili ya kuendesha mabaraza ya ardhi ya Kata, kukosekana kwa ruzuku kunasababisha mazingira magumu sana ya uendeshaji na hivyo kujenga mazingira ya rushwa.

(c) Halmashauri zipewe nguvu/mamlaka ya kuyavunja mabaraza haya pale inapothibitika kuwa yamekiuka maadili. Kwa hali ilivyo hivi sasa, kuna urasimu mkubwa katika kuchukua hatua kwa Mabaraza ya Ardhi. Jambo hili limepelekea matatizo yetu na bado wajumbe hawa wanakuwa na jeuri kwa kuamini kuwa si rahisi kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la ardhi Wilaya, katika ngazi ya Wilaya Mabaraza yetu yanakosa wataalam. Mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, kuna mrundikano mkubwa wa kesi kutokana na kukosa Mwenyekiti wa Baraza. Mara kwa mara Wilaya imekuwa inapata huduma ya Mwenyekiti ambaye haishi pale na matokeo yake anahudumia mara moja kwa mwezi na kwa muda usiozidi masaa sita. Hili limepelekea kuwepo kwa kesi za mipaka miaka miwili zisizofanyiwa maamuzi. Ombi, Baraza la Ardhi la Wilaya ya Ukerewe lipangangiwe Mwenyekiti wa Baraza ambaye atakuwepo muda wote ili kupunguza migogoro ya ardhi hasa ikizingatiwa kuwa eneo katika Wilaya hii ni dogo na hivyo kuwa na migogoro mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifaa vya upimaji; kuwe na utaratibu mzuri wa kupatikana kwa vifaa vya kupima ardhi ili mipango mizuri ya matumizi ya ardhi iwezekane.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi, nilichangia katika hotuba ya Utumishi na Utawala Bora, kwamba mabaraza haya tuyajengee uwezo japo hata kutembelewa na Mwanasheria *as an observer* ili tu kujiona *proceedings* kusudi upungufu

utakaobainika, itafutwe namna ya kuupunguza kwa kutumia ama semina au mafunzo ya muda mfupi kadri ya mazingira yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Diaspora vs Umiliki wa Ardhi*; lililoko tamko ambalo limeleta mkanganyiko hasa kwa Watanzania ambao wanaishi nje ya nchi lakini wamebaki na utaifa/uraia wao kama Watanzania. Tafsiri ya watu wengi walioko nje ni kwamba kwa Mtanzania anayeishi nje hastahili kumiliki ardhi kumbe iwekwe wazi kwamba ni haki kwa Mtanzania kumiliki ardhi hata kama anaishi nje ilimradi tu ni raia wa Tanzania kwa wale waliobadilisha uraia *diaspora per se*, utaratibu mbele ya safari uje utazamwe ilimradi kufungua fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafinga Mjini vs upimaji wa ardhi na uwepo wa *Master Plan*. Mji wa Mafinga unakua kwa kasi sana kutokana na biashara ya mazao ya misitu (mbao, nguzo, milunda na kadhalika.) Ukuaji huu umeleta mahitaji ya ardhi iliyopimwa kwa kasi, hata hivyo uwezo (*capacity*) wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga kuendana na *speed* hiyo umekuwa mdogo kutokana na uhaba wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi/ushauri, Wizara ifikirie kuwezesha upimaji/uandaaji wa *Master Plan* kwa Mji wa Mafinga na maeneo mengine ambayo ni miji ili kuepukana na ujenzi holela/*squatters*. Kwa jitihada zangu nilionana na Profesa Lupala ambaye kwa ushirikiano na ushauri wake, wanafunzi wa *field* wa Ardhi *University* watatusaidia kukusanya *data* ili baadaye Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri yetu tutakamilisha *Master Plan*. Nimewasilisha ombi la kupewa baadhi ya watumishi wa ilivyokuwa *CDA* hasa Maafisa Ardhi, Mipango Miji na Wapimaji kama jitihada za kukabiliana na uhaba wa watumishi wa kada ya ardhi ili kufanikisha azma ya kupanga Mji wa Mafinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi; naamini ni jambo la gharama kubwa lakini kama sehemu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na

kukabiliana na migogoro ya wakulima na wafugaji, hatuna namna zaidi ya Wizara hii ku-take *lead* kwenye suala hili ambalo linagusa kilimo, maliasili na hata usalama wa nchi. Tukifanikisha jambo hili tutaondokana na malalamiko mengi ya kila mmoja katika Taifa kuanzia kilimo, kufuga, hifadhi na hata uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutengwa maeneo ya *Industrial Clusters*; wakati tunapoelekea uchumi wa viwanda ni muhimu kila Halmashauri kutenga maeneo kwa ajili ya viwanda na kwa kuwa uwezo wa kupima maeneo yote ni mdogo, basi angalau tuanze na jambo hili kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambayo imekuwa ikilisema jambo hili mara kwa mara katika kulitekeleza. Nashauri utolewe Waraka kwa kushirikiana na TAMISEMI kuziagiza Halmashauri kutenga hizo *Industrial clusters*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Raís wangu kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuwatumikia wananchi hasa wale wanyonge. Pia nimpongeze Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na timu yake kwa hotuba yake nzuri iliyojaa matumaini makubwa yenyе nia ya dhati na yenyе kugusa na kuondoa kero zote za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri Serikali iwape fedha Wakala wauzaji wa vifaa vya ujenzi vya bei nafuu. Kama kweli Serikali inataka Watanzania wenye kipato cha chini wawe na uwezo wa kununua nyumba za bei nafuu. Basi tuwawezeshe Wakala wa vifaa vya Ujenzi. Pamoja na hayo, wakala wawe wanatoa elimu ya ufundi. Kwa hiyo, wakala wale wapewe uwezo ili wafike mkoani hadi wilayani kutoa elimu kwa vijana wetu wa Kitanzania ili vijana wetu wakishapata elimu waweze kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niishauri Serikali yangu, iharakishe na kutoa mafungu katika Wilaya ili mafungu haya yaendane na kasi ya upimaji na upatikanaji

wa hati kwa haraka. Kwa mfano, Wilaya ya Lushoto wananchi wapo tayari kupimiwa na kupewa hati lakini kuna ukiritimba katika idara ya ardhi. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri afuatilie hili suala katika Ofisi ya Ardhi Lushoto ili wananchi wangu wasinyanyasike pindi tu wanapotaka kupimiwa shamba na hao wananchi wameshajua umuhimu wa kupima ardhi na ukizingatia watu wanahitaji kupata mikopo kwenye mabenki. Pamoja na hayo kuna rushwa sana katika Idara ya Ardhi, maana wananchi wengi wametoa fedha zao ili wapate hati lakini fedha zinaliwa na hati hawapati. Naomba Mheshimiwa Waziri aondoe tatizo hili katika Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali yangu Tukufu ili migogoro katika nchi hii iishe ni kupima ardhi yote ya nchi hii. Naamini maeneo yote yakipimwa na kila mtu akamiliki ardhi kihalali migogoro hii itakwisha. Pia nniombe Serikali yangu itenye mafungu ya kutosha yaende katika kupima ardhi kuliko kutegemea wafadhili. Mheshimiwa Waziri nimependa sana zoezi lile linaloendelea katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Kilombero. Kwani ni mpango mzuri na wenye tija. Kikubwa wapewe mafungu ya kutosha ili kuharakisha zoezi lile. Pamoja na kuwaongeza wataalam ili kumaliza zoezi kwa haraka na ikiwezekana ifikapo 2020 Ardhi yote ya Tanzania iwe imeshapimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii muhimu kwa utoaji huduma katika sekta ya Ardhi. Migogoro ya ardhi nchini ni mikubwa mno hivyo naomba kuendelea kuishauri Serikali, kuitia Wizara hii ya Ardhi kuweka mpango madhubuti, kutenga maeneo ya wakulima na wafugaji ili kuepuka migongano hii ambayo haina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). Kumekuwa na changamoto kubwa ya kodi nyingi

kwenye ujenzi wa nyumba za *NHC*, hivyo kupelekea nyumba hizi kuendelea kuuzwa bei ya juu. Kama Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii nimekuwa nikitoa maoni yangu kuhusu Wizara ya Miundombinu, Nishati na Madini, Maji na Umwagiliaji ili kuona ni namna gani ya kupunguza mzigo kwa *NHC* ambao imekuwa ikiubeba na kugharamia kila kitu na kufanya gharama hizi kwenda kwa mnunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kubwa za upimaji wa ardhi; kumekuwa na malalamiko makubwa kwenye suala la upimaji wa ardhi na hivyo kupelekea wananchi wengi kutokupima ardhi zao. Ushauri, Wizara ya Ardhi ishirikishe sekta binafsi katika suala la upimaji. Maeneo mengi kwenye Halmashauri zetu hayajapimwa hivyo kufanya ugumu wa uwekezaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Wizara ya Ardhi kujikita kwenye mikoa mipy na inayokuwa ili kuendelea kupanga mipango miji ambayo ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu, sambamba na kujenga maeneo ya uwekezaji kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Songwe ni mkoa mpya, nashauri Wizara itoe upendeleo wa kipekee kuendeleza Mkoa wa Songwe kwa kupima viwanja, kutenga maeneo ya uwekezaji ili kuvutia wadau mbalimbali kuendeleza mkoa, sambamba na ujenzi bora wa nyumba za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri kwa hotuba nzuri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi inayoleta faraja kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayoendelea kufanya yapo mambo yanayohitajika kufanyiwa kazi kuwa nguvu:-

- Wizara kuongeza *speed* ya kupima ardhi yote ya Taifa hili. Kiasi cha asilimia 15% ni kidogo sana, eneo kubwa bado halijapimwa.

- Kupima maeneo kwa ajili mifugo na malisho. Sheria ya Ardhi imeelekeza Waziri kutenga ardhi kwa ajili ya mifugo na malisho, kuyagazeti na kuyalinda.

- Serikali itueleze ni maeneo kiasi gani na wapi maeneo ya malisho yametengwa na kupimwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza *speed* ya kuanzisha Mabaraza ya Ardhi katika Wilaya zote hapa nchini, ili kurahisisha usuluhishi wa migogoro ya ardhi. Mabaraza tuliyonayo ni 53 tu, yanayofanya kazi ni machache sana. Mabaraza haya yawezeshwe kifedha ili yaweze kutekeleza majukumu yao vizuri. Pia Serikali iwezeshe Wajumbe wa Mabaraza kwa kuwapa posho wanapokaa wafanye kazi yao vizuri. Serikali/Wizara kufanya *follow-up* kwa Maafisa Ardhi popote walipo watekeleze majukumu yao kwa kuwajibika na kuza ardhi mara mbili (*double allocation*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viongozi wa Vijiji wapewe elimu wafuate Sheria ya Ardhi katika kugawa ardhi ya wananchi. Viongozi wanakula rushwa wanauzwa maeneo makubwa bila kuitisha mikutano ya wananchi. Waziri atoe tamko hapa Bungeni lakini pia semina kwa viongozi wa Vijiji ni kiasi gani cha ardhi kinaweza kuuzwa na viongozi wa vijiji na kiasi gani hawaruhusiwi. Wafugaji wanapokelewa vijijini wanatoa fedha nyingi, wanapewa maeneo ya kufugia wakati wananchi wengine hawana habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kama Taifa tuwaze miaka 100 ijayo mbele. Leo tunajivunia Tanzania tuna ardhi kubwa, tusipopanga matumizi bora na hii ardhi tutakosa ardhi kwa matumizi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika na Taasisi zinazojenga majengo na nyumba za makazi wajenye nyumba kwenda juu (*flats*) na sio kwenda chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wa miradi mbalimbali wapewe ardhi kuendana na mradi wao au eneo linalofaa kwa mradi huo. Maeneo ya kilimo yabaki kwa kilimo, maeneo ya malisho yabaki kwa malisho na maeneo ya ujenzi yasiwe ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uanzishwaji wa miji kiholela bila utaratibu; maeneo mengi kila leo miji mipyä immeanzishwa kando kando ya barabara, hakuna maelekezo yoyote, hakuna udhibiti, hayo yanakuwa makazi holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watumishi *House* waongeze *speed* ya kujenga nyumba za watumishi, *speed* yao ni ndogo sana. Wafike kwenye wilaya mpya ikiwepo Kaliua wajenge nyumba za watumishi kusaidia makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba (*National Housing*) waliahidi kuja Halmashauri ya Kaliua kujenga nyumba tangu mwaka 2016. Napenda kujua ni lini watafika na maeneo tulishayatayarisha ya kutosha na yapo mjini.

**MHE. DEVOTA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hotuba ya Waziri kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze Waziri na Naibu Waziri wa Ardhi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha ardhi inawanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo baadhi ya mambo ambayo lazima tuseme ili kusaidia kusukuma Wizara hii muhimu kwa Watanzania. Ofisi za Ardhi za Kanda, mpango huu ulipoanzishwa ulikuwa na nia ya kusogeza huduma karibu na wananchi. Kanda ya Kati, Mkoa wa Morogoro ndipo yalipokuwa Makao Makuu na Wizara/Serikali ilijenga Ofisi za Ardhi za Kanda kwa gharama kubwa. Ofisi hii zimesaidia sana chini ya Kamishna imepunguza kwa kiasi fulani migogoro na malalamiko ya ardhi hususan Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri amesema katika hotuba yake, Serikali imebadilisha/kuhamisha Ofisi ya Kanda Morogoro na kuhamishia Dodoma, hii si sawa. Kwa kipekee Mkoa wa Morogoro utazamwe kwa namna nyingine kutokana na kukithiri kwa migogoro ya ardhi ya mara kwa mara ambayo imegharimu maisha ya watu kwa kusababisha vifo na majeruhi hasa katika Wilaya za Kilosa, Kilombero, Mvomero na Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa vifaa vya kupimia ardhi; Maafisa Ardhi wanafanya kazi katika mazingira magumu ambapo unakuta mfano, Mvomero ina kifaa kimoja tu cha kupima, hali inayosababisha ucheleweshaji wa upimaji wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kero ya bomoa bomoa; katika vitu vinavyolalamikiwa na wananchi ni uvunjaji wa nyumba za wananchi wanaojenga kwa jasho kwa vibali vyote kwa kuzingatia masharti mbalimbali hasa waliopo kando ya barabara ambapo hivi sasa Serikali kupitia *TANROAD* wanakusudia kuvunja nyumba za wananchi na barabara ya Dar es Salaam, Morogoro kwa zaidi ya mita 20 kila upande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hizi zinafanyaje kazi Ardhi na Miundombinu? Kwa nini kusiwe na mpango wa kuzuia wananchi kujenga badala ya kusubiri wananchi wajenge kisha waje kubomoa. Yapo maeneo ambayo wananchi nao wamepelekewa huduma muhimu kama maji, umeme na kadhalika

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgogoro wa ardhi ya vijiji-Kakonko; Vijiji vya Nyakayenzi na Kiga vina mgogoro wa mpaka wa muda mrefu kwenye bonde la Mto Ruhwiti. Mgogoro huo ulipelekea Kijiji cha Kiga kuhodhi ardhi ya Nyakayenzi kwenye mpaka wa vijiji hivyo. Mheshimiwa Waziri alipokuja Kigoma, akiwa Kibondo viongozi wa Nyakayenzi walifanikiwa kuonana na kuongea na Waziri aliagiza *DC* ashughulikie kutatua mgogoro huo ambaao maamuzi aliyotoa hayakuwaridhisha wananchi wa

Kijiji cha Nyakayenzi maana wananchi wa Kiga walipewa haki ya mashamba kwenye eneo la Nyakayenzi. Wananchi wa Nyakayenzi walitaka mashamba hayo yaendelee kutambuliwa kama ya Nyakayenzi huku yakilimwa na wananchi wa Kiga kwa mujibu wa ramani na mipaka ya vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikata rufaa kwa Waziri Bunge lilitlopita na kuwasilisha kwa Naibu Waziri wa Ardhi. Ushauri, naomba Serikali/Wizara isimamie na kumaliza mgogoro huo kwa kujibu au kushughulikia rufaa hiyo. Bado wananchi wa Nyakayenzi wana imani na Wizara kuwa haki itatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa ardhi kambi ya JKT Kanembwa na Vijiji; kumekuwepo na mgogoro kati ya eneo la Kambi ya JKT Kanembwa na Kijiji cha Kazilemihunda kwani mipaka imekuwa ikibadilika mara kwa mara kwa Kambi kuongezea eneo na kuingia katika ardhi ya Kijiji cha Kazilamihunda. Ushauri, maeneo hayo yapimwe kwa kushirikisha Serikali ya Kijiji cha Kazilamihunda na uongozi wa Kambi ya Kanembwa JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ya wananchi iliyochukuliwa Kambi ya Wakimbizi-Mtendeli. Kuna wananchi wa Kasanda walionyang'anywa ardhi ili kupisha wakimbizi kwenye Kambi ya wakazi Mtendeli. Baada ya ardhi hiyo kuchukuliwa wananchi hawakupewa ardhi nyingine kwa matumizi ya kilimo na mifugo. Ushauri, wananchi hao wapewe ardhi nyingine pamoja na fidia kwa mazao yaliyoharibika hasa eneo la juu ya Kambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri juu ya bomoa bomoa, kumekuwepo na bomoa bomoa ya nyumba zilizokwishajengwa hasa zile ambazo zimekamilika ama kwa kigezo cha nyumba, kujengwa eneo lisilostahili kama vile hifadhi ya barabara, *open space*, hifadhi ya Mto, Ziwa, Bahari, na kadhalika. Mjenzi anakuwa na *documents* zote za ardhi, kama vile ramani, kiwanja na amelipia na kadhalika. Ushauri, kwa nini ardhi wasisimamie kuhakikisha hawatoi kibali cha

ujenzi bila kuwasiliana na Wizara ya Miundombinu na Mazingira kujiridhisha kuwa eneo hilo linaruhusiwa kujengwa nyumba kuliko kuacha ijengwe kisha inabomolewa.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mikakati mingi mizuri ya Wizara ya Ardhi, bado kuna changamoto nyingi katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii ungewekwa mkakati wa dharura wa kuhakikisha inawapimia mapema kabla hawajajenga wawe na hati ili kuondoa migogoro ya fidia kupunjwa na kunyanyasa wanaopisha ujenzi wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi Manispaa ya Mpanda; Kata nyingi za Manispaa ya Mpanda hawajapimiwa je, ni lini sasa Wizara kuititia Ofisi za Kanda itaharakisha kupima maeneo haya ili wananchi wapate hati ambazo zinaweza kuwasaidia kukopa fedha katika benki. Kata ya Illembu, Misunkumilo, Kata ya Kakese, Kata ya Mwamkulu na Kata ya Kashamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara isisubiri watu wajenge nyumba zao nzuri halafu inakuja kubomoa na kuwalipa fidia ndogo na za kucheleweshwa. Katika Bajeti hii Mheshimiwa Waziri ameonesha wazi kuwa na dhamira ya kutatua kero ya fidia kwa kuanzisha Bodi ya Fidia hii ikasimamiwa vizuri itasaidia vizuri na kuondoa kero za malalamiko nchini, hii nadhani ipangiwe mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi na wananchi wa Kata za Mpanda hotel na Misunkumilo; naomba bajeti hii ione namna ya kutatua mgogoro huu ni wa muda mrefu sana .

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza gharama za uuzaaji nyumba za NHC Manispaa ya Mpanda; mpaka sasa hakuna faida iliyopatikana kutokana na uuzaaji wa nyumba hizi, je hamwoni kuendelea kuziacha nyumba, kama

gharama haziwezi kupungua basi zipangishwe kwa watumishi wa Serikali kwa sababu kuna uhaba wa nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu katika nyumba hizo bado haitoshi, barabara, hospitali, shule, masoko. Hivyo kwa kuzingatia ukosefu wa miundombinu hii ndio inasababisha watu kushindwa kuhamia kule.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumza juu ya mgogoro wa muda mrefu wa shamba la Malonje. Serikali inatakiwa kumaliza mgogoro huu ambao Serikali imekuwa ikipiga danadana kila siku. Hakuna jambo linaloweza kushinda Serikali kwani tunashuhudia jinsi Mheshimiwa Waziri Lukuvi anavyojitahidi kutatua migogoro mbalimbali katika nchi hii na mara ya mwisho aliwaahidi wananchi wa Vijiji vinavyozunguka shamba hilo kuwa atakuwa Waziri wa mwisho kuzungumzia mgogoro huo. Hivyo wananchi walishajenga imani kubwa sana kwake kwa kauli aliyoitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba aumalize mgogoro huu. Kama kuna makosa yaliyofanywa na viongozi wa Wilaya, Mkoa ndiyo maana yote hayo yamefikishwa kwake hakuna sababu tena ya kukwepa jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Tarafa ya Kipeta na hifadhi ya akiba ya Uwanda Game Reserve. Tunaomba mipaka ichunguzwe upya kwani uwekaji wa mipaka ya hifadhi hiyo imeingilia maeneo ya Vijiji jambo linalofanya wananchi wa maeneo hayo kukosa ardhi ya kilimo na mifugo, tunaomba Serikali ifuatilie jambo hili haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa vijiji hivyo wapo hapa Dodoma kutaka kuonana na Mheshimiwa Waziri Lukuvi, pia ikishindikana kumwona Mheshimiwa Waziri, wamwone Mheshimiwa Rais. Tunaomba wasikilizwe (ni juu ya shamba la Malonje).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa kwenye Mabaraza ya Ardhi, Vijiji na Kata, ni vurugu na mambo ya ajabu. Mfano, hukumu inampa ushindi mtu kwa kuwa alileta mashahidi wengi kuliko upande wa pili. Wananchi wanazungushwa sana katika rufaa hawapewi hukumu mpaka anakata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeruhusu makampuni binafsi ya upimaji waweze kushirikiana na Halmashauri zetu kibiashara/Huduma. Watendaji wa Halmashauri bado hawataki kushirikiana na Makampuni hayo mfano ni Halmashauri ya Biharamulo. Tunaomba uharakishwaji wa utatuzi wa migogoro mikubwa ambayo nimeorodhesha tayari. Mfano Mgogoro wa Jeshi na Kijiji cha Rwebya unasumbua sana.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa mageuzi makubwa aliyoafanya na anayoendelea kuyafanya katika Wizara hii. Namtakia kila la kheri na ni matarajio yangu kuwa tutafika mahali pazuri pa kuwa na Wizara na Taasisi zinazowajibika ipasavyo. Katika sekta hii muhimu sana kwa maendeleo ya kijamii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi na dira hizi naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri, kupitia kwa kina bila hiyana hotuba ya Kambi ya Upinzani na kuyafanyia kazi mengi ya mapendekezo yake. Sote katika Bunge lako hili Tukufu tupo kwa maslahi ya wananchi wetu na si vinginevyo na hivyo tukishirikiana itapatikana tija zaidi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimshauri Mheshimiwa Waziri, kushughulikia kwa kina suala la kuwapatia na kuwahakikisha watumishi wa umma nchini makazi bora na ya uhakika katika maeneo mbalimbali. Hivi sasa *NHC* inaonekana kuweka mkazo zaidi katika kujenga na kuuza badala ya kupangisha hata kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa umma kwa asili yao si watu wa kudumu katika maeneo yao ya kazi bali katika maeneo yao ya kuzaliwa. Hivyo msisitizo unapowekwa katika kuwauzia nyumba watumishi panatengeneza mazingira ya kuwafanya watumishi wa umma, kutaka kubaki maeneo waliyopangiwa na wakati mwingine kutumia hata njia chafu kuhakikisha kuwa hawa hawahamishwi. Hali hii si zuri kwa kujenga kada ya watumishi wa umma waadilifu na walio tayari kutumikia popote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Wabunge wako wengi nikiwemo mimi mwenyewe, tumehangaika kwa zaidi ya mwaka na nusu sasa kutafuta makazi ya kukaa hapa hapa Dodoma, Makao Makuu ya Serikali. Hii ni dalili wazi kuwa Wizara hii na Serikali kwa ujumla hajatoa kipaumbele au hajajipanga ipasavyo katika eneo la makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuwapongeza, Waziri Mheshimiwa Lukuvi, Naibu Waziri Mheshimiwa Angelina Mabula, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuleta bajeti hapa Bungeni ili tuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Migogoro ya Ardhi, niipongeze Wizara na Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii kwa kuendelea kutatua migogoro mingi nchini ikiwemo ya wakulima na wafugaji. Ni kwa nini Serikali isingetenge maeneo ya wafugaji peke yake na yakaainishwa na yakawekewa miundombinu kwa ajili ya kuwezesha wafugaji kutohama hama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ipo migogoro inayowahuju Maafisa Ardhi katika Halmashauri zetu. Tunashukuru hata hivi Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wanafanya juhudini kubwa sana kuwasaidia wanyonge waliokuwa wakipokonywa ardhi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanagawiwa ardhi ya eneo moja zaidi ya watu wawili na kusababisha

usumbufu mkubwa sana, lakini huwa tunapata tabu sana, Afisa anayeharibu Halmashauri moja badala ya kubadilisha anahamishiwa eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Wataalam wa Ardhi; Halmashauri zetu nyngi nchini bado zina upungufu mkubwa na kunasababisha wananchi wengi kupata usumbufu mkubwa wanapotaka kupimiwa ardhi au kupata hati na sasa hivi na hili la vyeti feki nalo limechangia kwa kiasi kikubwa sana kuendelea kuwa na idadi ndogo ya wafanyakazi. Ni vizuri Serikali ikaweka utaratibu wa kujua nafasi hizi mapema ili kusaidia utendaji katika Halmashauri zetu na kupunguza kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango Miji, ni kwa nini miji yetu mingi hajapangwa, je kazi ya Maafisa Mipango Miji ni nini? Kumekuwa na mwingillano mkubwa sana wa shughuli katika miji yetu kama vile hakuna wataalam. Ushauri wangu ni vizuri Maafisa Mipango Miji wangekuwa wanasimamia ile michoro iliyopangwa au kama miji haujapangwa basi wasigawe viwanja kabla ya kuitishwa michoro. Hata hivyo, kuna maeneo ambayo hayajapimwa ungekuwepo utaratibu maalum ili kuweza kusaidia jamii, kwa sababu kuna baadhi ya maeneo hayafikiwi kihuduma, wananchi wamekuwa wakipata mateso makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *NHC*, niipongeze Serikali kwa ajili ya kazi nzuri inayofanywa na Shirika hili, lakini tuombe majengo haya yajengwe hata katika miji midogo sababu hata wafanyakazi wanapata shida sana wanapohamishiwa mikoani. Ni kwa nini Halmashauri zetu zisitenge maeneo na kuingia ubia nao ili iweze kusaidia upungufu uliopo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, haya mashirika yanayojenga nyumba kwa ajili ya Walimu kama Watumishi *Housing* nao wangefika katika Halmashauri zilizopo pembezoni ambako kuna matatizo makubwa sana ya nyumba za watumishi wakiwemo Walimu hata kama ya

kawaida sana ya vyumba vitatu au viwili ili kuyafanya maeneo hayo pia wafanyakazi waweze kuishi kama mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko ya ukarabati wa nyumba za mjini, naomba kujua je kuna sheria yoyote iliyotolewa na Serikali nyumba za katikati ya mji zisikarabatiwe zijengwe maghorofa. Sababu kunakuwa na malalamiko kwa wananchi wa Manispaa ya Iringa kutopatiwa vibali vya kukarabati nyumba zao hata kama ni magofu na kusababisha majengo mengi kuwa na hali mbaya sana. Sababu hawana uwezo wa kujenga maghorofa sasa tunaomba Serikali itupatiate ushauri. Sasa hivi hakuna wawekezaji kabisa kutokana na hali ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeiwezesha leo kupata nafasi na kuweza kuchangia angalau kwa maandishi. Pili, nichukue nafasi hii kukupongeza kwa kazi nzuri, pamoja na Mheshimiwa Spika, na Naibu Spika na Wenyeviti wenzako. Nizidi kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wataalam na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya, nawaombea Mungu wasonge mbele kwa kazi yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunajua kuwa Morogoro ni mkoa ulioweka historia, kwa migogoro ya wafugaji na wakulima. Nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayoendelea nayo, ya kupima, kurasimisha na kutoa hati miliki kwa wananchi. Upimaji wa ardhi na kuwamilikisha wananchi kwa kupewa hati ya kumilikisha ardhi hii ni mkombozi wa kutatua migogoro. Naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, upimaji wa vijiji na mashamba pia ni utatuzi tosha wa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilifikia wakulima kushindwa kwenda mashambani na hasa Mbigili, Kilangali na sehemu za wakulima wa Mpunga Wilayani Kilosa kama

Mabwerebwere. Kundi kubwa la wanawake, ambao ndio wakulima wakubwa, kweli, hali ilikuwa mbaya mpaka mapigano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo pia ilifikia wakati ikakatwakatwa mpaka wengine kufa. Mifugo ilihamia katika Wilaya zote za Mkoa wa Morogoro, Kilosa, Gairo, Mvomero, Morogoro Vijiji, Morogoro Manispaa, Kilombero, Malinyi na Ulanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na kuipongeza Serikali kwani baadhi ya Mawaziri walifika na hasa Mvomero na Kilosa ili kuona na kutatua migogoro hii kwa kusaidiana na Uongozi wa Mkoa na Wilaya, nawapongeza. Tatizo kubwa lilikuwa ni kutafuta malisho na maji katika ardhi iliyo wazi ambayo haijapimwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na kupongeza Serikali ya Uingereza Sweeden na Dernmark kwa kuititia kwenye Mashirika yao ya Maendeleo DANIDA, SIDA, na DFID, kwa ufadhili wao wa upimaji ardhi mpaka kutoa Hatimiliki na kujenga Masjala ya Ardhi katika Wilaya ya Kilombero, Ulanga na Malinyi. Naamini, upimaji kiasi chini ya Serikali umefanyika Mvomero na kidogo Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji ardhi ni gharama, Nashauri na kuionomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, fedha ziendelee kutafutwa, kama tulivyosaidiwa na nchi rafiki zetu kwenye mradi huu wa Kilombero, Ulanga na Malinyi, kusudi wananchi wote katika Wilaya hizi, kila mmoja apimiwe ardhi yake na kupewa hati miliki. Wakati mwingine tunashauri, taasisi Mheshimiwa Waziri, hata maeneo ya taasisi zetu zikapimwa na kupewa Hati miliki za maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yetu ione kuwa upimaji ardhi na matumizi bora ya ardhi ni muhimu kwa utatuzi wa migogoro ya ardhi. Nishauri maeneo yote ya wilaya zote za Morogoro yapimwe na wananchi wapewe hati miliki zao. Matumizi bora ya ardhi kwa kuchanganua ni wapi kilimo, mifugo, ifanyike na kadhalika. Hii itasaidia

wananchi na kwa kuambatanisha na miundombinu kama mabwawa na majosho. Sasa hivi tumetulia kwa sababu malisho yapo baada ya mvua kunyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ikiwezekana Mikoa/Wilaya zote zenye migogoro, ardhi yao ipimwe. Pia Hati miliki inaweza kutumika katika kuomba mikopo. Naomba benki (*CRDB, NMB, NBC*) wazipokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba (*NHC*) pamoja na Watumishi *Housing*, natoa pongezi kwa Serikali kwa kazi hii, liko tatizo nyumba hizi ni ghali. Nashauri, Serikali itathmini tena ili gharama zipungue, wananchi na hasa vijana wapate pa kuishi na kumudu maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa ardhi ni wachache, kwa hiyo, nashauri kwa kupitia Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo cha Tabora na Morogoro udahili uongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DESPERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Pia nampongeza Waziri, Naibu Waziri, kwa kuchapa kazi, wamejitahidi kufanya kizalendo na wametatua migogoro mingi sana. Wananchi wamekuwa sasa na imani na Serikali yao kuhusu namna migogoro ya ardhi inavyoshughulikiwa. Wito wangu waendelee kufanya kazi na kusimamia haki za wananchi katika masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Nkasi Kusini lina mashamba na hifadhi nyingi za kufanya wananchi kukosa ardhi ya kilimo. Nashauri Wizara kuona kama mashamba yaliyopo Jimboni yanaendeshwa kwa ufanisi au la ili kuweza kutoa uamuzi wa kuongeza ardhi kwa wananchi.

- Shamba la Nkundi linalotumiwa na Mheshimiwa Mzindakaya. Wananchi jirani hawana ardhi ya

kutosha na sehemu kubwa halitumiki ipasavyo lipunguzwe wapewe wananchi wangu.

- Shamba la Kalambo Ranchi lina ukubwa wa hekta 23,000, lakini lina ng'ombe 710 tu. linatumika chini ya kiwango eneo kubwa halitumiki. Lipunguzwe wapewe wananchi wangu.

- Shamba la Milundikwa kwa eneo walilopewa JKT mwaka jana ni kubwa lote halitumiki na wananchi wengi wanalima ndani bila kuruhusiwa kwa sababu ya ukosefu wa ardhi ya kilimo, lipunguzwe wapewe wananchi.

- Shamba la China linatumika lakini tuone kama lazima lote liwe kwa mtu mmoja wakati watu wengi hawana ardhi ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Misitu ya *TFS* imepora ardhi ya Kijiji cha Kasapa na kufanya kijiji kukosa kabisa eneo la kulima. Naiomba Wizara ionne namna ya kuwasaidia wananchi wa kijiji hiki. Maeneo yao ambayo wamekuwa wakilima miaka yote, tangu miaka ya 1956 yametwaliwa na kufyeka mazao yao. Wizara inisaidie kutatua mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya King'ombe, Mlambo, Ng'undwe, Mlalambo, Nkata na Kasapa vinadaiwa kuwa Ndani ya Mbuga ya Lwanfi *Game Reserve*, kwa hiyo, wananchi hawana ardhi na wanapata usumbufu mkubwa. Kamati ya Migogoro ya Ardhi itembelee kuona shida iliyopo.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. Baada ya hayo, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni rasilimali muhimu kwa kilimo, ufugaji, viwanda, misitu, hifadhi na kadhalika, hatimaye kwa kutuhifadhi sote tutakapokufa. Bahati mbaya sana, Mungu alishamaliza kuumba ardhi. Kwa namna hii

lazima usimamizi wa ardhi ufanyike kwa uangalifu mkubwa sana. Mpango wa matumizi bora ya ardhi unahitajika sana na Serikali ina wajibu wa kuziwezesha na kusimamia Halmashauri zote nchini, vijiji vyote na mpango wa matumizi bora ya Ardhi ya Vijiji chini ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto, yako mashamba makubwa katika maeneo mbalimbali ambayo hayaendelezwi vizuri na baadhi kuwa mashamba pori. Kwa kuwa baadhi ya mashamba haya; umiliki umebatilishwa na Hati kufutiwa, ni lini sasa mipango ya matumizi ya mashamba hayo itafanyika? Ushauri wangu ni kwamba, hayo mashamba yagawiwe vyama vyta ushirika na vijiji, badala ya kugawa kwa watu binafsi. Kwani ni wengi na itasababisha migogoro zaidi, mbaya zaidi wananchi wengine huuza maeneo waliyogawiwa. Katika mashamba hayo yatengwe pia maeneo ya uwekezaji wa viwanda, ujasirimali wa vijana, shule, vituo vyta afya na mahitaji mengine ya shughuli za Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi yaliyofanywa mwaka 1973 kumilikisha mashamba makubwa ya kahawa kwa Vyama vya Msingi vya Ushirika huko Kilimanjaro, tunaona faida zake hadi sasa. Baadhi ya wawekezaji wanalipa kodi ya pango kwa Vyama vya Ushirika, lakini pia wanatoa maeneo kwa shughuli za jamii. Muhimu zaidi ni kwamba bado wanaendeleza zao la kahawa. Ombi, wawekezaji hawa washauriwe kuelimisha jamii inayowazunguka jinsi ya kuendeleza zao la kahawa kuitia *CSR –Corporate Social Responsibility*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. STELA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza kaka yangu Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Waziri; na Naibu wake Mheshimiwa Angelina Mabula kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni moja tu kwa Mheshimiwa Waziri. Nyasa ni Wilaya changa, lakini ina

*potential* nyingi hasa *beach*. Tunaomba msaada wa ruzuku ya upimaji wa ardhi ili kuipanga Wilaya yetu vizuri. Gharama za kodi za ardhi ni kubwa hasa kwa taasisi za Serikali ambazo zimehitaji maeneo makubwa na ulipaji wa ardhi hizo ni Serikali yenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini maeneo ya Serikali kama Vyuo mfano (*UDOM*), Sokoine na Vyuo vingine kama *FDCs* ambavyo maeneo hayo ni muhimu kwa ajili ya shughuli za vitendo kwa nini yasimilishikwe na kupewa hati kwa gharama za upimaji tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri alifikirie hilo kwa niaba ya ombi la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nawasilisha.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote. Kwa umakini wao ndani ya Wizara hii, kwa matokeo mazuri hadi sasa kwa wananchi na kuwapa matumaini ndani ya changamoto zao za ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto nyingi za ardhi kwa wananchi wetu na kupelekea miji yetu kuwa na majengo ndani ya ujenzi holela na maeneo yasiyopimwa yanaleta magomvi kwa wananchi wetu, mandhari ya mji itakuwa siyo nzuri kiusalama na malalamiko ya wananchi hayapati ufumbuzi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Waziri kwa umahiri wake aone uwezakano wa kuteua Kamati za Kugawa Ardhi ngazi ya Wilaya haraka iwezekanavyo, kwani Mkoa wa Rukwa unachipukia kukua na wananchi kuwa na kasi ya maendeleo yao na Wilaya moja (Nkasi) tu ndio yenye Kamati ya Kugawa Ardhi. Wilaya ya Kalambo na Sumbawanga tushughulikiwe, hali mbaya hivi sasa, miji yetu itashindikana kupangiwa hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa upo pembezoni, lakini kwa mujibu wa taarifa ya Halmashauri ziliviyotekeleza katika kutoa Hati miliki, Vyeti vyaa Ardhi ya Kijji, Hati Miliki za kimila. Ukurasa Na. 109 umedhihirisha kwenye jedwali Na.4 kwa Mkoa wa Rukwa haujafanya vizuri ni kutokana na rasilimali watu na rasilimali fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mkoa wa Rukwa kuangaliwa kwa ukaribu zaidi, tukifahamu wazi kuwa tupo mpakani mwa nchi mbili (Zambia na DRC) ni vema tukavihakikisha vijiji vyetu na wenye maeneo kuwa na hatimiliki. Ni vema ukawekwa kipaumbele kwa mikoa ya pembezoni inayopakana na nchi mbalimbali, kupimiwa ardhi yao na kuipanga, kuepukana na migogoro ya ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuona umuhimu wa kupatiwa kibali cha kuajiri Maafisa Ardhi wa kutosha kwenye Halmashauri na vitendea kazi kulingana na mahitaji ya nchi kwa hii bidhaa adimu ya ardhi, kwa kila sekta. Ni vema Wizara ikaweka malengo ya utekelezaji kwenye Halmashauri na kufuatiliwa na kutathminiwa ili kila mmoja aweze kuwajibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii, bado napenda kuikumbusha Serikali kupitia Wizara hii kumaliza kulipa fidia Kurasini. Tathmini imefanywa muda mrefu lakini hadi leo wananchi wale hawajalipwa fidia hiyo pamoja na mapunjo yao. Fidia inapokaa muda mrefu huleta matatizo kwa raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri awahimize *NHC* kuharakisha makubaliano yetu ya kujenga jengo la biashara ya fenicha pale Keko.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na wimbi kubwa sana la migogoro ya ardhi hapa nchini; migogoro ya wakulima na wafugaji na migogoro hii inasababishwa na wawekezaji hasa maeneo ya hifadhi

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni Kata ya Kyanyari, wananchi wanateseka sana wamefukuzwa kwenye makazi yao kwa lengo la Serikali eti kupisha hifadhi. Wananchi hawa toka wamefukuzwa wanahangaika sana hadi sasa hawana makazi maalum ya kuishi na hawana matumaini ya maisha yao, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha inawapa makazi ya kuishi wananchi hawa pamoja na mashamba (maeneo) kwa sababu maeneo waliyofukuzwa ndiyo yaliyokuwa yanawasaidia kwa makazi pamoja na mashamba lakini kwa sasa hawana sehemu ya kulima na wananchi hawa walitegemea sana kilimo ili kuinua kipato cha maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwaondoa kwenye maeneo yao kumewaathiri sana wananchi wa Kata ya Kyanyari wanateseka na kutia huruma. Napende kuishauri Serikali iwe inawatengea maeneo mbadala kabla ya kuwahamisha wananchi kwa lengo la kupisha hifadhi tofauti na sasa kuwahamisha wananchi bila kuwatengea maeneo kwani wanapowaondoa bila kuwatengea maeneo wanategemea wananchi hao watakwenda wapi? Pia Halmashauri husika ihakikishe inasimamia na kutetea haki ya wananchi wake katika maeneo husika.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mezani. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Waziri pamoja na Makamu wake, ninayo machache ya kushauri upimaji wa ardhi yote ya Tanzania ambayo ni 950,000 *square kilometres*, matumizi yake yajulikane na vile vile wamiliki halali wajulikane na kudhibiti wageni kumiliki ardhi nchini mwetu. Maeneo ya mlimani Usa Arusha kuna mashamba makubwa, mengine yana farasi kwa ajili ya burudani. Je, wenyewe hawa ni wamiliki halali? Je, matumizi yake ndiyo yaliyokubaliwa na Wizara au Kituo cha Uwekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itumie sekta binafsi katika upimaji na kupanga matumizi ya ardhi, kwa sababu wataalam Serikalini hawatoshi, vinginevyo itachukua miaka mingi sana zoezi hilo kukamilika. Serikali isitumie udhaifu wake kuumiza wananchi kwa mujibu wa sheria na kanuni. Kodi hulipwa kufuatana na eneo na matumizi ya ardhi, haiyumkiniki kusikia Tamko la Waziri kwamba, kodi italipwa kwa maeneo yote ambayo hayajapimwa. Je ni kosa la nani kwamba ardhi hiyo haijapimwa? Je, kodi hiyo italipwa kwa kigezo gani? Hakuna mtu wala taasisi iliyo juu ya sheria. Serikali yenyewe ndio imetunga Sheria ya Ardhi na lazima izingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba kuna *improvement* kwenye mchakato wa kupata hati miliki ya ardhi, bado juhudii zaidi inahitajika, bado kuna watumishi wanaojivuta. Napendekeza utoaji hati miliki zisizo na migogoro kwa wakati kiwe kigezo cha kupima utendaji wa watumishi wanaohusika na utoaji wa hati miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali sasa ifanye maamuzi magumu ya kutatua kero ya migogoro ya ardhi iliyodumu kwa miaka mingi Serikali sasa iepuke kukwepa kufanya maamuzi ya kero hii kwa kuunda Tume na Kamati za kutoa mapendekezo miaka nenda, miaka rudi. Pamekuwepo na Kamati/Tume zaidi ya tatu na bado migogoro hii haijapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na fursa ya kuchangia leo. Nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na timu yake ya wataalam kwa kazi nzuri sana waliyofanya. Naomba masuala machache yafanyike ili kuboresha huduma ya Wizara ya Ardhi inayoendana na maendeleo ya makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza jimboni kwangu, Serikali iharakishe kupitia mgogoro wa ardhi ya miaka mingi

iliyotutesa na kusababisha migogoro hii kutumika kisiasa wakati wote. Migogoro ya Vijiji vya Ayamango, Gedamar na Gidejabong na *TANAPA* Tarangire, Serikali ndio iliweka vijiji hivyo hapo katika eneo la hifadhi. Wapatiwe eneo mbadala na pia shamba la Galapo *Estate* pia lisitolewe viwanja na badala yake iwe eneo la kuwapa hao wanaondolewa katika hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba suala la mashamba ya Bonde la Kisumu, migogoro ya ekari 25. Tunaomba pale mapendekezo ya Wilaya na Mkoa zifanyiwe kazi pia Serikali itoe tamko la kuvamia mashamba na kuharibu mali ya wawekezaji ambayo wana haki na wanatimiza wajibu kisheria. Pia tunaomba ardhi ya kilimo ilindwe kisheria ili matumizi ya ardhi ya kilimo isiweze kubadilishwa bila Bunge kupitisha mabadiliko hayo kuwa ya makazi, viwanda au matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba Wizara iandae *program* ya kila Halmashauri kupata vifaa vya kupima kwa mkopo pamoja na vifaa vya kuweka kumbukumbu ya hati na vifaa vya kuchapa hati. Kwanza tutaweza kulipa ndani ya muda mfupi. Leo Halmashauri nyingi hawana bajeti ya kununua kwa fedha taslim.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba Wizara ya Ardhi iangalie namna ya kulipia gharama ya matumizi ya *satellite*. Hii itafanya upimaji kwa ramani iliyopo inakuwa bora na wa uhakika. Leo hii ramani nyingi zina tatizo sababu hawana fursa ya kutumia hiyo huduma ya *satellite*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pia tuwe na sheria ya kuzuia kuza kiholela kwa ardhi hasa yenye hati ya kimila ili wenye uwezo wasinunue ardhi nyingi na wasiokuwa na uwezo kukubali kuwa vibarua na mbele ya safari tutakuwa na hatari sawa na Afrika Kusini na nchi zingine kama Kenya ya wachache kuwa na ardhi. Leo kila Mtanzania ana uwezo wa kuwa na ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba Serikali itumie fursa hii kutoa tamko kwa umma na sisi wanasiasa kutumia ardhi kisiasa na kuhamasisha vurugu kwa maslahi ya kisiasa na hasara kwa umma na wamiliki wa ardhi, hifadhi mbalimbali na vyanzo nya maji.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wachangiaji wenzangu kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, kwa kuchapa kazi ya kusimamia Wizara hii na kupunguza migogoro ya ardhi nchini na migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia migogoro ya mipaka ya vijiji na hifadhi, natambua Mheshimiwa Waziri ni mzoefu wa kupunguza migogoro ya ardhi na kwa kuwa migogoro ya hifadhi na vijiji vilivyo sajiliwa vinamgusa kwenye Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana tena sana Mheshimiwa Waziri Lukuvi tushirikiane kwa ukamilifu sana na Wizara ya Maliasili na Utalii na TAMISEMI ili basi mgogoro wa hifadhi na Vijiji nya Sibwesa na Kalilani, unaweza kutatuliwa na kwisha ili basi wananchi na hifadhi wenyewe waweze kufanya shughuli za kimaendeleo na kufanya mahusiano ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa watumishi wa ardhi; niombe kwa Mheshimiwa Waziri akipata watumishi wa ardhi, basi atukumbuke Halmashauri ya Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la *NHC*, kwanza nimpongeze Mtendaji Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa Tanzania (*NHC*). Kwa kuchapa kazi na kwa kasi kubwa anayofanya ya kuwajengea Watanzania nyumba za bei ya kati ambayo Watanzania wengine wamemudu kununua. Rai yangu katika hili tuombe *NHC* nao waweze kutoa fursa kwa Watanzania kulipa asilimia 10 na baadaye walipe kila mwezi hadi hapo mkataba utapokwisha ndio wapewe Hatimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya kulipa asilimia 10 halafu zilizobaki mtu alipe ndani ya miezi mitatu kwa kweli inatunyima fursa Watanzania wengi kuweza kununua nyumba hizi na wadau ni wengi, mtu anaweza kuwa na nyumba Dar es Salaam akapenda kuwa na nyumba pia Arusha, lakini kwa utaratibu wa kulipa 10% halafu miezi mitatu awe amemaliza kwa kuchukua mkopo Benki, hili ni gumu. Sababu ni kwamba, wapo Watanzania tayari wana mikopo mingine benki ya biashara, sasa akichukua mkopo benki kwa ajili ya kununulia nyumba mikopo inakuwa mingi inamzidua. Hivyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, aone namna ya kuchukua mfumo wa *NSSF* mtu analipa *downpayment* ya miezi mitatu kisha kila mwezi analipa pango hadi amalize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe pia Mheshimiwa Waziri, *NHC* waje Uvinza kutujengea nyumba za bei za kati na bei za nafuu katika ukanda wa Ziwa Tanganyika. Ziwa hili lina mandhari nzuri sana na viwanja tunavyo. Sambamba na hili tunaomba pia waje kujenga Uvinza, viwanja vikubwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizi tunavyo na huku kwa vile ni Wilaya mpya watumishi wengi wa Serikali na Taasisi mbalimbali hawana nyumba za kuishi, hivyo tunawakaribisha *NHC* kuja kujenga nyumba za bei nafuu na kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye Wizara. Naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuwa na afya njema na kushiriki katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge la Bajeti. Nampongeza Mheshimiwa Job Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson; Wenyeviti wa Bunge, Katibu wa Bunge Dkt. Kashililah , pamoja na watendaji wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake; Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan; Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kasim Majaliwa pamoja na Baraza lote la Mawaziri, kwa kazi kubwa wanayofanya katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana tena sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi; Naibu Waziri, Mheshimiwa Angelina Mabula pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa na nzuri sana ya kuendelea kutatua mgogoro ya ardhi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ziara allyoifanya Naibu Waziri Mheshimiwa Angelina Mabula katika Mkao wa Iringa na kutatua mgogoro uliokuwepo kati ya Manispaa na wananchi waliopo kwa maeneo walionunua kwenye Serikali ya Kijiji cha Igumbilo, Kata ya Igumbilo. Nashukuru sana mgogoro uliokuwepo unaelekea kumalizika kwa maelekezo sahihi aliyojatoa au kuagiza Manispaa itekeleze, wananchi wamepatiwa viwanja katika maeneo yao, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Angelina Mabula. Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wetu wa Iringa unaendelea kupanuka kwa majengo pamoja na idadi ya watu kuongeza bado ujenzi holela nao unaongezeka, nimwombe Mheshimiwa Waziri, Ndugu yangu Lukuvi atusaidie kupunguza eneo la mipaka ya Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuzirudisha nyumba za *National Housing* Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maeneo ya mipaka lipo katika maeneo mengi hasa mipaka ya Mbulu na Iramba; Manyara na Karatu; na Mbulu na Hanang. Tunaomba wapimaji waje kutatua na kusoma (*GN*) ili wananchi wajue wanapotakiwa kuwajibika kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la mgogoro wa ardhi Yayedha Chini na mwekezaji aliyepora eneo la wananchi bila kupewa na Serikali ekari 3903. Mara nyingi Serikali hukubali kutoa eneo kwa wingi wa wananchi kusema apewe, lakini Wahadzabe, Wabarbaig mara nyingi jamii hizi hazijapewa elimu kuhusu ardhi, hivyo panapotoka mtu mmoja kuwadanganya wanaweza kutoa eneo hilo na baadaye mgogoro hautakwisha. Sasa kwa kuwa Wahadzabe ambao mara nyingi wana hamahama kutafuta matunda na asali pia wanahitaji ardhi hiyo na kwa bahati mbaya wapo wachache katika jamii. Ushauri wangu ni kwamba, wakati mwingine haki ya wachache izingatiwe ili jamii isipate tabu.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi nchini ni moja ya kero kubwa inayokwamisha maendeleo ya kiuchumi na ya watu wetu. Migogoro hii imedumu muda mrefu na kama nchi lazima tunatakiwa kuchukua hatua sasa. Ili kumaliza migogoro hii Serikali ni lazima ihakikishe ardhi yote imepangwa, imepimwa na kumilikishwa kisheria. Kuhusu migogoro ya mipaka kati ya Mkoa na Mkoa, Wilaya na Wilaya na Kijiji na Kijiji, nishauri Serikali kufanya utaratibu wa kutafsiri *GN* zilizounda maneno hayo ili haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karatu inayo mashamba 40 ya wawekezaji (Mikataba). Mengi ya mashamba hayo hayajaendelezwa kwa kiwango cha kuridhisha na yamekuwa chanzo cha migogoro. Shamba la Tembo na Tembe lenye ekari 562 na 545 ambayo yote yametekelvezwa kwa chini ya 50% yamekuwa kero kubwa katika Wilaya ya Karatu. Naomba Serikali ichukue hatua ya kuyachukua mashamba hayo au hata sehemu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba la *Acacia Hill*, lenye ekari 1556, nalo tunaomba sehemu yake irudishwe kwa wananchi maana nalo limeendelezwa kwa chini ya asilimia 50%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba la Bendhu *Limited* lenye ekari 472 limetelekezwa baada ya mmiliki wake kufariki. Tayari Halmashauri ya Wilaya imeshaomba shamba hilo kufutiwa umiliki na lipewe wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niiombe Wizara iongeze wataalam wa ardhi na vifaa katika Wilaya ya Karatu.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika suala hilli. Kwa sababu ya muda naomba nianze kumpongeza Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi na Naibu wake Mheshimiwa Angelina Mabula, pamoja na wataalam wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya kukabiliana na changamoto mbalimbali za ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu wa Kijiji cha Lukonde wana matatizo makubwa, wanapata kipigo kutoka kwa mwekezaji wa Shamba la Kidago alilopata kwa njia ambazo sio halali toka Uluguru *Toller* aliywanyang'anya wananchi bila ya kufuata taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro huu ni mkubwa sana kwa Kijiji na Kitongoji cha Kidago, Lukonde, nyumba zao zaidi ya sitini (60) zimechomwa moto zaidi ya mara tatu tofauti na kwa miaka tofauti na kuchoma mazao yao na mfugaji huyo aliyepewa ardhi hiyo. Ombi langu, Mheshimiwa Waziri baada ya Bunge hili kumalizika naomba afike kidogo na kujiona hali halisi na kuwasaidia wananchi hawa ili waweze kuishi katika nchi yao kwa amani na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka kushauri Serikali kutenga Bajeti na kupima ardhi yote ya Halmashauri ya Morogoro Vijijini. Kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora

ya ardhi, kupanga matumizi ya ardhi kwa ajili ya wakulima na wafugaji na hifadhi na kujenga miundombinu ya kiufugaji kama majosho, mabwawa katika maeneo ya wafugaji na kutoa elimu kwa wafugaji kufuga kisasa na umuhimu wa kuwa na mifugo kutokana na ukubwa wa ardhi walijonayo na miundombinu ya mifugo iliyopo sehemu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwaondoa wafugaji wavamizi waliokuja Morogoro vijjini na Morogoro kwa ujumla bila kufuata sheria Kanuni na taratibu za kuhamisha mifugo toka sehemu moja kwenda sehemu nyingine na kuharibu mazingira, mashamba ya wakulima, vyanzo vyaa maji na barabara zetu tulizojenga kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.  
Ahsante.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kunijaalia kuchangia. Naunga mkono Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani na pia nawapongeze Mawaziri kwa kazi .

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni kwamba, hapo zamani za kale Tanzania hapakuwepo na migogoro ya ardhi hususan ya wakulima na wafugaji, lakini siku za karibuni migogoro ipo kila kona ya Tanzania. Sababu kubwa watu wamejua thamani ya ardhi kuwa ni mali. Ardhi ni rasilimali muhimu ambayo pia ni urithi na utajiri wa asili toka kwa Mwenyezi Mungu. Naishauri Serikali, ardhi yetu ipimwe, ipangiliwe isiwe nchi nzima ni viwanda, barabara, makazi na maeneo ya vijjini tu ndio mashamba. Ardhi ipimwe na imilikiwe na wananchi kama ilivyo kwa South Africa, Kenya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashamba ya Mkonge (*Amboni Company Limited*). Halmashauri ya Jiji la Tanga lina mashamba makubwa ya Mkonge ya Amboni *Company Limited*sasa (*COTAIL*) ambayo imechukua nafasi ya Amboni

*Limited.* Naipongeza Kampuni ya *Cotall Limited* kwa kuipa Halmashauri ya Jiji la Tanga ardhii kwa ajili ya shughuli za maendeleo yenyewe ukubwa wa takriban heka 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamejitokeza matatizo baada ya Halmashauri kupata mwekezaji wa China anayetaka kujenga Kiwanda cha *Cement*. Kuna wakulima ambao wanalamiko kuwa wamepunjwa fidia, hivyo naomba, Mheshimiwa Waziri tukatembelee eneo husika ili kutatua kero ndogo ndogo na kuweza kufanya mradi mkubwa wa Kiwanda cha *Cement* uanze bila malalamiko ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashamba ya Marungu na Kwamkembe. Sheria inaelekeza kuwa majiji hayana mashamba yenyewe zaidi ya 50 *hectors*, lakini Jiji la Tanga katika Kata ya Marungu kuna mashamba tajwa hapo juu ambalo siku za karibuni wameuziwa na wamiliki wenye Hatimiliki, wameondoa wananchi waliokuwa wakulima mazao ya chakula na biashara, yaliyowezesha kupata kipato cha kila siku na kulipia ada za watoto. Waliahidi kuwakatia wakulima baadhi ya maeneo kwa ajili ya kilimo (mashamba yana zaidi ya ekari 2000 – 4000). Namwomba Mheshimiwa Waziri hili pia alishughulikie na kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha miaka 21-Tanga. Hili ni eneo lilitwaliwa kinyume na taratibu. Nashauri, Mheshimiwa Waziri, Ofisi yake ilirudishe Halmashauri ya Manispaa ya watu wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Ngamiani Kusini Kati na Kaskazini. Eneo hili ni katikati ya mji kuanzia Barabara 1-21, kuna nyumba zaidi 10,000 na ni eneo la kihistoria lakini wamiliki wake hawana hatimiliki wana Hati ndogo (*offers*) tu. Ushauri, naomba Wizara ya Ardhi isaidie katika kupima au kutoa Hatimiliki (99 years) ili wananchi waweze kutumia katika shughuli za maendeleo kama kukopa mabenki kwa ajili ya biashara na kilimo. Tukumbuke wananchi hawa wanalipa *property tax*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu 30% ya makusanyo, naiomba Wizara irudishe 30% ya mapato ya ardhi katika Halmashauri ili zitumike kwa shughuli za Maendeleo.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa jitihada kubwa walizofanya kuleta mabadiliko makubwa ya kiutendaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali ardhi ina umuhimu wa kipekee kwa uhai wa maendeleo ya binadamu, wanyama, mimea na viumbe vyote. Kwa uchumi wa Taifa letu ambalo wananchi walio wengi wanategemea sana kilimo kama sekta muhimu katika kukidhi mahitaji yao ya kila siku; rasilimali ardhi inakuwa na umuhimu wa kipekee, kiasi kwamba ni haki ya kila mwananchi kupata, kuimiliki, kuitumia na kuitunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wimbi la kuwepo kwa migogoro ya mipaka na uvamizi wa ardhi katika maeneo ya viji ni limeendelea kuwa tatizo kubwa katika nchi yetu. Tatizo hili ni kikwazo kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Tumeendelea kushuhudia migogoro hii ikisababisha upotevu wa mali za wananchi, vifo na kuendeleza uhasama kati ya jamii na jamii na hivyo kuwafanya wananchi kubaki maskini na kuishi maisha duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ndogo ya upimaji ardhi imeendelea kuwa donda ndugu, wataalam wa ardhi kutowashirikisha wananchi wakati wa uwekaji wa mipaka; na kutowaelimisha wananchi juu ya mipaka iliyowekwa, kama Taifa hatuwezi kuiacha hali hii iendelee. Wizara ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kuwa wataalam wa ardhi wanawashirikisha na kuwaelimisha wananchi wakati wa uwekaji wa mipaka. Wizara iongeze kasi ya upimaji wakati wa uwekaji wa mipaka. Wizara iongeze kasi ya upimaji ardhi ili kuzuia wajanja wachache kuvamia maeneo pasipo viongozi wa viji kujua na hatua kali zichukuliwe kwa viongozi wa viji wanaogawa ardhi kinyume na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wakulima na wafugaji imeendelea kuwa chanzo cha machafuko na umwagaji damu nchini. Lazima kasi yetu ya kutenga maeneo maalum ya wafugaji na wakulima iandamane na utunzaji wa sheria kali utakaozuia uvamizi wa maeneo unaofanywa na pande hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, bado mashamba makubwa yasiyoendeleza yameendelea kuwa chanzo kikubwa cha migogoro ya ardhi nchini. Bado mfumo wetu wa kufuta miliki ya ardhi isiyotumika ipasavyo kwa mujibu wa makusudio ya umiliki wa ardhi husika umeendelea kutoa mwanya wa watu wachache kuhodhi ardhi bila kuitumia na kuwaacha wananchi wengi wakitaabika kwa kukosa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kufanya mapitio ya Sheria ya Umiliki Ardhi na kanuni zake ili tupunguze urasimu katika mfumo wetu ili mashamba yaliyotelekezwa yaweze kufutiwa hati za umiliki mara tu yanapothibitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine nilete kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Wilaya ya Mkinga, ambayo ni mionganini mwa wilaya zinazokabiliwa na migogoro ya umiliki wa ardhi na mashamba yaliyotelekezwa kwa muda mrefu. Licha ya jitihada kadhaa ambazo kwa nyakati tofauti Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkinga na mimi binafsi tumewasilisha Wizara ya Ardhi mapendekezo ya Wilaya kuhusu utatuzi wa migogoro hiyo; bado utatuzi wa migogoro hii umekwama kupata majawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mapendekezo ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkinga yaliwasilishwa Wizara ya Ardhi tangu mapema mwaka 2007 wakati huo Mkinga ikiwa bado ni sehemu ya Wilaya ya Muheza; ofisi yangu iliwasilishwa tena maombi hayo kupitia mchango wangu wa maandishi wakati wa Bunge la Bajeti mwaka jana na kufuatiwa na barua kwa Waziri wa Ardhi yenyewe Kumb. Na. MB/MKN/Ardh 01/2016 ya tarehe 30 Mei, 2016. Napenda

kuikumbusha Wizara juu ya maombi haya ambayo kimsingi yamechukua muda mrefu kupatiwa ufumbuzi.

(i) Shamba la Kilulu; shamba hili ndipo palipojengwa Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga. Shamba hili kwa mara ya kwanza lilimilishwa kwa Bwana Van Brandis na Bibi Mary Van Brandis hadi tarehe 31 Oktoba, 1959 ambapo umiliki ulihamia kwenda ama Bwana Akberali Walli Jiwa. Mmiliki huyu hakuendeleza shamba hili lenye ukubwa wa ekari 5,699.9 hadi umiliki wake ukafutwa mwaka 1972. Baada ya kufuta umiliki, Serikali illipa fidia na shamba likawa chini ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye Wilaya ya Muheza ilipokea maombi ya kumilikishwa shamba hilo toka Kampuni ya *M/S Arusha Farms Limited (CHAVDA)*. Taratibu zote zillizofanyika na alimilikishwa ekari 2,699.9 na ekari 3,000 walipewa wananchi wa vijiji jirani vya Vuo, Mwachala na Parungu Kasera waliokuwa na shida ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *M/S Arusha Farms Limited* walipewa barua ya toleo (*Letter of Right of Occupancy*) ya tarehe 10 Mei, 1991 ambayo ilisajiliwa na Msajili wa hati tarehe 10 Mei, 1991 ambayo ilisajiliwa na Msajili wa hati tarehe 13 Mei, 1990 kwa *Land Office Number 125127*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmiliki huyu aliomba mkopo kutoka *CRDB Bank* kwa kuweka rehani barua ya toleo. Aidha, alishindwa kurejesha mkopo huo na *CRDB* waliuza shamba kwa *M/S Mbegu Technologies Limited* tarehe 27 Juni, 2004 ambao walilipa mkopo huo. Hata hivyo, pia hakuweza kuliendeleza shamba hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwana Akberali Jiwa licha ya kunyang'anya shamba hilo na kulipwa fidia aliwasilisha ombi lake la kurejeshewa umiliki wa shamba hilo. Ombi lake liliwasilishwa katika Kikao cha Kamati ya Kugawa Ardhi tarehe 10 Oktoba, 1996 na iliazimiwa liwasilishwe katika Kamati ya Ushauri wa Ardhi Mkoa. Kamati hiyo chini ya Uenyeviti wa

Mkuu wa Mkoa iliridhia Bwana Akberali Jiwa apewe shamba hilo kwa vile *M/S Arusha Farms Limited* ameshindwa kuliendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Muheza ilitoa barua ya toleo kwa miliki ya miaka 99 kuanzia tarehe 1 Oktoba, 1998 kwa Akberali Jiwa kwa jina la Kampuni ya Kilulu (2000) *Limited*. Baada ya tatizo hilo la *double allocation* kujitekeza, Halmashauri ya Muheza iliandika barua Kumb. Na. MUDF/3844/63 ya tarehe 2 Aprili, 2007 kwenda kwa Kamishna wa Ardhi kwa ajili ya kuomba kufuta miliki hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, licha ya ufuatilaji uliofanywa wa mara kwa mara, kwa mujibu wa taarifa ya Halmashauri hadi leo Halmashauri haijapata hati yoyote inayoonesha kufutwa milki ya shamba tajwa. Kikao cha *RCC* kilichofanyika mwaka jana kiliridhia hati ya shamba tajwa ifutwe; hivyo kuagiza taratibu za kutoa *notice* zifanyike. Hata hivyo, tangu wakati huo kumekuwa na urasimu mkubwa wa utoaji *notice* tajwa. Naiomba Wizara ifuatilie jambo hili.

(ii) Shamba la Moa; shamba hili lina ukubwa wa ekari 15,739.60 na linamilikiwa na Mkomazi *Plantations Limited* wa S.L.P. 2520 Dar es Salaam kwa hati Na. 4268,9780 & 9781. Halmashauri ya Wilaya ilituma notisi ya kuwafutia hati miliki yao kwa kutoendeleza na kutolipia kodi. Baada ya hapo Halmashauri ya Wilaya iliwasilisha barua ya Mapendekezo kwa Kamishna wa Ardhi yenyе Kumb. Na MKG/LD/F/2/54 ya tarehe 28 Julai, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za ufutaji hati miliki ziliendelea Wizarani, lakini Halmashauri ilipokea barua ya mmiliki akieleza kuwa jina la umiliki lilibadilika na kuwa *Moa Plantation & Aquaculture* wa S.L.P. 364 Dar es Salaam na kwamba wanataka kuendeleza shamba hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ilishawasilisha Wizarani barua ya mapendekezo ya kufuta hati miliki, ililazimika kumwandikia Kamishna wa Ardhi

barua yenye Kumb. Na. MKG/LD/F/2/56 ya tarehe 9 Juni, 2011 kumweleza kupokea barua hiyo na kwamba shamba hilo lina vijiji vinne ambavyo vimeanzishwa na kusajiliwa (Moa, Ndumbani, Mayomboni na Mhandakini).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, vijiji hivyo tayari vina huduma za jamii kama shule, zahanati, barabara na kadhalika katika maeneo hayo; hivyo aendelee na taratibu za ufutaji hati miliki au kama atasitisha ufutaji basi wamiliki wakubali kumega maeneo yanayokaliwa na vijiji na kuendelezwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati hali ikiwa hivyo, mwaka 2013 mmiliki wa shamba atengeneze *PP*na kuomba kubadilisha matumizi ya sehemu ya shamba ili kupima viwanja 450 vya makazi. Hata hivyo, viwanja hivyo havikuwahi kupimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatilia ucheleweshaji usioeleweka wa kufuta hati ya shamba hili, mnamo mwezi Oktoba, 2016 mmiliki wa shamba alitumia mwanya huo kutengeneza *PP*nyingine ya eneo lote la shamba ili kupima viwanja. Aidha, amekabidhi hati ya shamba tajwa ili ipelekwe kwa Afisa Ardhi Mteule-Moshi ili taratibu zinazokusudiwa ziweze kufanywa. Naiomba Wizara iingilie kati mchakato huu ili ardhi tajwa irejeshwe mikononi mwa Halmashauri ya Wilaya.

(iii) Mwele Seed Farm; shamba hili lina ikubwa wa hekta 954. Mmiliki ni Wizara ya Kilimo. Wakati ambapo shamba hili lilikusudiwa kuwa shamba la kuzalisha mbegu, hali halisi ni kwamba kwa kipindi cha takribani miaka 15 sasa shamba hili limeshindwa kutumika kama ilivyokusudiwa na sehemu kubwa kubaki kuwa pori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba hili Mbambakofi, Maramba A, Maramba B na Lugongo ndio wamekuwa nguvukazi ya

kulifanyia usafi shamba hili pale wanaporuhusiwa kufungua mashamba mapya na kulima mazao ya muda mfupi kila msimu mpya wa kilimo unapowadia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 21 Septemba, 2007, Halmashauri ya Wilaya ililandika barua kwa Kamishna wa Ardhi Kumb. Na. *MUD/ASF/VOL. VI/35* ikipendekeza kumegwa kwa shamba hili na kugawiwa kwa wananchi wa vijiji jirani kutokana na uendelezaji wake kuwa mdogo sana na kodi kutolipwa. Hata hivyo, maombi haya hayakuwahi kupatiwa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba hili lilipakana na Kijiji cha Mbambakofi chenyeh takriban kaya 500 zenye jumla ya wananchi wapatao 3173. Mbambakofi ni kijiji pekee katika Wilaya ya Mkinga ambacho kimekosa hata eneo la kujenga huduma muhimu za kijamii kama shule ya msingi na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, shamba hili limepakana na Mji Mdogo wa Maramba ambao unakua kwa kasi kubwa, ukiwa na takriban watu 30,000 na kuzungukwa na mashamba makubwa ya Maramba JKT, hekta 2,445; Lugongo Estate, hekta 6,040; Kauzeni Estate, hekta 189.66; na Mtapwa Estate, hekta 476.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kutekelezwa kwa shamba hili imezidi kuwa mbaya sana sasa kuliko ilivyokuwa mwaka 2007, wakati Halmashauri ya Wilaya ilipoomba kwa mara ya kwanza kumegwa kwa shamba hili. Kwa sasa hali imekuwa mbaya kiasi kwamba hata majengo mengi yaliyokuwepo yameanguka na machache yaliyosalia yamekuwa magofu, mashine na mitambo yote ya kilimo iliyokuwepo shambani hapo imeharibika na michache iliyoosalia imehamishiwa Morogoro. Kwa sasa shamba limebakini na wafanyakazi wasiozidi watatu kutoka ishirini na vibarua thelathini waliokuwepo miaka ya 1988 – 1995.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Halmashauri ya Wilaya kusubiri kwa muda mrefu jibu la Kamishna wa Ardhi

bila mafanikio, kikao cha RCC kiliiagiza Halmashauri kuandaa maelezo kuhusiana na shamba hili ili Mkuu wa Mkoa aweze kuandikia Wizara husika kuomba rasmi Halmashauri kukabidhiwa eneo tajwa. Tayari Halmashauri imetekeleza maagizo haya. Naiomba Wizara ya Ardhi isaidie katika utatuzi wa kero hii ambayo inawasumbua sana wananchi.

(iv) Kwamtili Estate; shamba hili lina ukubwa wa hekta 1,150 na linamilikiwa na Kwamtili Estate Limited yenye *Certificate of Incorporation* Na. 2649 iliyosajiliwa tarehe 9 Januari, 1961 ikiwa na wanahisa wafuatao:-

S/N	JINA LA MWENYE HISIA	ANAPOISHI	MAELEZO
1	DENNIS Martin Fielder	4 Market Square Tenbery, Wells Worcestershire -UK	Amerudi Uingereza
2	National Agriculture & Food Corporation (NAFCO)	Box 903 Dar es Salaam	Shirika limefutwa
3	Handrick Tjails Scheen	Cl/30 Algamines Bank, Amsterdam, Netherland	Amefariki
4	Louis Van Wagenburg	Laycsan Ag Vaghel, Holland	Amefariki
5	Schoonmakers Bart Vandenburg	De Congqabsen, 163 Schikhher, Holland	Amefariki
6	Tracey Elan Allison	The Willos Terrigton, Herefordenshire, UK	Amefariki
7	Juvent Magoggo	42 Block S. Mikanjuni Box 5855 Tanga	Anaishi Tanga
8	W.J. Tame Ltd	Box 118 Tanga	Amefariki
9	Jacobus Cornelius Josephus Moris	Logtamburg Vaghel Holland	Amefariki

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba hili lililopo katika eneo la Kwamtili, Kata ya Bosha Wilaya ya Mkinga, lilitumika kwa kilimo cha kibashara cha zao la kakau. Hata hivyo, kwa muda wa miaka takriban 26 sasa shughuli za kilimo cha zao la kakau zimesimama baada ya iliyokuwa Menejimenti ya Kampuni chini ya Ndugu Dennis Fielder kutelekeza shamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, baada ya shamba kutelekezwa, mmoja wa wanahisa Ndugu Juvent Magoggo amekuwa akifanya shughuli ndogo ndogo ikiwemo kuvuna miti ndani ya shamba hili kwa lengo la kupata fedha za kufanya uzalishaji mdogo mdogo; na hali kadhalika kuruhusu wananchi wanaozunguka shamba hilo kulima mazao ambayo si ya kudumu. Hata hivyo, kwa sasa ndugu Magoggo ameshindwa kuendelea kufanya shughuli hizo baada ya kunyimwa vibali nya kuvuna miti kusafirisha magogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwepo kwa ombi la umiliki wa shamba hili, yamezuka makundi ya watu yanayodai kuwa na haki ya kumiliki shamba hili na hivyo kuwakodisha wananchi wanaozunguka shamba hili maeneo ya kulima kwa kuwalipisha sehemu ya mavuno yatokanayo na matumizi ya ardhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kumekuwa na wimbi la kujitokeza raia wa kigeni kwa kutumia kivuli cha aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa shamba na kulitekeleza Ndugu.Dennis Fielder kufanya uharibifu wa mali za kampuni, ikiwemo upasuaji wa mbao na kuanzishwa michakato ya kujimilikisha ardhi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, wananchi wanainyooshea kidole Ofisi ya Wakala wa Hifadhi ya Misitu, Wilaya ya Mkinga kutaka kujingiza katika kufanya udalali wa ardhi hii. Wananchi bado wanakumbukumbu nzuri ya jinsi watumishi hawa wa *TFC* Wilayani Mkinga walivyotumika kuwezesha mwekezaji wa Kiitaliano aliyejaribu kupatiwa ardhi ya Mkinga takriban hekta 25,000 kinyume na taratibu ili kulima *Jatropher*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali haijaweza kulipatia ufumbuzi tatizo lingine ambalo kimsingi limeanzishwa na *TFC* kutaka kupora ardhi ya wananchi katika shamba la Segoma, *TFC* hiyo hiyo inataka kuzalisha mgogoro mwagine wa kupora ardhi nyingine katika Wilaya ya Mkinga.

Hatupo tayari kuona hili likitokea hasa ikizingatiwa kuwa Kwamtili inakabiliwa na tatizo kubwa la ardhi. Tunaiomba Serikali kutumia busara kuacha jambo hili na kuirejesha ardhi hii kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kwamtili na Kata ya Bosha kwa ujumla wamebaki katika umaskini wa kutupa baada ya shughuli za kilimo cha kakau katika shamba la Kwamtili ambacho ndicho kilitoa ajira kwao kusitishwa. Nusura pekee kwa wananchi hawa ni kupatiwa maeneo katika shamba hili ili kwa kutumia utaratibu wa wakulima wadogo wawze kufanya shughuli ya kilimo na hivyo kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ifanye uamuza wa kufuta hati ya shamba la Kwamtili na kisha kuligawa kwa wananchi kwa ajili ya kilimo na sehemu nyingine kwa wananchi kuwa hifadhi ya msitu wa kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua changamoto kubwa inayowakabili wananchi wa Kwamtili, *RCC* iliagiza mmiliki wa shamba hili kupewa *notice* ili taratibu za kufutiwa hati ziweze kufanyika. Kwa masikitiko makubwa kumekuwa na urasimu mkubwa wa taratibu wa kutolewa *notice* tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Afisa Ardhi Mteule toka Ofisi ya Kanda-Moshi kuja Mkinga kufanya zoezi la uhakiki mwanzoni mwa mwezi Aprili hadi leo hakuna kinachoendelea licha ya kukumbushwa mara kadhaa kwa simu na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Mkinga. Naiomba Wizara iingilie kati jambo hili ili ujanja ujanja usitumike kuvuruga mchakato wa kuwapatia haki wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja. Aidha, naomba Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na TAMISEMI itusaidie Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga tuweze kuajiri Afisa Ardhi Mteule ili atusaidie kuondoa migogoro.

**MWENYEKITI:** Tumemaliza wachangiaji upande wa Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi kwa dakika 40 na baadaye Mtoa Hoja atakuu kumalizia kwa dakika 10.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO**

**YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa fursa hii ambayo amenipa na kunipa afya njema na hatimaye kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu na kuweza kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba nichukue fursa hii kutoa pole kwa wananchi wa Mkoa wa Mwanza na mikoa ya jirani ambao jana wamepatwa na tetemeko na hususan Jimbo langu ambalo karibu Kata saba zote zimepitiwa na tetemeko hilo. Tunamshukuru Mungu kwamba madhara hayakuwa makubwa sana na tunamwomba Mungu amrehemu yule Askari ambaye amepoteza maisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge hili kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya na mmekuwa mkituongoza vizuri katika shughuli nzima ya kuendesha Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati yetu pamoja na Makamu wake ambao wamekuwa wakitupa ushauri kupitia Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambayo tumekuwa tukifanyanao kazi vizuri. Namshukuru sana pia Waziri Kivuli ambaye naye amefanya kazi nzuri katika kuwasilisha hotuba yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nachukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Ilemela kwa kuniamini. Nashukuru Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini, lakini Serikali pamoja na Viongozi wa Dini ambao wamekuwa pamoja nasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naungana na wachangiaji wote waliotangulia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana ambayo anaifanya. Kwa kweli, amekuwa ni kiongozi wa mfano, kiongozi wa vitendo, kiongozi ambaye anasimamia kauli zake. Nasi wasaidizi wake tunasema tutakuwa tayari kumsaidia pale ambapo tunahitaji kusaidia kwa kadiri alivyotuamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wetu Mkuu pamoja na Makamu wa Rais. Kwa kweli wamekuwa wakitupa ushirikiano mzuri na kutupa maelekezo mazuri ya kuweza kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea pongezi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Naomba nichukue fursa hili kuwashukuru sana, lakini niseme pongezi hizo hazikutustahili sisi peke yetu, ni sisi pamoja na ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, ushirikiano mliotupa umefanya pia kazi yetu iwe rahisi. Kwa hiyo, nasi tunawashukuru sana. Maandiko yanasema, "*moyo usio na shukrani hukausha mema yote.*" Hivyo hatuna budi kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani na pongezi mlizozitoa, kwetu sisi ndani ya Wizara ni chachu ya kuzidi kuongeza kasi ya kutenda kazi vizuri na kuweza kusaidia jamii ambayo muda wote inategemea utendaji wetu. Nawashukuru sana pia Watendaji wetu ndani ya Wizara ambao wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana katika kuona kwamba, shughuli hizi zinafanyika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee kabisa, nimshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Lukuvi. Ni Waziri ambaye amekuwa ni *mentor* wangu mzuri, ni kiongozi ambaye anaweza kuelekeza vizuri, ni kiongozi ambaye anasimamia maamuzi, ni kiongozi ambaye kama ni mwanafunzi mzuri, kwa kweli utafuata nyayo. Mheshimiwa

Waziri nakushukuru sana kwa sababu umenifanya niwe kama nilivyo katika Wizara hii ambayo ina changamoto nyingi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa niseme kwamba Sekta ya Ardhi inakabiliwa na changamoto nyingi. Wote ni mashuhuda, tumeona namna ambavyo Waheshimiwa mmechangia katika kutoa hoja zenu. Katika michango yenu jumla ya Waheshimiwa Wabunge 77 wamechangia; 40 wamechangia kwa njia ya kuzungumza na 37 wametoa kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa ya michango ya Waheshimiwa Wabunge waliyooita, imejikita katika suala zima la utawala wa ardhi ambapo sehemu hii inahusu migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali wakiwemo wakulima, wafugaji, wawekezaji na hifadhi zetu ambazo zipo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna suala la kutolipwa kwa fidia kwa wakati kama ambavyo mmesema, lakini kuna ucheleweshwaji wa utoaji wa Hakimiliki za Ardhi. Yote haya yako katika utawala wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ambayo pia imezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana ni suala zima la upimaji na ramani. Katika maeneo haya limezungumziwa suala la uhaba wa wataalam wa upimaji na vitendea kazi, gharama kubwa za upimaji, umuhimu wa kuimarisha mipaka ya nchi, migogoro ya mipaka ya Vijiji, ya Kata, Wilaya kwa Wilaya, lakini pia migogoro kati ya wananchi kwenye vijiji pamoja na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mipango Miji, nako Waheshimiwa wengi wamezungumzia. Maeneo mengi waliyozungumzia upande huu walikuwa wakitoa kama ushauri; suala la kuharakisha zoezi la urasimishaji wa makazi katika miji mbalimbali ambalo tayari limekwishaanza; Waheshimiwa Wabunge wameishauri Wizara kuongeza kasi ya uaandaaji wa mipango kabambe, ushauri tumeupokea,

lakini pia limezungumziwa suala la uhaba wa watumishi na vitendea kazi katika Halmashauri mbalimbali. Tunakiri uhaba huo upo na ni kikwazo kikubwa katika kupanga miji yetu ili kuwa na miji salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lilirozungumziwa na Waheshimiwa Wabunge, ni la maendeleo ya nyumba. Hili limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana. Kubwa hapa lilizungumziwa kuhusu gharama kubwa za ujenzi wa nyumba kwa wananchi, imekuwa gharama ni kubwa kwa hiyo, vipato vyao ni vidogo na hawawezi kumudu kulingana na bei ambayo imewekwa na *National Housing*. Pia, mmezungumzia uhaba wa nyumba kwa watumishi katika maeneo hasa ya vijiji. Haya yote tumeyapokea kwa sababu ni michango; ni hali halisi ambayo ipo, lakini bado tutazungumzia majibu yake kwa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limezungumziwa ni suala la Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika Wilaya zetu. Upande huu umezungumziwa uhaba wa watumishi wa mabaraza katika Mabaraza yetu kwenye Wilaya, lakini pia mkazungumzia suala zima la azma ya Serikali ya kuwa na mabaraza haya katika kila wilaya. Ni kweli, hatujaweza kutimiza azma hiyo, lakini nia ya Serikali ni njema na tutaendelea kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa utangulizi wa maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyachangia, naomba sasa nianze kujibu hoja mbalimbali ambazo zimetolewa, nikianza na hoja kutoka kwenye Kamati yetu ya Bunge ya Kudumu ya Wizara ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambayo imetoa hoja mbalimbali. La kwanza amezungumzia ufinyu wa bajeti katika Tume yetu ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ambayo imekuwa ikipatiwa rasilimali kidogo kulingana na kazi wanazozifanya na ndivyo jinsi ambavyo mmeliona suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwahakikishie kwamba Serikali imekuwa inatoa fedha kulingana na bajeti inavyopata katika Tume ile. Kwa sasa Tume ile inalo Fungu

lake, inayo *Vote* yake Na. 3 ambayo sasa imeanza kutengewa bajeti kuanzia mwaka 2016. Mwanzoni ilikuwa iko ndani ya bajeti ya Wizara kwenye Fungu Na. 48, lakini kwa kasi ambayo yao na kazi wanayofanya, wameweza kufanya majukumu yao kulingana na pesa waliyopata na wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mafungu kadiri yatakavyozidi kuongezeka, tutawaongezea kwa sababu Tume hii ni muhimu sana katika kufanya shughuli za upangaji miji yetu katika maeneo yetu hasa katika mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kwa hiyo, niseme tu kwamba tumepokea maoni hayo na tutazidi kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha huu wa 2017/2018 Serikali imeipatia Tume vibali vya ajira kwa watu saba. Kwa sababu wakati mwengine pia utekelezaji wake haukuwa mzuri sana kwa sababu hawakuwa na *personnel* ya kutosha. Kwa hiyo, wataongeza wataalam wengine saba ambao ni kutoka katika kada mbalimbali kwenye eneo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali kupitia Wizara yangu itaendelea kuipatia Tume ushirikiano mzuri, hasa wa rasilimali fedha na watumishi pamoja na vitendea kazi ili waweze kufanya ile kazi ambayo wote tumeitambua kwamba ni muhimu, Tume hii ifanye kazi yake vizuri katika kusaidia katika mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala pia la kuongeza kasi ya elimu kwa umma kwa matumizi ya ardhi ambayo yameonekana kwamba kwa watumiaji mbalimbali imekuwa ni shida. Katika kutekeleza jambo hili, majukumu ya kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi, ngazi ya Kata na Vijiji, Tume hutoa elimu kwa timu za usimamizi wa ardhi kwenye vijiji na hususan katika Halmashauri. Hili limekuwa likifanyika na kumekuwa na ushirikiano mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, timu ya kusimamia mipango ya matumizi bora ya ardhi katika Wilaya hujengewa uwezo wa kuratibu na kupanga utekelezaji na usimamizi huu wa mipango ya matumizi bora ya ardhi nchini. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Tume ilitoa elimu katika Halmashauri 24 nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Tume imekuwa ikifanya kazi yake vizuri, pamoja na ufinyu wa bajeti ambao umekuwa ukitokea. Pia Tume hii huandaa vipindi maalum vyta elimu kwa umma. Hii yote ni katika kupanua uelewa katika maeneo yetu ili kusaidia kujenga uelewa wa pamoja. Imekuwa ikitumia njia mbalimbali ikiwemo kutumia vyombo vyta habari, maonesho ya Saba Saba, Nane Nane, Wiki ya Utumishi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanafanyika ili kuweza kupanua wigo wa kutoa elimu. Vipindi hivi pia vimekuwa vikihusisha sheria, taratibu na miongozo ya kupanga na kusimamia matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Elimu kwa Umma umeandaliwa kwa kushirikisha wadau wa matumizi ya ardhi kama Taasisi za Umma na Asasi Zisizo za Kiserikali. *Care International Tanzania, Haki Elimu, Ardhi Oxfarm na Ujamaa Community Resource Team*. Hawa wote wamekuwa wakishiriki katika zoezi hilo. Kwa hiyo, kazi inayofanyika ni nzuri kiasi kwamba ni kiasi cha kufuatilia tu zile programu zinapokuwepo ili watu waweze kujengewa uelewa mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine wamezungumzia kuwa Serikali itenye fedha za kutosha ili kuyafikia maeneo mengi zaidi nchini yenyeye migogoro ya mipaka ya ardhi. Katika suala hili Serikali itaendelea kutenga fedha kadri zinavyopatikana. Aidha, Wizara pia itaendelea kushirikiana na wadau wa Sekta binafsi ili kufikia maeneo mengi katika kutoa elimu na masuala ya ardhi ili kuepusha migogoro hii. Kwa hiyo, Serikali peke yake haiwezi, ndiyo

maana tunashirikisha sekta binafsi ambazo zipo katika taaluma hii ili kuweza kufikia wananchi wengi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa fedha pengine unakuwa nao ni kikwazo sana, lakini Serikali itaendelea kuishughulikia changamoto hii katika kuweza kupata rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imetoa ushauri katika mambo mengi na sisi tunayachukua na tumeyapokea kama yalivyo, wamezungumzia suala la Serikali ihamasishe Halmashauri kukopa ili kutekeleza miradi ya kupima viwanja. Hilo tumelipokea. Kuwezesha Bodi ya Mfuko wa Fidia ya Ardhi iweze kutekeleza majukumu yake tumelipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuhusu Wizara kuendelea kufanya kazi kwa pamoja na wadau wengine, tumelipokea na tunaendelea kulifanyia kazi; kuhusu Sheria ya Ardhi kwamba iboreshwe na kusimamiwa kikamilifu ili kuondoa migogoro baina ya watumiaji ardhi, huo ushauri tumeupokea, tunaendelea kuufanyia kazi; kuongeza kasi ya kutoa elimu nimesema tunaendelea, kwa hiyo, ushauri huo tumeupokea na tunaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba Serikali itenye fedha za kutosha kwa ajili ya kuanzisha Mabaraza ya Ardhi. Kama nilivyosema kwenye utangulizi, nia ya Serikali ni kuwa na mabaraza haya katika nchi nzima. Tuseme tu kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza ya Ardhi ya Na.2 ya mwaka 2002, kila Wilaya inatakiwa kuwa na Baraza. Lengo la Serikali ni kuwa na Mabaraza haya katika kila Wilaya. Hadi kufikia 15 Mei, 2017 Serikali tayari ilikuwa imeshaunda Mabaraza 97 kati ya yale Mabaraza 100 tuliyokuwa tumekusudia kuweka, ambapo kati ya hayo Mabaraza 53 tayari yanatoa huduma; na Mabaraza 44 hayajaanza. Kwa hiyo, nia ya Serikali ni njema na tunaendelea kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali inatarajia kuajiri watumishi 291 na kati ya hao, watumishi 98 ni ajira mpya katika Mabaraza. Kwa hiyo,

tuna imani tukishawapata hao, basi yale maeneo yote ambayo yana upungufu wa watumishi hao katika Sekta hiyo, watakuwa wamepata. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuwe na uvumilivu, Serikali ina nia njema na itaweza kufanya haya yote kadri ya muda unavyoruhusu na bajeti inavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilitolewa kwamba, Serikali iangalie namna ya kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba za *National Housing*. Hili zimezungumzwa na wachangiaji wengi, lakini Kamati pia imelizungumza. Naomba niseme kwamba Serikali imepokea ushauri huu, lakini pamoja na hayo Mheshimiwa Rais alishatolea maelekezo, kwa sababu wengi walilalamikia gharama kwamba zimekuwa kubwa. Tumekuwa tukilieleza siku zote kwamba pengine gharama kubwa inachangiwa na *National Housing* kufanya kila kitu wao wenyewe; kwa kuweka miundombinu ya barabara, maji na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hili tayari Mheshimiwa Rais ameshalitolea maelekezo kwamba Taasisi zinazohusika na huduma, kabla *National Housing* hawajaweza kufanya uwekezaji wao, basi kama ni barabara iwe imeenda, miundombinu ya umeme iwe imesogea na maji yawe yamekwenda. Wakiweza kusongeza huduma hizo, ni wazi gharama ya nyumba itapungua. Kwa hiyo, hili linafanyiwa kazi na Mheshimiwa Rais ameshalichukulia hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limefanyika hata kwenye hizi nyumba za lyumbu zinazojengwa sasa hivi hapa, tayari maelekezo yalishatolewa. Kwa hiyo, nina imani kwamba kwa sababu maelekezo yamekwenda katika Halmashauri zote katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge ambao mnataka kuwekeza katika maeneo yenu kwa kuwashirikisha *National Housing*, basi nadhani tukitekeleza hayo pia kwa itakuwa ni rahisi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *National Housing* wako tayari kwenda maeneo yote na siyo *National Housing* peke yake, hata *Watumishi Housing* ambao wanajenga nyumba

za watumishi nao wanahitaji kuwa na miundombinu hiyo hiyo ambayo inatakiwa kuwekezwa. Hii itapunguza sana gharama za nyumba ambazo tunazungumzia. Kwa hiyo, hili tumelichukua na Rais amelitolea agizo na litatekelezwa kadri ambavyo miradi itakavyozidi kuwekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilitaka Wizara ihakikishe Manispaa ya Dodoma inatekeleza dhima iliyokuwa ikifanywa na *CDA* na kupeleka huduma ya jamii ya miundombinu. Hii illkuwa ni hoja ya Kamati na walizungumzia lyumbu na nimeshaizungumzia. Kwa hiyo, suala la miundombinu limewekwa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo limezungumziwa, kuhusu kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mipango Miji kwani kuna changamoto nydingi. Niseme tu kwamba Sheria Na. 8 ya 2007 inazipa Halmashauri zetu za Wilaya na Miji pamoja na Manispaa mamlaka ya kupanga na kudhibiti uendelezaji wa miji. Wizara kama msimamizi mkuu, kwa Waraka wake Na.1 wa mwaka 2006 unaoelekeza taratibu za kufuata katika kubadili matumizi ya ardhi na mgawanyo wa viwanja na mashamba, hili linasimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Wizara ilitoa Waraka Na. 4 mwaka 2006 ambao unatoa maelekezo ya miongozo ya udhibiti ya undelezaji miji. Kwa hiyo, jukumu hili bado liko katika Halmashauri zetu kwa sababu sheria zipo. Tukiangalia tu Wizara peke yake tunaweza pengine tukachelewa kudhibiti hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana katika hili Halmashauri zetu Sheria Na. 8 ya mwaka 2007 hii ya Mipango Miji lazima isimamiwe katika maeneo hayo. Haya yote yataepusha hizo changamoto ambazo tunasisema. Kwa hiyo, Wizara kama msimamizi, tuko karibu sana na Halmashauri kushirikiana nazo, lakini Waheshimiwa Wabunge ni jukumu letu pia kuhakikisha kwamba tunapoona hali inakuwa siyo nzuri, kwa sababu tunahitaji miji iliyopangika na miji ambayo ni salama, ni jukumu letu pia kuwakumbusha wataalam wetu kuweza kusimamia mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mipango kabambe ya miji ambayo inatakiwa isiihie kupanga tu miji mikubwa, bali ipanue wigo wake. Hili linafanyika na sasa hivi kuna kujumla ya mipango kabambe 26 ambayo iko katika hatua mbalimbali. Mpaka sasa mji wa Mtwara pamoja na Musoma mipango yake kabambe imekamilika toka mwezi Mei na Mheshimiwa Waziri alikwenda kuzindua. Kwa hiyo, mipango mingine bado iko kwenye mchakato na tutaendelea kufanya hivyo. Wizara imeandaa programu ya utayarishaji wa mipango kabambe kwa nchi mzima ikiwemo miji midogo ambayo inakua kwa kasi. Kwa hiyo, hili tunalichukulia kwa uzito wake na tutaendelea kulisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa hoja za hotuba ya Waziri Kivuli, ametoa hoja nyingi sana. Niseme tu kwa ujumla wake pamoja na zile ambazo nimemaliza kuzijibu kwamba tunaandaa pia kitabu ambacho kitajibu hoja zote, maana kwa muda uliopo siwezi kuzijibu zote, nitajibu chache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kupima ardhi ya Mkao wa Morogoro kama mpango wa dharura ili kupunguza migogoro; wameongelea kwenye hotuba hiyo. Niseme tu Tume inaendelea na mipango ya matumizi bora ya ardhi. Kama nilivyosema awali na hata katika kujibu maswali tunapojibu, Morogoro ilichukuliwa kama eneo ambalo Serikali ilikuwa inaliangalia kwa jicho pana zaidi kutokana na migogoro yake iliyokuwepo. Ndiyo maana zile Wilaya tatu ambazo sasa tunapima ardhi yote, imeanzia Morogoro, ni kwa sababu ya tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili nalo tunalichukua, hivyo vipande vya ardhi vyote vitapimwa na kuwekewa alama za kudumu ili kuweza kuепusha hii migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ambalo limeongeleta kwenye maeneo ya Hembeti, Ndimboho, Buguma, Mkindo, Kigugo, Kambara vilivyopo katika bonde la Mto Mgongola

Wilaya ya Mvomero, nadhani Serikali itachukua taratibu zake vizuri kuweza kuona kwamba tunafanyaje, kwa sababu hali halisi kila mmoja anaifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume inashirikiana na programu ya kurasimisha ardhı katika Wilaya tatu nilizowaambia. Kwa hiyo, hatua zinachukuliwa na tunaendelea. Vile vile Tume inashirikiana na Halmashauri za Wilaya Mvomero na asasi za kiraia kama ile ya *PELUM Tanzania TFCG* na *IWASHI* katika kutoa elimu. Lazima elimu iwfakie ili waweze kutambua ni nini kinatakiwa kufanyika. Kwa hiyo, haya yanafanyika. (*Makofı*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, Kambi Rasmi imeongelea kuhusu changamoto kubwa ya kibajeti katika Wizara na wakashauri pengine Serikali iongeze nguvu katika kushirikiana na Sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Urasimishaji katika eneo la Kimara ni mojawapo ya mfano ambao tunaweza kuusemea. Mradi huu lengo lake pia ulikuwa umekusudia kurasimisha viwanja 6,000, lakini mpaka tunavyoongelea sasa, viwanja 4,333 tayari vilikuwa vimeshapimwa na Hatimiliki zimetolewa 82 na kuna barabara ya urefu ya kilomita tisa imetengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *speed* ndogo ya kutoa hati inachangiwa na wananchi wenyewe. Kama Wizara imeweza kupima viwanja 4,333 kati ya 6,000, ilikuwa imekusudiwa watu wote 4,333 wawe wamechukua hati. Sasa hiyo huwezi kusema kwamba ni tatizo la Wizara. Ni tatizo la wananchi ambalo tunasema tunawapa elimu ili waweze kuona manufaa ya kurasimishiwa maeneo yao ili pia waweze kutumia zile hati katika shughuli za maendeleo. Viwanja vimepimwa lakini watu hawachangii. Ni jukumu letu Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuhamasisha wananchi wetu kuchukua hati zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa wale wote ambao zoezi hili linaendelea ikiwemo na Mkoa wa

Mwanza katika zile Wilaya za Nyamagana na llemtela, lakini tunao wenzetu wa Musoma, Lindi, Kigoma, Ujiji na Sumbawanga; nawaomba sana, zoezi hili ni kwa nia njema ya kutaka kuwasaidia wananchi. Kwa hiyo, pale ambapo urasimishaji unafanyika, nawaomba sana wananchi, kwanza mchango siyo mkubwa ukilinganisha na gharama halisi ya upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba nia ya Serikali ni nzuri. Kwa hiyo, watumie fursa hii ya sasa ambayo ipo. Mkishaweka mipango kabambe katika maeneo yenu, unaweza kukuta urasimishaji tena hauna nafasi na tusingependa tufikie hapo. Kwa hiyo, hatua tuliyonayo sasa ni vizuri wananchi wanakaifanyia kazi iliwaweze kufaidika na zoezi hili linaloendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wameongelea suala la migogoro kati ya mpaka wa Kisopa King'azi na Mloganzila; fidia ilishalipwa kama ambavyo ilikuwa imetajwa katika masuala mazima ya uendelezaji na hii iko katika Wilaya ya Kisarawe ambayo ilikuwa imeanzishwa kwa *GN* hiyo 117 ya tarehe 28 Novemba, 1980. Katika ule mgogoro uliokuwepo pale, wale ambao walikuwa wameendeleza walikuwa tayari Serikali imelifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa *GN* 69 ya 29/1/2016, eneo hilo la Ubungo ilimega sehemu ya Kinondoni ambayo ilijumuisha maeneo ya Kisopa na King'azi, Mloganzila hiyo ilikuwa ni chanzo cha migogoro. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara itashirikiana na TAMISEMI ili kupata suluhu ya mgogoro huu. Kwa sababu kama kunakuwa na mgongano wa *GN* au kunakuwa na mgongano wa kijiji na kijiji, bila kuwa na elimu kwa wale hasa walioko katika maeneo yale inaweza ikaleta shida; suala la mipaka wakati mwingine linakuwa lina shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi Wilaya mpya inapoanzishwa siku zote inakuwa na changamoto zake, hasa upande mmoja unaposhindwa kuridhia ama kuachia baadhi ya maeneo. Kwa hiyo, migogoro kama hii inakuwepo tu,

lakini Serikali itaendelea kushirikiana na TAMISEMI kuhakikisha mgogoro huu unakwisha katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine inayosema Serikali imalize ufanuzi kuhusu mgogoro wa mpaka kati ya vijiji na hifadhi ya wanyama Serengeti, ambayo imezungumziwa hasa katika maeneo ya Viji ya Marenga, Nyamakendo, Mbalimbali na vijiji vingine kama vilivyo, hivi vyote katika Wilaya ya Serengeti vina mgogoro na hifadhi kama ambavyo ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri tu Mheshimiwa Mbunge kuwa ni vema tukasubiri maamuzi ya Mahakama, sababu hili suala liko Mahakamani na hatuwezi kulitolea maamuzi hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo ilikuwa limezungumziwa na Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba Serikali ieleze Bunge sababu za kuipa *TRA* mamlaka ya kukusanya kodi ya majengo ambayo ilikuwa ni chanzo muhimu kwa Halmashauri zetu. Tumesema *TRA* ilipewa jukumu la kukusanya kodi ya majengo ili kuimarisha mfumo wa ukusanyaji kodi. Hii yote ilipangwa kwa nia njema katika kurahisisha ukusanyaji maduhuli ya Serikali na zoezi limeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile limezungumziwa suala zima la kupanga *rates ambazo* pengine wakati mwagine zinaweza kuwa ziko juu au zipangwe kulingana na viwango. Hii tumechukua kama ushauri ambao tunaweza kwenda kuufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia suala la kutatua migogoro ya eneo la mnada wa Pugu Kajungeni na UKIVIUTA, Kipawa. Eneo la Mnada wa Pugu Kajungeni lipo chini ya Wizara ya Kilimo na Mifugo na eneo hili limevamiwa na wananchi na kuendelezwa. Utatuzi wa mgogoro huu utahusisha wadau mbalimbali ikiwemo Wizara yenyewe ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba wavute subira kwa sababu itafanyiwa kazi. Vile vile kuhusu UVIKIUTA, suala hili liliifikishwa Mahakamani na Mahakama ilioa ushindi kwa UKIVIUTA. Kwa hiyo, nalo tayari lilishatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna lingine limeongelewa kwamba Wizara iandae takwimu za hati ambazo zipo. Ushauri umezingatiwa, tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameongelea pia suala la Wakuu wa Wilaya kuingilia majukumu ya Mabaraza ya Ardhi. Suala hili, kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza ya Ardhi, Sura Na. 216 kama ambavyo imerejewa mwaka 2002, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba Wilaya ni chombo huru cha kuamua migogoro ya ardhi. Hivyo haipaswi kuingiliwa na chombo chochote katika kutekeleza majukumu yake. Kwa hiyo, masuala haya yako kisheria na tunasema yataendelea kusimamiwa chini ya sheria husika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kuhamisha ajira ya Watumishi wa Sekta ya Ardhi kutoka Halmashauri kwenda Serikali Kuu. Serikali itaendelea kutekeleza ile dhana ya *D by D*, hatuwezi kusema leo tunaibadilisha hapa kwa sababu tayari utekelezaji wake unakwenda vizuri na wote tunaona, lakini hayo yote yatafanyika kwa utaratibu ambao Serikali imepanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuhamisha ajira za watumishi katika Sekta ya Ardhi kutoka Halmashauri, unakinzana na dhana hii ambayo Wabunge wanaipendekeza. Ili kuongeza huduma kwa wananchi, Wizara imefungua ofisi za Kanda, kwa hiyo, tutashirikiana na Watumishi wa Ardhi kwenye Halmashauri kuona kwamba kazi hizi zinafanyika katika utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia suala la Serikali kuwa na vipaumbele vya kutekeleza kulingana na mapato yake kuliko kuwa na vipaumbele vingi ambavyo wakati mwingine havitekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba Serikali imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa kuweka vipaumbele muhimu ikiwa ni pamoja na kutekeleza bajeti kulingana maoteo yanayopangwa katika *projections* zetu tunazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, suala la kuwa na vipaumbele vingi sidhani kama ni sahihi sana kwa sababu wakati mwingine unapanga ukitarajia kwamba maoteo yanakwenda kufanya kazi katika utaratibu uliopangwa. Isipokuwa wakati mwingine ufinyu wa bajeti unafanya usitekeleze jukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kusema kwamba usipange, maana hizi ni *projection* ambazo ni lazima uziandae. Kwa hiyo, unapoandaa unategemea pia utapata pesa na tunafanya kazi kwa *cash budget*, kwa hiyo, lazima pia haya nayo tuyazingatie. Pia fedha ya Serikali inatolewa kutegemeana na makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nawaomba tu Waheshimiwa Wabunge, tuisitize katika kukusanya pato la Serikali ili tuweze kuhudumia bajeti zetu ambazo tumezipitisha. Ni vema wananchi walipe kodi zao kwa wakati ili kuwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake. Usipolipa kodi kwa wakati, matokeo yake shida inakuwa ni hiyo. Sasa hivi watu mpaka wafuatwe na Polisi, *Summons* za Mahakama ndio walipe kodi. Kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukiwa wazalendo kweli, kila mmoja akatimiza wajibu wake; unajua unatakiwa kulipa kodi ya ardhi kila mwaka, wewe lipa. Kwa nini unangoja mpaka uletewe *Summons*? Wakipelekewa *Summons* za Mahakamani, kesho yake unaona foleni kubwa iko kwenye Ofisi za Wizara. Sasa hivi ukienda *TRA* hapaingiliki katika zile kodi za majengo. Watu wamejaa pale, wanashinda pale. Kwa nini unangoja mpaka ufikie hatua hiyo? Lipa kodi kwa wakati ili uondoe usumbufu. Tukiweza

kuwajibika, haya yote hayatakuwa tena na usumbufu katika utekelezaji. Kwa hiyo, ni jukumu letu kuona ni jinsi gani tunasaidiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia hoja mbalimbali za Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba sasa nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge mmoja mmoja na nitaziunganisha zile zinazofanana ili kwenda na wakati na kwa zile ambazo nitakuwa nimezijibu wakati najibu hoja za Kamati pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani, nitaziruka na sitazirudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mheshimiwa Abdallah Ulega na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, walikuwa wanazungumzia suala la kupunguza urasimu katika upimaji ardhi kwa wananchi wa vijiji ili kuwaondolea usumbufu. Wizara yangu imepunguza sana gharama. Walikuwa wanazungumzia gharama na kupunguza urasimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imepunguza sana gharama na hata kama kwenye bajeti mmesikia, tumezidi kupunguza gharama. Lengo letu ni kuhakikisha usumbufu kwa wananchi haupo. Kwa hiyo, ni jukumu letu kuwahamasisha wananchi wetu waweze kuona umuhimu wa kupima maeneo yao ili waweze kuwa na umiliki halali ambaeo utawasaidia pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Wizara ni kuendelea kuhakikisha tunawawezesha wananchi. Unamwezesha kwa kutumia ile ardhi yake; ukiweza kumpa Hakimiliki kisheria tayari utakuwa umemsaidia. Kwa hiyo, niseme kwamba Wizara itaendelea na utaratibu wa kupata vifaa vya upimaji ili waweze kupimiwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa habari njema tu, kama mmesoma magazeti ya jana, tayari kuna *tender* imetangazwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo na ile *No objection* tuliyokuwa tunaisubiria kutoka *World Bank*, nayo tayari imetoka. Kwa hiyo, tuna uhakika vifaa hivi mtakwenda

kuvipata na kazi itafanyika na watu watapimiwa, tuwahamasishe tu wajitokeze kwa wingi ili waweze kupimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo limeongelewa na Wabunge kama wanane; ameongea Mheshimiwa Mama Makilagi, Mheshimiwa Paresto, Mheshimiwa Shekilindi, Mheshimiwa Mwassa, Mheshimiwa Bashungwa, Mheshimiwa Bilakatwe, Mheshimiwa Chumi na Mheshimiwa Allan. Wamezungumzia kwamba Serikali itenye fedha kwa ajili ya kuanzisha mabaraza. Nilishalizungumzia lakini bado limejirudia. Lengo letu bado lipo pale pale, tumechukua hoja zetu na tutafanya kama ambavyo imekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ule utaratibu wa maeneo ambayo pengine hayana Wenyeviti, nachukua fursa hii kumwomba sana Mkuu wa Mkoaa wa Singida pamoja na Mkuu wa Mkoaa wa Tabora; tunajua huko kuna matatizo na Wenyeviti ambao muda wao tayari ni kama ulikwisha lakini Wizara ilishawaandikia barua kwa ajili ya kuleta mapendekezo katika hatua ile. Mpaka leo hawajatoa na limejitokeza hapa kama ni tatizo. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa katika maeneo hayo watusaidie ili tuweze kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la uwezeshaji Mabaraza nalo limezungumzwa na Mheshimiwa Paresto tena, likazungumzwa na Mheshimiwa Makilagi, yamejirudia katika maeneo hayo. Mabaraza yana changamoto nyangi na ndio maana yamezungumzwa sana. Wengine wamezungumzia suala la kutoa elimu kwenye Mabaraza ya Kata. Napenda niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba suala la Mabaraza ya Kata yapo chini ya TAMISEMI. Kila tunapokwenda katika ziara tumekuwa tukishirikiana nao kuweza kutoa elimu katika yale mabaraza kwa kutumia wale Wasajili wetu wa Mabaraza kwenye yale maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishasema kwamba Halmashauri yoyote iliyopo tayari, Wizara ipo tayari kutoa

wawezeshaji wakisaidiana na Mwanasheria wa Halmashauri kuweza kuwapa elimu wale Wajumbe wa Mabaraza waweze kufanya kazi yao vizuri. Hii ni kwa sababu haya yapo chini ya TAMISEMI, lakini kwa sababu yote yanasmamia Sekta ya Ardhi, basi tunashirikiana kuhakikisha tunawapa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu lilizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge hapa ni kwamba wapewe mafunzo ambayo imezungumzwa pia na Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Bilakwate na Mheshimiwa Allan ili waweze kufanya kazi yao vizuri. Tutaendelea kusaidiana na Halmashauri zetu. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba hawa watu wanapata elimu na wanawasimamia masuala yote ya ardhi katika maeneo yao kwa sababu wao ndio hasa waliopo kwenye zile changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako hilli, nawashukuru sana viongozi wa Mkoa wa Katavi na Sumbawanga, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi, wamechukua hatua mahususi ya kuweza kuanza utaratibu wa kutoa mafunzo ya mabaraza hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Wilaya ya Kalambo walitoa mafunzo ya siku ya zaidi ya 20 kutaka kuwezesha yale Mabaraza. Jambo hilli linawezekana pale ambapo dhamira ya dhati katika maeneo na viongozi husika wakilionia kwamba ni changamoto, inawezekana kuyapatia ufumbuzi. Nitumie fursa hii kuwapongeza na nitoe rai kwa mikoa mingine kuweza kuiga mikoa hii miwili ambayo imeweza kufanya kazi nzuri katika kuelimisha Wajumbe wa Mabaraza waweze kufanya kazi zao vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbaraka Kitwana alikuwa anazungumzia mgogoro wa Shamba la Utumanî lenye ukubwa wa hekari 4,000 na shauri hili lipo Mahakamani, kwa hiyo akataka sasa watu wa Mafia wafanyiwe ugawaji. Sasa nasema, hili suala bado halijafikia hatima yake. Kwa hiyo, halizezi kufanyika jambo lolote katika utaratibu huo, lazima hatua za Kimahakama ziishe ili tuweze kwenda kwenye hatua nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Shangazi amezungumzia suala la Mnazi *Sisal Estate* la Lushoto ambalo nalo amelizungumzia. Taratibu za kufuta zimekwama kutokana na miliki za shamba hili kuwekwa dhamana benki. Hii ni kwa sababu kuna wamiliki wengi wa mashamba wengine walichukulia mikopo na hasa kwa Korogwe, Mkoa wa Tanga, mashamba mengi sana yamechukuliwa mikopo benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo linapokuwa limewekwa dhamana ya benki, huwezi kuanza kufanya taratibu nyingine. Kasoro hizi ambazo zinatokana na hiyo, Halmashauri inaagizwa pia itume tena ilani katika shamba hilo ili benki waweze kupewa nakala ya ilani hiyo na ufutaji utaendelea baada ya taratibu zote kukamilika. Kwa sababu kuwa na dhamana isiwe ni kikwazo. Tumeni tena ilani na benki wapewe nakala illi wajue pamoja na kwamba wana dhamana hiyo, lakini shamba hili lina changamoto zake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwakasaka alizungumzia suala la nyumba za *NHC*, watu kununua kwa wingi na kupangisha. Sina uhakika na malalamiko yake labda angetupa mfano mzuri ni wapi, kwa sababu Tabora, Uyui na Igunga kuna nyumba zimejengwa pale, hazijapata wapangaji na hazijanunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa aliyenunua na kuhodhi nyingi ni zipo? Kwa sababu hiyo ni *case study* ambayo iko wazi kwamba nyumba zipo, lakini hazijanunuliwa. Ni vyema akatufahamisha ni wapi ambapo nyumba zimenunuliwa na mtu mmoja halafu anaanza kupangisha ili tuweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lupembe vile vile amezungumzia nyumba ambazo zimejengwa lakini zinakaa *idle*. Niseme kwamba nyumba kukaa *idle* wakati mwingine Halmashauri pia zinakuwa zinahusika. Mnaomba kujengewa, zinajengwa. Zikishajengwa zimekamilika, hamko tayari kuchukua. Sasa hii kidogo inakuwa ni shida. Ndiyo

maana tukasema, Mheshimiwa Kalanga alikuja na wazo la kwamba watu wapewe miaka mitano kulipa lakini Shirika la Nyumba linatoa miaka 10 kwa mpangaji mnunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelekezo katika nyumba zilizojengwa ambazo Halmashauri hazijawa tayari kuzichukua, utaratibu wa shirika utabadilika kuliko kuacha ziharibike, zitakwenda kwenye ile sera ya mpangaji mnunuzi na zitauzwa kwa mtu ye yote aliyeo tayari kununua ili zile nyumba ziweze kupata wapangaji. Ikienda kwa mpangaji mnunuzi, maana yake una miaka kumi ya kuweza kulipa. Mheshimiwa Kalanga aliomba miaka mitano, lakini *National Housing* wameweka miaka 10. Kwa hiyo, bado nafasi tunayo ya kuweza kutumia nyumba hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, kwa sababu tusipofanya hivyo, haya mambo wakati mwingine tunaweza tukawa tunawalaumu wawekezaji, tunalaumu *National Housing* lakini sisi wenye we tunaohitaji pia tunakwamisha. Niwape mfano mzuri wa Jimbo la Busokelo, waliomba wakajengewa nyumba nzuri za mfano na tayari wamechukua; na Jimbo la Mombasa pia nao wamejengewa nyumba nzuri na zinafanya kazi na wanakwenda hatua nyingine ya pili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Halmashauri zetu, mnapohitaji muwe tayari pia kuhakikisha kwamba mnakwenda kuzichukua nyumba zile ili kuepusha uwekezaji unaokwenda kudumaa. *National Housing* hawawezi kusonga mbele kama wanawekeza halafu haziendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sakaya ameongelea wawekezaji wa miradi mbalimbali kwamba wapewe ardhi kuenenda na maeneo yanayofaa katika miradi husika. Viongozi wa Vijiji wapewe elimu. Hili tumelichukua kwa sababu Sheria ya Ardhi iko wazi na inatoa utaratibu mzima wa ugawaji ardhi. Sasa katika hili nadhani ni elimu tu izidi kutolewa kwa watu wetu waweze kujua ni jinsi gani ya kuweza kusimamia haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la ujenzi holela ambalo limeongelewa na Mheshimiwa Kigola. Nadhani nimeliongelea kwa upana wakati nazungumzia masuala ya uandaaji wa mipango kabambe na kuhamasisha wananchi kutojenga ili kuepuka hili. Wizara inashirikiana na mamlaka za upangajji katika maeneo hayo ili kuandaa mipango kabambe na hili suala litakuwa limepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Cosato Chumi ameongelea kupewa baadhi ya Watumishi nyumba za *CDA*. Wizara haihusiki moja kwa moja na utoaji wa nyumba hizi katika kupangia watumishi, lakini haya yamepokelewa na yanaweza kufanyiwa kazi kulingana na maombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Watumishi wa *CDA* kutawanya katika maeneo mengine, hili pia lipo chini ya Wizara husika kwa sababu *CDA* sasa hivi ipo chini ya Manispaa ya Dodoma, maana yake ipo chini ya Ofisi ya TAMISEMI. Hivyo, Wizara inayohusika kwa kushirikiana na Wizara yetu, kwa sababu wako pia Watumishi wengi tu wa Sekta ya Ardhi, basi tutaona ni jinsi gani bora ya kuweza kutatua hilo tatizo na hasa katika kuwapanga watu katika maeneo yanayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani muda umekuwa finyu na mambo ni mengi. Naomba uniruhusu tu nizungumzie suala moja la asilimia 30 ambayo imezungumziwa. Ndugu zangu suala la asilimia 30 limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie tena; baada ya ile Sheria ya Bajeti mwaka 2016 tulivyoipitisha ya kuondoa mambo ya *retention*, asilimia 30 haipo tena. Ndiyo maana tulisema na nikipita katika ziara nawaambia kwamba Halmashauri zinazopanga bajeti ya asilimia 30 kutegemea Wizara, tunapotosha bajeti zetu, kwa sababu hiyo iliondolewa katika bajeti iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa zinazokuja kwenye Halmashauri, zinatokana na *OC* ambayo Wizara inakuwa

imepangiwa shilingi bilioni kumi kwa mwaka 2016/2017 kwa nchi nzima na zinatolewa kutegemeana na zinavyoingia. Kwa hiyo, hajii kama asilimia 30 ambayo wewe unaiweka. Kwa hiyo, unapoweka kwenye bajeti yako asilimia 30 kwamba unadai Wizara, kibajeti kidogo inakuwa haiko sahihi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nisisitize katika hili maana limekuwa likijirudia, hakuna asilimia 30 kama 30 inavyorudi kule. Kinachokuja ni *OC* kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri zetu kwa shughuli za sekta na pesa hizo lazima zifanye kazi ya Sekta ya Ardhi na siyo Mkurugenzi kupanga matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, zitakuja kwa kadri zinavyoingia kutegemeana na bajeti ya Wizara illyowekwa kuliko hiyo ambayo ninyi mnaitegemea sasa kwamba ni asilimia 30, inapotosha kila kitu katika maelezo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nawashukuru kwa kunisikiliza. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa majumuisho mazuri. Sasa namkaribisha mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili aweze kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana wewe na Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima mliyotupa Serikali kupitia Wizara yangu kwa michango mizuri sana. Kila mmoja alikuwa anatamani kusikiliza michango kuanzia mtu wa kwanza mpaka wa mwisho, yaani tumefanya kazi ya kibunge vizuri. Hakuna jambo ambalo mimi sikuandika; kila jambo

nimeandika. Ingawa sikuandika maneno yote, lakini angalau kila hoja ya mtu naijua. Naweba kusema tulikuwa *very serious* katika kujadili mjadala huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza sana nasi kama Wizara tutaendelea kutekeleza mwongozo wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli; yeche kila siku anasema kwamba yeche ni Rais wa CCM, ametokana na CCM ndiyo, lakini amechaguliwa na Watanzania wote na kila mara amekuwa anasisitiza tutoe huduma bila ubaguzi wowote. Kwa hiyo, ndiyo maana *spirit* ya Wizara yangu ni kutoa huduma kwa wananchi wote na wananchi wote tutaendelea kuwahudumia bila ubaguzi wa aina yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu nawashukuru sana kwa niaba ya Wizara yangu na wenzangu wote, tuendelee kushirikiana, maana yake hii kama ninyi msingekuwa mnashirikiana nasi pengine tusingejua matatizo yenu. Kwa hiyo, tuendelee kushirikiana na moto ni huo huo. Tuna Ofisi hapa Dodoma, tuna Ofisi sasa kwenye Kanda na hapa nyuma yangu nimeleta viongozi wote wa Kanda nane. Kwa hiyo, kila jambo mlilolisema kama linahusu Mabaraza ya Ardhi, Msajili wa Mabaraza yupo hapa, Amina. Kama linahusu ardhi Kanda ya Magharibi, Kamishna na Msajili wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge Iijalo Mungu akipenda, mtazungumza mkiwa na Mthamini wa Kanda, Mpima wa Kanda, Kamishna wa Kanda, Msajili wa Kanda na wote hawa watakuwa wamekamilika na watumishi wao na vitendea kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili alilosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tumesema moja ya jambo ambalo mmelizungumza watu wengi humu ndani, kwamba tunakwama kupanga na kupima mashamba na wananchi kupata viwanja vyao kwa sababu hamna vifaa; tumeshaagiza vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetangaza kwenye gazeti, tutavisambaza hivi vifaa tena kwa teknolojia mpya, kwa sababu sasa tunatumia *satellite* na vifaa vya mapokezi ya *satellite* tumewaonesha jana, tumevinunua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tutakuwa na vifaa ambavyo vinapima kwa upana mkubwa kwa teknolojia mpya na tutawafundisha Maafisa wenu wote. Tutawaita hivi karibuni, Maafisa wenu wote Wapima, hawavijui hivi vitu, tutawafundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkipata nafasi, kule nyuma tumeweke Maonesho ya Wapima Binafsi, baadhi ya vifaa vya kisasa vya upimaji viko nyuma kule tunakofanya sherehe. Atakayepata nafasi aende. Tunaposema *RTK* mtaziona kule, kwa nini kifaa hiki kinaweza kikapima mpaka kilometra 30 kwa wakati mmoja na kikatumia watu wawili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wilaya yako yote inaweza ikapimwa kwa siku tano au sita tukapima mashamba yote. Kwa hiyo, teknolojia hii tumeagiza na tutasambaza kwenye Kanda na awamu ya pili tunakwenda kuandika tunataka tupeleke vifaa hivi kila Wilaya ili hata kama unamwita mpima binafsi, basi uwe una kifaa chako inapunguza gharama. Kwa hiyo, tutatatua kero za ana kwa ana, lakini tunafikiri vilevile twende kwenye mifumo na baadaye tutakuja kwenu kuomba sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachowashukuru ni kwamba mmetusaidia sana kuainisha mambo mbalimbali na haya sasa siyo kujibu tu kwa maandishi lakini tutayapangia na ratiba, tutakuja Mikoni kote huko. Tutakuja Kilimanjaro kufanya *audit*, tutakwenda Chumbi kwa rafiki yangu Mchegerwa, tutakwenda Mikoa ya Kagera kule Karagwe, tutaenda kila mahali. Tutakuja mikoni. Sasa hatuji mikoni tukisubiri ratiba za mikoa, tutakuja kuthibitisha haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshajua mambo ya kuanza nayo. Tutakuja kila mkoa. Mkoa wa Manyara, Iringa,

Ruvuma mpaka Mbinga tutakuja na kila mahali tutakuja, angalau tuna mambo ya kuanzia. Nataka kuwahakikishieni kwamba haya yote tutayaandika, lakini tutawapa majibu ili mjue lakini yatatusaidia sana tukija mkoani kufuatilia haya na kuhakikisha tunayatatua on the spot. Kwa hiyo, tutakuja ndugu zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepanga Kanda vizuri, sasa tunateua Watendaji wetu wapya kwenye Kanda wafanye hii kazi, mambo yote tutayafanya. Dar es Salaam tutakuja wenyewe nami bado nipo pale, yale yote ya Dar es Salaam tutayamaliza; ya Dodoma hapa tutayamaliza na mikoa yote tutafika na kuyafanya kazi. Kwa hiyo, nafikiri Waheshimiwa Wabunge hebu msibiri tuje. Tuna ratiba ya miezi 12 kabla hatujakutana hapa, tushirikiane huko huko mkoani kutatua haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengi yatatatuliwa, tutaulizana tena huko mkoani na wenzangu wanaotoka hapa wanaanza kuyafanya kazi. Inawezekana baadhi ya mambo mkrudi huko mtakuta yamekwisha kwa sababu viongozi wangu wa kanda wote wapo hapa wamesikiliza. Sasa tumewawezesha na magari mapya, wanakimbia kila mahali, kwa hiyo, hawana shida sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu nawashukuru sana kwa haya yote mliyoyasema nataka kuwaahidi kwamba tutawaijibu kwa maandishi, lakini tutakuja huko mkoani, tutajadiliana sana, tutafanya makongamano, tutaitisha na viongozi wengine wa mikoa tuzungumze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inayoendelea kubatilisha mashamba ya watu ambao hawayatumii, tutaeendelea kuifanya kila mahali; kazi ya kukagua mashamba yasiyotumika, tutafanya; kazi ya kupima kwa kasi ili kila mtu amilikishwe kiwanja, tutafanya. Leo ingawa bado mnazungumza gharama, lakini hizo gharama mnazozijua tumepunguza tozo kwa asilimia 67. Kwa hiyo, Mheshimiwa wa Mbinga hebu angalia taarifa yako. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kubwa ambazo hata ninyi Waheshimiwa Wabunge mna *offer* nilizowapa, angalieni ile kitu inaitwa *premium* mlicholipa; 67 ya ile mliliyolipa imepungua. Kwa hiyo, umilikishaji sasa utakuwa nafuu sana na tungependa kutoka sasa Halmashauri zote zisiruhusu hata kidogo watu kujenga katika maeneo au viwanja ambavyo havijapimwa na kupangwa. Kwa sababu kilio chao cha kupunguza tozo tumefanya, gharama za upimaji zitapungua sana na hivyo hakuna sababu mtu kuendelea kuvamia na kujenga katika maeneo ambayo hayajapimwa. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ya kwanza ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Nafikiri ni kengele ya kwanza!

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Eeeh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie ndugu yangu Mheshimiwa Malocha, alizungumza juzi hapa kwa uchungu sana juu ya shamba lake la Malonjo. Watu wako mmelitoa nje ya Mahakama mzungumze. Malizeni mazungumzo, mimi nasubiri. Wakati ule niliwashauri mpeleke *notice* na mtu wangu alisaidia kuandika *notice* tuka-serve *notice* kwa *Efatha*, lakin akawapeleka Mahakamani. Ninyi mmetoa kesi Mahakamani mzungumze. Zungumzeni, mimi nawasubiri. Kwa hiyo, kabla mambo hayajaja kwangu, msinilaumu. Nilisema miezi sita mkileta kwangu nitakuwa nimeamua, lakin haijaja kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri tutashirikiana na nimemwomba Mkuu wa Mkoa wa Rukwa asimamie hayo mazungumzo yenu, Mheshimiwa Malocha na Wabunge mshiriki haya mazungumzo ili yaishe vizuri. Kwa sababu hata yule mwekezaji ajue, lolote atakalofanya,

hataweza kulima lile shamba kwa ustaarabu kwa sababu wale wananchi wamechukia. Kwa hiyo, kwa mwekezaji lazima ajue kwamba lile shamba ni moto na wananchi mtekeleze haya mazungumzo yenu vizuri, *win-win situation*, mwendelee na hilo shamba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani zangu zote nimalizie kwa kusema changamoto zilizoainishwa kwenye mapendekezo yenu na hoja zenu ni nydingi sana, yaani nashindwa hata nianzie wapi; lakini ya Watumishi imezungumzwa sana hapa, Watumishi hatunao. Tutakachokifanya cha dharura kwanza, tutashirikiana na TAMISEMI kuangalia watumishi waliopo tuwapange vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zunguka yangu nimegundua kuna Wilaya zimependelewa, kuna Watumishi wengi sana. Ilemela na Nyamagana wana Watumishi wasiopungua 100 Wilaya mbili wa Sekta ya Ardhi, tutawaondoa huko. Hii ni kwa sababu kuna Wilaya nyiningine haina Mtumishi hata mmoja wa Sekta ya Ardhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutapita, kabla ya kuajiri wapya, tutaangalia uwiano wa jinsi walivyopangwa ili tuwa-*switch* angalau kazi za dharura ziweze kufanywa kwa watumishi waliopo tugawanye vizuri ili watumishi hawa wasambae maeneo mengine. Watu watapangwa upya halafu baada ya hapo ndio tutasimamia vibali kwa Mheshimiwa Angellah Kairuki ili wapya wakipatikana, tuwapange vizuri. Upangaji haukuwa mzuri tutaurekebisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi mmezungumza habari ya asilimia 30; masuala haya ya upangaji na kodi ya asilimia 30, kinachosisitizwa hapa ni kwamba tungependa miji yetu ipangwe, watu wajenge kwenye viwanja vilivyopangwa, lakini watu wamilikishwe mashamba angalau wapimiwe ili wapate hati. Sasa imekuja tu asilimia 30 lakini faida kubwa zaidi ya watu kujenga kwenye viwanja vilivyopangwa ni kuendeleza miji yetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, msiangalie tu asilimia 30, mwangalie vilevile kwamba hawa watu kodi tunazokusanya tunazikusanya kwenye viwanja ambavyo vimepangwa na kupimwa, kwa hiyo, Miji yetu imepangika. Kwa hiyo, tuendeleze kasi ya kushirikiana ya kupanga Miji yetu ili iweze kupangika vizuri na kuwawezesha wananchi kupata hati. Kila mwananchi akipata hati, tutaelewana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Naomba uhitimishe hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, lile suala la kutoza kodi kwa viwanja vyat mijini na mashamba madogo madogo ya mijini ambayo hayajapimwa, nina maelezo ya ziada. Nitakutafuta wewe na Mheshimiwa Mwassa wenyе hoja hii, tuzungumze, tujadiliane. Kinachokufanya wewe useme ni shamba lako mjini ni nini? Hicho hicho tuta-register.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu haiwezekani wewe unapata faida kubwa pale mjini, una ekari 40 Dar es Salaam, una ekari 4,000 Dar es Salaam hutaki kupima, lakini unauzu vipande vipande unapata hela; hulipi *capital gain*. Hivyo hivyo, unavyojifanya wewe vinavyokutambulisha kwamba ni shamba lako, tutavisajili hivyo hivyo na utatulipa pesa, lakini nitawatafuta ninyi wawili, msishike shilingi ili niwafahamishe vizuri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, Mwenyezi Mungu awajalie wale wanaoendelea kufunga na sisi wala futari, makobe, tupo, tutawasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuhitimisha hoja. Katibu.

**WABUNGE FULANI:** Hajatoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Katibu, tuendelee.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na  
Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1001 *Administration and HR Mgnt.* ... Sh. 6,736,586,549/=

**MWENYEKITI:** Tumeshapokea majina ambayo tutaanza nayo. Tunaye Mheshimiwa Lwakatare na huku tunaye Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Ester Mmasi. Tuanze na Mheshimiwa Lwakatare.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wetu kama Kambi ya Upinzani, tulilizungumza kwa kina na kulihoji suala la bomoa bomoa pale Dar es Salaam. Sitaingia kwenye *angle* ambayo wakati wa kujibu Serikali ilizungumzia masuala ya Mahakamani kwamba haiwezi kutoa maelezo. Ni suala la *principle* tu, ambayo nikiacha historia niliyoieleza ya barabara

ile ya Morogoro, lakini ningetaka Serikali itufafanulie na kwa faida ya wananchi hasa upana wa barabara na huu utata unaozungumzwa sana na kuleta sintofahamu, unaanzia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nikienda kwenye sheria ya mwaka 2007 ambayo ilikuja kutengenezewa kanuni mwaka 2009, upana unaotamkwa unakuwa na maana ya pande zote mbili. Kama upana ukitamkwa wa mita 60, maana yake inakuwa 30 kwa 30; ukitajwa upana wa mita 90, maana yake ni 45 kwa 45; na ikitajwa 121 maana yake ni *half* ya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ya 121 upande mmoja na 121 upande mwingine, barabara yenyewe upana wa 240 na kitu, yaani ni viwanja vya mpira viwili na kitu, inatoka wapi? Ni barabara ya wapi hii? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai Serikali inaweza ikawa na shughuli za kimaendeleo katika eneo fulani; tunafahamu kabisa watu waliolipwa fidia ni mita 28.85, sasa watu wanaokuwa nje ya mita hizo mbona hawazungumziwi kwenye fidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu na yasipotoka kisawasawa, nakamata shilingi yako, sijui utakula wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii ili niweze kufafanua hoja ya bomoa bomoa ambayo Waziri Kivuli, Mheshimiwa Lwakatare, ameiongelea. Naomba tu nimweleze kwamba eneo hilo lina historia ndefu na kulishawahi kuwa na kesi na hatimaye Mahakama ikaamua katika eneo hilo. Wanaokaa pale wanalifahamu sana, mwanzo kwa kupitia Mawakili wao na hatimaye kesi ikaamuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile eneo liko maalum, lina futi, maana wakati huo masuala ya mita hayakuwepo katika sheria, lina futi 400 kila upande na ndiyo msingi wa kesi ambayo iliendeshwa na hatimaye Serikali ikashinda. Kesi iliamuliwa mwaka 1997, kwamba eneo hilo ndiyo hifadhi ya barabara na ilipangwa muda mrefu tu tungeshaweza kuliendeleza hilo muda mrefu lakini hiyo kesi ndiyo ilikuwa imesimamishwa kwa muda mrefu na bahati nzuri tunashukuru kesi iliisha na hivi sasa tunatekeleza tu hukumu ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upana ni futi 400 ambayo ukija kuibadilisha kwa mita unapata mita 121.5. Huo ndiyo msingi wa maamuzi hayo, ni ya siku nyingi; ni eneo ambalo Serikali ilishali-*claim*, ilishallilipia fidia kwa wale amba walistahili kulipwa fidia mwaka 1977 na hatimaye ugomvi wa pale uliisha. Kwa kweli nashukuru sana wananchi wengi katika maeneo yale wanalifahamu hilo na wako tayari kubomoa maeneo yale. Walikuwa wanadhani tu kwamba mipango ya Serikali labda imesimama kwa muda mrefu, kwa hiyo, wakayaendeleza yale maeneo huku wakijua kwamba wako ndani ya hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba sana ndugu zangu, mtupe fursa ya kujenga miundombinu na katika eneo hilo, lipo kwa mujibu wa sheria na uamuzi ulishapita mwaka huo niliosema, 1997. Hukumu ilitoka.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, umeeleweka. Mheshimiwa Lwakatare.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri sijui kama anakwenda na *reality* ambayo ipo. Kwa kweli katika suala hili naomba nitoe shilingi ili Waheshimiwa Wabunge wapate nafasi ya kujadili hoja hii, kwa sababu eneo liliolipiwa fidia ni la mita 28.8 na ushahidi upo. Sasa Mheshimiwa Waziri anapozungumza kwamba hilo eneo lote limelipiwa, ni uongo na nina uwezo wa kuthibitisha nikipewa muda, kwamba eneo lingine halijalipiwa na watu wanadai. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nieleze, hizi futi 400 ambazo ame-convert kwenye mita 121, ni kutoka wapi? Katikati ya barabara kwenda pande zote au ni katikati, tunazigawanya mara mbili? Ndiyo hilo nataka nipate majibu hapo. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hujatoa hoja.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuondoa shilingi.

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja ya kujadiliwa.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tizeba, Mheshimiwa Jafo na huku Mheshimiwa Millya na mwanamke, Mheshimiwa Mwassa. Wanatosha. Basi Wanatosha hao jamani, tunaendelea.

**MBUNGE FULANI:** Mwenye Jimbo.

**MBUNGE FULANI:** Tunawahi kwenda kuswali!

**MWENYEKITI:** Mwenye Jimbo! Basi tumtoe mmoja, tunamweka mwenye Jimbo. Haya, tunaanza na Mheshimiwa Jafo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia hoja ya kaka yangu hapa, Mheshimiwa Lwakatare, ni hoja ya msingi, lakini nadhani Mheshimiwa Waziri hapa, nina wasiwasi inawezekana tukam-slaughterbure, tutamwonea kwa eneo lake kwa sababu mshahara wake huo wa Waziri ambapo tukienda nayo inawezekana tukamwonea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tulikuwa na jambo kubwa la *consensus* kwamba leo mjadala huu uende vizuri tumalize salama; na kwa sababu najua jambo hili ilibidi lilelewe vizuri katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ndiyo kama tungekamata mshahara wa Mheshimiwa Waziri ingekuwa kidogo na utamu wake. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe tu Mheshimiwa Lwakatare, nadhani hoja yako ni ya msingi imesikika. Kama Serikali, tunesikia hizi *concern* kuona nini tutafanya kuboresha mambo mengine ya msingi ili mradi wananchi wapate huduma yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mwenye Jimbo halafu katika ninyi wawili, mmoja. Tumekubaliana.

**MHE. SAED A. KUBNEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja ya Mheshimiwa Lwakatare.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri ameliambia Bunge kwamba wananchi wa eneo hili wapo tayari kubomoa na wapo tayari kuhamza. Habari hii siyo ya kweli. Wananchi wa Kimara na Mbezi hawako tayari kubomoa. Ndiyo maana wanajiandaa sasa hivi kwenda Mahakamani kuomba zuio ili eneo hilo lisibomolewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema katika maelezo yake, kwamba eneo hili ni eneo la barabara na kwamba barabara hiyo imekuwepo kwa miaka yote hiyo, lakini wananchi wa Kimara wanaishi pale kwa hati ya kijiji iliyotolewa mwaka 1974.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anazungumzia mambo ya 1977. Kama barabara walijua mwaka 1977 kwamba itapita Kimara, kwa nini mwaka 1974

walitoa hati ya kuishi? Hati ya wananchi wa Kimara, wananchi wa Mbezi ni ya mwaka 1974 ya Vijiji vya Ujamaa. Mheshimiwa Waziri anazungumzia mambo ya mwaka 1977. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wako tayari kuhama, lakini ni lazima walipwe fidia. Haiwezekani watu wamefanya kazi miaka 30, 40, wamejinyima, wamejenga nyumba zao halafu Serikali ikabomoe hizo nyumba bila kulipa fidia. Mbona maeneo mengine wamelipa fidia? Mbona katika maeneo ya Majimbo mengine wamelipa fidia? Kwa nini wananchi wa Kimara, Ubungo, Mbezi na wananchi wa Jimbo la Kibamba wasilipwe fidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatupingi ujenzi wa barabara, tunachotaka wananchi ni wananchi walipwe fidia.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SAED A. KUBNEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mwassa.

**MBUNGE FULANI:** Iko Mahakamani tayari.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami niendelee kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Lwakatare hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, Naibu Waziri, mimi naona bado hujaelewa vizuri Sheria za Ardhi. Kwa sababu unavyotuambia kwamba toka mwaka 1970, kama umeweka 1970 *mark* ya eneo ina maana hilo eneo ultakiwa ulilinde. Kama watu wamejenga wewe ukiwepo, kuna maghorofa makubwa, watu wamekaa, ulikuwa wapi? Sasa kwa nini uweke alama? Kwa sababu umiliki wa ardhi

unasesma kwamba mmiliki lazima alinde eneo lake. Sasa kama ni *road reserve*, ulikuwa wapi mpaka mwananchi anajenga? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mtu ambaye alizaliwa mwaka 1970 ni mzee na Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 inasema kwamba mtu akikaa kwenye eneo husika miaka mitano anapata umiliki wa asili. Basi wale wana umiliki wa asili, kwa sababu tayari wana miaka zaidi ya 40 pale. Kwa hiyo, wana haki ya kulipwa fidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Wizara hii ni mtambuka, ashirikiane na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano waende kwenye hilo eneo, Mbezi na Kimara, wawapatie fidia zao. Hawawezi kuwawekea 'X' miaka!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hizo 'X' zilizowekwa zimewekwa miaka isiyozidi hata mitano na ile *marking* imewekwa hivi karibuni, siyo miaka ya 1970. Kwa hiyo, wana haki ya kulipwa fidia. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eng. Kamwelwe, Naibu Waziri wa Maji, halafu Mheshimiwa Tizeba.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili nitoe historia kidogo. Barabara ya Morogoro ina hifadhi ya futi 400 kila upande. Hifadhi hiyo iliwekwa na Mwingereza baada ya Vita Kuu ya Pili. Eneo hilo liliipwa na Mwingereza ikiwa ni pamoja na mashamba ya katani na *cheque* za mashamba ya katani zilikuwa zimeandikwa 'X' *Enemy*. (*Makof*)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
waliangea bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Subirini niwaambie. Kwa hiyo, hiyo ni hifadhi ya barabara na Mwingereza aliweka na maandishi yapo. Ni kwa nini aliweka

hifadhi hiyo? Ni kwa sababu alikuwa amelenga kwamba Miji ya Dar es Salaam na Morogoro itaungana na akaona kwamba maendeleo yatakuwa makubwa kiasi kwamba *container terminals* hazitakaa kule Bandari ya Dar es Salaam, ila zitakuwa ziko pembeni ya barabara ya Morogoro na kwamba zitajengwa *trams* kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro, ndio maana aliweka hifadhi hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba walilipa mita 28.8. Kipindi Mwingereza analipa fidia, *concentration* ya binadamu ilikuwa kaeneo kadogo kwa sababu ni miaka hiyo ya nyuma. Maeneo mengine yalikuwa ni mapori ndio maana ukienda kupata *record* utakuta kaeneo kalikolipiwa fidia ni kadogo kwa sababu watu waliokuwa wanaishi hilo eneo walikuwa ni wachache. Kwa hiyo, eneo hilo tayari lilishalipiwa fidia na ushahidi upo na *cheques zipo*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kulikuwa na kesi. Kwenye hiyo kesi, mimi nilikuwa shahidi wa Serikali na tulishinda. Wananchi wa Kimara walishtaki na aliyekuwa anawasaidia ni Mwalimu mmoja wa Chuo Kikuu anaitwa Profesa Mgongofimbo. Mimi nilikuwa shahidi wa Serikali na kesi hiyo tulishinda na ushahidi wa kushinda upo. Kwa hiyo, huwezi ukalipa fidia mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa Mbunge arudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu ushahidi wote upo. Eneo hilo limelipiwa, ni halali, ni mali ya Serikali. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa historia fupi, tunaendelea na Mheshimiwa Tizeba.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee hapo alipokomea Mheshimiwa *Eng. Kamwelwe* kwamba, suala likishaamuliwa Mahakamani, mtu ye yeyote ambaye hakuridhika na uamuvi wa Mahakama, haji Bungeni isipokuwa anakwenda tena Mahakamani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu uamuzi ulishatolewa na Mahakama katika kesi mbalimbali, mimi niwashauri sana Mheshimiwa Lwakatare na Mheshimiwa Kubenea, yule ambaye anadhani kwamba kilichotendeka siyo haki anayo nafasi bado ya kuendelea kutafuta haki yake Mahakamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sheria mbili zinazotawala mambo ya ardhii katika miji, Sheria Na. 378 ya Mipango Miji na Sheria Na. 167 ya Barabara zinataja wazi size za mabarabara katika maeneo ya miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ya miji barabara ni kiwanja kama kingine; ina urefu na upana na kila kitu na vyote vinafahamika. Kwa maana hiyo, nirejee kwa hoja alioisema Mheshimiwa Mwassa kwamba kuna watu kwa sheria fulani wamekaa miaka mitano, hilo jambo haliendi *automatically*. Unaweza ukapata haki hiyo kama mwenye hilo shamba au hicho kiwanja amekuwa hakulalamikii kwamba uwepo wako pale unavunja haki yake ya umiliki wa hicho kiwanja au shamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka za Serikali zimekuwa mara zote zikiwaambia wananchi wa Kimara kwamba hapo mnapojenga ni eneo la hifadhi ya barabara au ni *right off wayya* barabara ya Morogoro - Dar es Salaam. Kwa hiyo, haya mambo kwa yejote ambaye anadhani kwamba bado mambo yake hayajafanyiwa haki, arejee Mahakamani, akate rufaa, haki yake itapatikana huko.

Mheshimiwa Lwakatare, mwachie Mheshimiwa Waziri shilingi yake na wale wote wanaofikiri wako bado *aggrieved*, wanayo haki ya kurudi Mahakamani kutafuta haki yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lwakatare umeridhika ama tulihoji Bunge?

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa ni hivi, kaka yangu Mheshimiwa Lukvi ananielewa. Suala linalotakiwa hapa ni jepesi tu, la kuangalia tuendeje mbele.

Sitaki kuingia kwenye mtazamo wa mmoja wa Waheshimiwa Wabunge ambaye amesema majibu ya Mheshimiwa Waziri anayashangaa huenda alikuwa hajafika hata Dar es Salaam, pamoja na kwamba yeye ni shahidi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilichotaka kujuu, Kanuni za mwaka 2009, urefu unapotajwa wa barabara, tafsiri yake inakua ni kuanzia katikati ya barabara, unaigawanya mara mbili; kwenda huku na kwenda huku. Nataka kujuu, hiyo 121 kwenda hivi na 121 kwenda huku mmetoa kwenye Kanuni zipi? Hilo ndilo swali nillotaka kujibiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Serikali inapaswa itambue, kuna watu wana hati na wanazilipia mpaka hata jana kwenye eneo hili. Serikali wako wapi tangu hiyo miaka tunayotajiwा hapa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ningefurahi sana tungekwenda na mkondo aliouzungumza Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo kwamba hii *issue* ina *complications* zake. Ni vizuri Serikali, TAMISEMI, Ardhi na wananchi, pamoja na *TANROADS* wakakaa, hili jambo likazungumzika kutokana na *facts* zilizopo badala ya kila mmoja kuleta hadithi za mwaka 1947 za *Queen Elizabeth*, sijui lilitokea wapi, ambalo litatuingiza kwenye hoja nyingine mpya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lwakatare kwa hiyo, umeridhika baada ya maelezo hayo? Umeridhika eeh? Haya ahsante sana, tunaendelea.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Naomba *commitment* ya Mheshimiwa Jafo aliyoshauri hapa, naomba tuendelee mbele.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waziri wa Sera wa huku, hatuna shida na kurudisha shilingi

ya Mheshimiwa Lukuvi, tunachosema, *commitment* aliyotoa Mheshimiwa Jafo ni jambo la msingi sana; na tumeanza vizuri hapa, umeona; kuliko haya mambo mengine yote ambayo yanaendelea.

**MBUNGE FULANI:** Ya *Queen Elizabeth!*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pamoja na watu wa kule wakae waone ni namna gani tutalimaliza hili kwa *commitment* ya Mheshimiwa Jafo, hatuna tatizo kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwetu huku upande wa Serikali, Serikali ni moja; *whether* limefanywa na Ujenzi, limefanywa na Mheshimiwa Jafo au Mheshimiwa Lukuvi, Serikali ni moja. Serikali hii inatekeleza wajibu wake kwa kutumia Sheria. Kwa hiyo, mimi ni mlipa fidia kwa waathirika. Kama hamstahili fidia, Serikali haiwezi kupilisha hela kwa Wizara kulipa fidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi hawa (*TANROADS*) ndio walipa fidia, ninyi wenyewe hamtapitisha fedha hapa ya kulipa fidia kwa jambo ambalo halistahili fidia. Kwa hiyo, jambo hili ingekuwa kuna fidia imekwama kwangu imeletwa, lakini haijafikishwa kwa mwenyewe, ndiyo mngeshika shilingi. Fidia haijaja kwangu kwa sababu sistahili kupata hizi fedha kuwalipa huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ushauri wangu ni mambo mawili. Kama kuna kesi, mmepata faida hapa, Mheshimiwa Halima dada yangu ni Mwanasheria na ame-*practice* sheria ndani ya Serikali, anajua; amekuwa Mwanasheria wa Serikali yeye. Kama kweli kuna hukumu ambayo mlisindwa, mmepata faida, hamjachelewa. Hata namna ya kurudisha kesi ilioisha muda, kukata rufaa mnajua. Vile vile juzi mmetunga Sheria nyingine na kuanzisha Bodi ya Fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema ni kwamba Wizara ya Ardhi haiwajibiki na kulipa fidia kwa jambo hili kwa sababu hatujapata fedha za kulipa fidia kwa sababu jambo lenyewe halilipiki fidia, halina sifa ya kupata fidia. Tutakapowezesha kupata sifa ya kulipa fidia, fedha zitakuja kwangu, nitalipa fidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sasa naomba tu kwa sababu Serikali ni moja, mimi kwa kweli naunga mkono maelezo ya Manaibu Waziri kwa sababu hawa ni Wahandisi waliofanya kazi ya *TANROADS* na yule ndio anawakilisha *TANROADS*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hili mimi halinihu sana. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kama hujaridhika nalihoji Bunge. Ameshatoa hoja, mimi nalihoji Bunge.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mujibu wa taratibu za Bunge, Bunge lihojiwe kwa suala hili.

**MWENYEKITI:** Sawa, ulishatoa hoja ndiyo maana nasema sasa nitalihoji Bunge kuhusu hoja yako, kama Bunge linakubali au kukataa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Hoja imekataliwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Soni. (*Makofi*)

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi pia na mchango wa kuongea hapo mapema, nilikuwa nimeombia Serikali kwa kupitia Wizara ya Ardhi iangalie namna; kwanza niwapongeze kwamba tayari wana mpango wa kuleta vifaa

kwenye Kanda. Nipongeze kwa jambo hilo kubwa, lakini anasema awamu ya pili ndiyo wataleta hivyo vifaa katika ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie namna, pawe na *program*, Halmashauri tupatiwe vifaa hivyo sasa hivi kwa sababu *program* ya mwaka mmoja baadaye kwenye bajeti inayokuja, hatutapata hivyo vifaa; na ndani ya mwaka kazi ya kupima inaweza kufanyika kubwa kabisa na inaweza kukaribia kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ituwekee dhamana kwamba kampuni inayotengeneza hivi vifaa au inayouza vifaa au itupatie namna ituwekee *guarantee* ili tukope kwa sababu Halmashauri nyingi hazina uwezo wa shilingi milioni kama 200 au 300, lakini Wizara ilipie gharama za *satellite imaging* ili hivi vifaa vinapotumika, tuweze kuona zile *satellite images*. Ukiwa na zile *satellite images* utaweza kupima ardhi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, viwanja vilivyopimwa Babati, leo vina mgogoro mkubwa kwa sababu tulipima bila kutumia vifaa hivyo na *satelite imaging* unakuta kiwanja chako kipo korongoni, kipo juu ya mlima kwa sababu wanatumia ramani hizi za *topography* za zamani, lakini tukienda na huu mfumo wa kisasa, Wizara ikalipia *satellite imaging* na tukakopeshwa hivi vifaa pamoja na vifaa vya kutolea hati, kwa mfano *computers, printer* na za kuwekea *data*, utakuta sehemu kubwa ya matatizo haya ya kupatiwa hatimiliki...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa umeleweka.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara itupe uhakika: Je, inaweza kufanya hivyo ili Halmashauri zote mwaka huu kuanzia sasa badala ya kusubiri awamu ijayo ya bajeti?

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

## WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA

**MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeagiza vifaa hivi *RTK* tulikuwa tunakwama zamani kupima kwa sababu vifaa vyote vya zamani tulikuwa tunahitaji hizo *satellite image*, hivi havihitaji. Ndiyo maana tumewe *link* kila mahali za *satellite straight*. Kwa hiyo, *technology* hii inayokuja ni tofauti, ndiyo maana nimewaalika Waheshimiwa Wabunge, kule nyuma vifaa hivi viro. Ungeenda kuviona vile, swali hili pengine usingeuliza.

Mheshimiwa mwenyekiti, habari ya *satellite image* ni *very expensive*, hata sisi imetukwamisha, hatuwezi. Upimaji wa mashamba umekwama sana kwa sababu lazima *satellite*; tumejitahidi hata ku-*download* kwenye *Google* na nini, ni *very expensive!* Hivi vifaa vina uwezo vyenyewe huhitaji tena *satellite image* na ndiyo maana vinapima mpaka ekari elfu 30 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumetafuta *technology* mpya na yeoyote ambaye anataka kuthibitisha angalau kidogo kuona jinsi vinyofanya kazi, tunamwalika pale nyuma, Makampuni haya yako pale. Tunanunua sasa vya kutosha kwenye Kanda ili kila Halmashauri ikodishe pale bure, ikapimie, lakini baadaye tunaandika sasa mradi wa pili ambao pesa tunazo, tunataka tununulie kila Halmashauri vifaa hivi na tutawapa bure wakati tunawa-*train*. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Mmasi. Hukutoa hoja Mheshimiwa Jitu? Haya tunaendelea na Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimepata ukakasi kidogo kwenye fungu la maendeleo *Vote number 48* kwa bajeti hii ya Wizara ya Ardhi kwa mwaka huu unaoishia 30 Juni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia fungu hili la maendeleo tunaona kabisa Wizara ilitengewa Sh.25,300,000,000/=, ni sawa na 4% ya bajeti nzima ya Wizara hii. Pia katika tengeo hili tumeona kulikuwa na tengeo la

shilingi bilioni 13 ambapo katika hizi ulikuwa umetengewa mradi ule wa *Land Tenure Support System* ambapo katika hizi shilingi bilioni 13, shilingi bilioni 10 zilitokuwa ni fedha kutoka nje ya nchi, yaani fedha za wahisani lakini katika hiyo shilingi bilioni 10 zilitoka Sh.3,400,000,000/=. Siyo hivyo tu, katika teneo hili tuliona fedha za ndani zilitengwa shilingi bilioni tatu lakini zilizoenda kwenye matumizi mpaka Mei, 2017 ni shilingi milioni 400 tu, katika shilingi bilioni tatu ambayo ni sawa na asilimia 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tukiangalia, ukakasi huu umepelekea miradi mingi ya Wizara kukwama. Mathalani, katika bajeti hii ya Wizara ya Ardhi, walikuwa wamejitengea kwa mwaka huu waweze kutoa hatimiliki za makazi 400,000 lakini wameishia kutoa hatimiliki za makazi 39,779.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, walikuwa wamejipanga kutoa Hati za Kimila 57,000, lakini mpaka sasa hakuna hata hati ya kimila iliyotoka, tunaambiwa kuititia *report* ya Kamati Wizara imeweza kuratibu hati 33,000...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelekezo ya Serikali ni kwa nini Serikali isione umuhimu wa kutenga fedha za ndani ili akinamama waweze kukopesheka katika mabenki kuititia miradi hii ya urasimishaji wa ardhi, lakini pia suala la ardhi ni suala nyeti sana...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Mtoa hoja.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya kina. Kwa kweli nitakuwa mchawi kama nitashika mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umemaliza muda wako.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Ahsante. (*Makofî/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishatoa hoja wakati nawasilisha hapa nilisema msiangalie bajeti yangu kwa takwimu hizi za shilingi bilioni 68, mimi nina hela nyingine hapa na ndiyo maana kazi inaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechukua na magazeti hapa, ukiangalia kurasa zilizomo humu, matangazo yote Wizara ya Ardhi kuna mabilioni hapa, kazi inaendelea. Kwa hiyo, niliwaambia kuna miradi inayoendelea ya kuboresha Sekta ya Ardhi ikiwa ni pamoja na upangaji na upimaji huo unaosema wa *Land Tenure*. Hatuwezi kuchukua pesa zote Hazina tukakaa nazo, tunafanya kazi halafu tunaomba pesa. Hata yule Balozi amekuja jana, fedha zote zipo Tanzania, lakini hatuwezi kuzipeleka kwenye *account* hili mpaka tufanye kazi. Kwa hiyo, pesa tunayo, usiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba fedha nyingi sana za maboresho ya sekta hii ziko kwenye mradi wa *World Bank* ambapo fedha zile ziko Tanzania hivi sasa. Tunafanya kwa awamu kila tunapotangaza tenda ya kazi fulani fedha zinatoka na ushahidi wa Magazeti ni huu. Hata hivyo, yaliyosababisha kutokufikia malengo ya kupima na kupanga hati hizi, siyo haya peke yake, mengine ni matatizo ya ndani. Wananchi wale hata viwanja viliviyopangwa na kupimwa havinunuliki, bei ni kubwa na gharama za kupima ni kubwa. Kwa hiyo, sisi tumeenda kwenye *source*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya kupima kwa sababu wapimaji binafsi hawana vifaa, wapimaji wa Serikali hawana vifaa, tuwanunulie vifaa. Tunamwaga vifaa. Ukipima na kupanga kiwanja pamoja na orodha yote hiyo ya kodi, lakini tozo ilikuwa inachukua asilimia 67, tumepunguza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafikiri kwamba mfanyabiashara yejote anayepata faida ni yule anayeuzwa bidhaa nyingi sana kwa faida ndogo ndogo lakini anapata

faida. Kwa hiyo, nasi tumekwenda kibashara zaidi, kwamba hebu tupange, tumilikishe kwa gharama ndogo lakini wamiliki watu wengi zaidi, tutapata fedha ya Serikali lakini kwa sababu watakaomiliki hata ingekuwa bure, kila mwaka wataendelea kulipa kodi ya Serikali. Tumeongeza wigo wa walipa kodi wa Serikali.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi, kuna fedha hujaziona humu, nakualika Ofisini kwangu na nitakuelekeza vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Kwa kutumia Kanuni ya tano (5) na kwa kuzingatia muda wa ibada, tayari tunaingia kwenye *guillotine*.

#### **Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1001 - <i>Administration and HR Mg'nt</i> .....Sh. 6,736,586,549/=
Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts</i> .....Sh. 848,465,000/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning</i> .....Sh. 696,730,000/=
Kif. 1004 - <i>Management Information Syst</i> .....Sh. 718,244,000/=
Kif. 1005 - <i>Internal Audit Unit</i> .....Sh. 350,066,000/=
Kif. 1006 - <i>Procurement Mg'nt Unit</i> .....Sh. 283,944,000/=
Kif. 1007 - <i>Gov't Communication Unit</i> .....Sh. 395,910,000/=
Kif. 1008 - <i>Legal Service Unit</i> .....Sh. 319,870,000/=
Kif. 2001 - <i>Land Administration Division</i> .....Sh. 13,790,040,000/=
Kif. 2002 - <i>Survey and Mapping Division</i> .....Sh. 3,995,954,000/=
Kif. 2003 - <i>Registration of Titles Unit</i> .....Sh. 960,226,000/=
Kif. 2004 - <i>Valuation Unit</i> .....Sh. 884,859,000/=
Kif. 2005 - <i>Dar es Salaam Zone</i> .....Sh. 446,760,000/=
Kif. 2006 - <i>Eastern Zone</i> .....Sh. 0/=
Kif. 2007 - <i>Central Zone</i> .....Sh. 449,010,000/=
Kif. 2008 - <i>Western Zone</i> .....Sh. 282,040,000/=
Kif. 2009 - <i>Lake Zone</i> .....Sh. 492,590,000/=
Kif. 2010 - <i>Northern Zone</i> .....Sh. 485,080,000/=
Kif. 2011 - <i>Southern Zone</i> .....Sh. 314,800,000/=
Kif. 2012 - <i>Southern Highlands Zone</i> .....Sh. 326,600,000/=
Kif. 2013 - <i>Simiyu Zone</i> .....Sh. 369,120,000/=
Kif. 3001 - <i>Rural and Town Planning Div</i> .....Sh. 3,964,556,609/=

Kif. 3002 - *Housing Division*.....Sh. 1,929,513,768/=  
Kif. 3003 - *District Land &Housing Trib.Unit*...Sh. 4,214,118,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Kif. 1001 - *Finance and Admin. Division*.....Sh. 1,751,692,000/=  
Kif. 1002 - *Planning Unit*.....Sh. 37,640,000/=  
Kif. 1003 - *Procurement and Mg'nt Unit*.....Sh. 18,240,000/=  
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 22,740,000/=  
Kif. 1005 - *Legal Service*.....Sh. 19,440,000/=  
Kif. 2001 - *Physical Planning Division*.....Sh. 134,140,000/=  
Kif. 2002 - *Landuse Coord, Communication and Policy Division*.....Sh. 66,290,000/=  
Kif. 2003 - *Research and Documentation*.....Sh. 65,190,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgnt*.....Sh. 1,100,000,000/=  
Kif. 2001 - *Land Administration Division*.....Sh. 20,000,000,000/=  
Kif. 2002 - *Survey and Mapping Division*.....Sh. 4,000,000,000/=  
Kif. 3001 - *Rural and Town Planning Division*.....Sh. 0/=  
Kif. 3002 - *Housing Division*.....Sh. 300,000,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**NDG. LAWRENCE MAKIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja taarifa.  
*(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono na imekubaliwa. Kwa hiyo, natangaza rasmi kwamba bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi 2017/2018 imepita na imepitishwa na Bunge hili. Kwa hiyo, nachukua fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu yao nzima ya Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya. Naamini kwamba Wizara nyingine zitafanya hivyo na zipongezwe.

Waheshimiwa Wabunge, hapa nina matangazo mawili, kwanza moja linatoka kwa Mheshimiwa Balozi Adadi, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuwa kile kikao kilichokuwa kifanyike leo saa 8.30 kimeahirishwa.

Tangazo la pili, ni kutoka kwa Meneja wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa John Kadutu anasema kesho asubuhi anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa kutakuwa na mchezo kati ya timu ya Bunge na *Azam Staff*

kabla ya mchezo wa Simba na Mbao; na pia anasema tiketi za mchezo wa Simba na Mbao zinapatikana *Canteen* kwa Nyange. Wote mnaarifiwa hilo tangazo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo...

**MBUNGE FULANI:** Hawalipii hizo tiketi?

**MWENYEKITI:** Hawalipii? Ni tangazo kwamba zinauzwa hizo tiketi.

Jamani Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kumaliza vizuri Wizara ya Ardhi, nami niwatakiele Watanzania wote kila la heri na baraka zote kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani na pia Mwenyezi Mungu atujaalie sisi ambao tutafunga tupokelewe funga zetu na tuweze kupata malipo mema. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana. Naahirisha Bunge hadi tarehe 29 Mei, 2017 siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.30 mchana Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatatu Tarehe 29 Mei, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*